ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR
MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ziwani.
9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge

10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa
11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando
13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa.
14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi
18. Mhe. Shawana Bukheti Hassan	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/ Jimbo la Dole
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu

22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Mpendae
30.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
31.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
32. Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa
33.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
34.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
35. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
36.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake

37. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
38.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
43.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
44.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
45.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
46.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
47.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
48.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
49.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
50.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
51.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
52.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
53.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
54.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	Jimbo la Kiembesamaki
55.Mhe. Marina Joel Thomas	Kateuliwa na Rais
56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
57.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake
58.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini

59.Mhe. Mohammed Haji Khalid Jimbo la Mtambile

60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad Jimbo la Chambani

61.Mhe. Mussa Ali Hassan Jimbo la Koani

62.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali Jimbo la Uzini

63.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa Nafasi za Wanawake

64.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi Nafasi za Wanawake

65.Mhe. Nassor Salim Ali Jimbo la Rahaleo

66.Mhe. Omar Ali Shehe Jimbo la Chake-Chake

67.Mhe. Panya Ali Abdalla Nafasi za Wanawake

68.Mhe. Raya Suleiman Hamad Nafasi za Wanawake

69.Mhe. Rufai Said Rufai Jimbo la Tumbe

70.Mhe. Saleh Nassor Juma Jimbo la Wawi

71.Mhe. Salim Abdalla Hamad Jimbo la Mtambwe

72.Mhe. Salma Mohammed Ali Nafasi za Wanawake

73.Mhe. Salma Mussa Bilali Nafasi za Wanawake

74.Mhe. Salmin Awadh Salmin Jimbo la Magomeni

75.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman Nafasi za Wanawake

76.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha Jimbo la Mwanakwerekwe
77.Mhe. Subeit Khamis Faki Jimbo la Micheweni
78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis Jimbo la Konde
79.Mhe. Ussi Jecha Simai Jimbo la Chaani
80.Mhe. Viwe Khamis Abdalla Nafasi za Wanawake
81.Mhe. Wanu Hafidh Ameir Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Ishirini na Tisa – Tarehe 24 Julai, 2013

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba sasa kuwasilisha hati mezani juu ya Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka 2013/2014. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Abdalla Moh'd Ali (Makamo Mwenyekiti wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari): Mhe. Spika, naomba kuweka hati mezani ya Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka 2013/2014. Naomba kuwasilisha.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Mwaka 2013/2014 – Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe kama tulivyokubaliana jana kwamba leo tukiingia tunaanza na majumuisho. Kwa hivyo, nimpe nafasi Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, kwanza kabisa nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia leo hii ikiwa tumo kwenye Mfungo wa Ramadhani mwezi 15. Vile vile Mhe. Spika, nianze kwa kumpongeza Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kwa kuweza kunipa mashirikiano ya pamoja kwenye kazi zetu za Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo. Mhe. Spika, pia nisimsahau Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari na Naibu Katibu Mkuu pamoja na watendaji wake wote.

Vile vile nisimsahau Afisa Mdhamini Pemba pamoja na watendaji wake kwa kuweza kunipa mashirikiano kwenye kazi zetu tunazozifanya tukiwa kisiwani Pemba. Mhe. Spika, pia niwapongeze Wanawake wa Mkoa wa Kaskazini Pemba kwa kunipa mashirikiano ya pamoja kwa kuweza kutekeleza majukumu yangu ya serikali pamoja na ya chama.

Mhe. Spika, kwanza kabisa nianze kwa kuwataka Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi waweze kutupitishia bajeti yetu hii ambayo ni ya Wizara ya Habari. Kama wanavyojua kuwa Wizara hii ni kubwa na ina majukumu mengi, hivyo waweze kuipitisha ili tuweze kutekeleza majukumu yetu kwa ufanisi zaidi.

Mhe. Spika, niingie kwenye kujibu hoja za Wajumbe kwenye Tume ya Utangazaji. Mhe. Viwe Khamis Abdalla, Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa na Mhe. Salim Abdalla Ali.

Mhe. Spika, hoja ya Mhe. Viwe ni kuwa mfumo wa *digital* unatoa fursa ya kupata vipindi vingi na kwa kuwa uzalishaji wa vipindi vya ndani ni mdogo, vipindi vingi vinavyooneshwa inabidi ni kutoka nje ya nchi. Hata hivyo, *digital* imewezesha utumiaji wa mchango mkubwa ili kuweza kuendeleza vipindi mbali mbali ambavyo mna vipindi vya dini, vipindi vinavyohusiana na mila na desturi ya Kizanzibari. Mhe. Viwe kwa kweli alichangia michango hiyo na akaelekeza upande wangu nikiwa Naibu Waziri wa Habari ili kuweka vipindi maalum kwenye *ZBC* ili kuelimisha jamii kuhusu mila na desturi za Kizanzibari.

Mhe. Viwe nikiwa Naibu Waziri wa Wizara hii kipindi hiki cha miaka miwili na nusu iliyobakia nakuomba sana, kwa sababu mwanamke mwenzangu na ni kijana tuweze kufanya kipindi kinachohusiana na mila na desturi ya Kizanzibari. Mhe. Viwe nakuomba sana tuwe pamoja na tuwe na mashirikiano ya pamoja.

Mhe. Spika, sasa niende kwa Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa juu ya hoja yake aliyoitoa kuhusu Tume ya Utangazaji. Kuwepo na mkataba wa kuingiza matangazo ya *ZBC* kwenye *Star Times*, *ZCTV* na kadhalika. Wizara inaangalia uwezekano wa kuliweka kwenye kanuni za utangazaji kama miongoni mwa sheria ya kupewa leseni mwenye kituo cha kuingia na kurusha matangazo ya *ZBC*. Mhe Mahmoud na wewe nakutaka kwa heshima na taadhima nakuomba sana bajeti yetu uipitishe ili tushirikiane pamoja kwenye Wizara hii.

Sasa niende kwa Mhe. Salim Abdalla Hamad, kama alivyoeleza hoja yake katika kufikia kiwango kizuri cha teknolojia ya habari je, tunahisi taaluma iliyotolewa inatosheleza? Mheshimiwa kwa kweli taaluma inatosheleza lakini pia nakuomba sana Mhe. Salim tuwe pamoja ili taaluma iliyotolewa iweze kuelimisha jamii ambayo tunakaa nayo, na wewe uweze kuitoa taaluma hii ili wananchi wetu wafahamu zaidi kuhusu mfumo huu wa *digital*.

Mhe. Salim nakuomba sana kwa heshima na taadhima ili uipitishe bajeti hii tuweze kushirikiana pamoja kwenye utekelezaji wa majukumu yetu. Mhe. Salim Abdalla nakuomba sana.

Mhe. Spika, pia niende kwa Mhe. Saleh Nassor Juma. Jana Mhe. Saleh alizungumza kwa ghadhabu kubwa, lakini namuomba Mheshimiwa ajue kwamba waandishi wetu wa habari wanafanya kazi vizuri na wanatekeleza majukumu yao. Kama alivyoeleza kwa ghadhabu namuomba Mhe. Saleh awe pamoja na waandishi wa habari ili kushirikiana katika kufanya kazi wakati wote ule.

Mhe. Saleh kwa kweli ni hatua moja wapo aliyoizungumza ya kuhusu malalamiko juu ya waaandishi wetu wa habari, waandishi wetu huwa wanatoa taarifa ya habari na wanaeleza taarifa vizuri na wanaanzia kama ni Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kama ni Makamu wa Pili, kama ni Makamu wa Kwanza huwa kuna vibwagizo ajue hilo.

Kwanza Mheshimiwa nataka nimwambie waandishi wa habari huwa wanamuheshimu Kiongozi yoyote yule anayekuwa na *function* yake, na kuna vibwagizo na lazima tuangalie kuna vibwagizo vya mwisho hata sisi Waheshimiwa tunapofanya *function* huwa waandishi wa habari wanakuja kwenye vibwagizo vya mwisho atakwambia Bi Hindi amesema hivi, sasa tusione kama viongozi wetu wanadhalilishwa vile ni vibwagizo vya waandishi wa habari. Lakini nataka nimhakikishie Mhe. Saleh awe pamoja na waandishi wa habari na mimi leo nikiwa Naibu Waziri wa Habari ninamuomba kwa heshima na taadhima awasamehe waandishi wetu wa habari, kubwa ni kuwaelekeza na kuwastahamilia na sio kusimama hapa Waheshimiwa mkasema kama *ZBC* inaajiri wana maskani. Hilo mimi nalikataa kwa sababu sote ni wanasiasa, siasa ina fani yake na *ZBC* ina fani yake, na sisi tukiwa ni wanasiasa tumeingia humu kwa fani yetu ya siasa na wenye taaluma wameingia kwa fani yao ya taaluma, sasa kwa kweli tunaposimama kwenye majukwaa tuweze kusema mambo ambayo ni mazuri na yanayoheshimika kwenye nchi yetu.

Mhe. Saleh Nassor nakuomba sana juu ya majibu yangu niliyokujibu basi uweze kuipitisha bajeti yetu ili tuweze kufanya kazi za kuendeleza nchi yetu pamoja na vyombo vya habari.

Mhe. Spika, niende kwa Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi. Nakiri kwamba Mhe. Mwanajuma Faki aliniuliza swali nikamjibu na nikamwambia Mheshimiwa nitakuja nije nikutane na timu zako, lakini nataka nikuhakikishie Mhe. Mjumbe kwamba nakuomba sana ujitayarishe na mimi nijitayarishe ili timu zako tuje tukae pamoja tuweze kuzungumza nazo na kuweza kuwapa kile tulichonacho baina ya mimi na wewe.

Mheshimiwa nataka nimwambie niko tayari kufanya kazi na wanawake wenzangu wakati wowote ule. Mhe. Mwanajuma nakuomba tena uipitishe bajeti yetu ukiwa mwanamke mwenzangu tuweze kutekeleza majukumu yetu.

Mhe. Spika, kwa niaba ya wanawake wenzangu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba naiunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, nakushukuru kunipa nafasi ya kusimama hapa siku ya leo ya Jumatano, mwezi 15 Ramadhani. Kwa kweli tupo kati kati ya Mwezi wa Ibada kubwa katika kalenda ya Wananchi wa Zanzibar, hili ni kumi la Maghfira na naomba nilikumbushe hilo kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ili nami nitarajie malipo ya ukumbusho huo. Tumeambiwa, *"Ballighuu anniy Walau-aaya"*.

Mhe. Spika, kwa niaba ya viongozi na wafanyakazi wote wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo naomba kukushukuru wewe kwa kuliongoza vizuri Baraza letu na pia kwa namna ulivyosimamia mjadala wa Baraza hili katika Bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo. Naomba uniruhusu niwapongeze Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza kwa namna walivyojadili bajeti ya wizara yangu, nimefurahi sana kwamba Wajumbe walitoa michango yao kwa kujenga zaidi, kwa kunielekeza kwa lengo la kufikia ufanisi wa taasisi zote zilizomo ndani ya wizara yangu. Nawashukuru wote.

Mhe. Spika, naomba nitambue kwamba bajeti ya Wizara yangu mwaka huu imechangiwa na Wajumbe 32; kati ya hao Wajumbe 21 wamechangia moja kwa moja kwa kusema na Wajumbe 11 wamechangia kwa maandishi. Kwa ruhusa yako naomba niwataje Waheshimiwa Wajumbe hao kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Mlinde Mabrouk Juma

2. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
3. Mhe. Saleh Nassor Juma
4. Mhe. Ismail Jussa Ladhu
5. Mhe. Salim Abdalla Hamad
6. Mhe. Salmin Awadh Salmin
7. Mhe. Wanu Hafidh Ameir
8. Mhe. Viwe Khamis Abdalla
9. Mhe. Hassan Hamad Omar
10. Mhe. Hija Hassan Hija
11. Mhe. Asha Bakari Makame
12. Mhe. Hamza Hassan Juma
13. Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi
14. Mhe. Mohammed Haji Khalid
15. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa
16. Mhe. Salma Mohammed Ali
17. Mhe. Panya Ali Abdalla
18. Mhe. Nassor Salim Ali
19. Mhe. Haji Faki Shaali (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum)
20. Mhe. Mussa Ali Hassan
21. Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo.

Waliochangia kwa maandishi ni:

1. Mhe. Ashura Sharif Ali
2. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu
3. Mhe. Mwanaid Kassim Mussa
4. Mhe. Suleiman Hemed Khamis
5. Mhe. Hamad Masoud Hamad
6. Mhe. Fatma Mbarouk Said
7. Mhe. Subeit Khamis Faki
8. Mhe. Bikame Yussuf Hamad
9. Mhe. Farida Amour Mohammed
10. Mhe. Nassor Salim Ali alichangia tena kwa maandishi
11. Mhe. Rufai Said Rufai
12. Mhe. Sahdya Mohamed Suleiman

Mhe. Spika, kama kuna Mjumbe yeyote ambaye nimemsahau naomba tukumbushane, sikukusudia, lakini kwa jumla Mhe. Spika, nawashukuru sana Wajumbe hao kwa michango yao.

Mhe. Spika, nianze na hoja ya Mhe. Mlinde Mabrouk, Mwenyekiti wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari ambaye alianza na Taasisi ya Gazeti

la Zanzibar Leo na pia nitawajibu Waheshimiwa wengine waliozungumzia hoja hiyo ambao ni Mhe. Saleh Nassor Juma, Mhe. Fatma Mbarouk Said, Mhe. Hassan Hamad Omar, na Mhe. Mohammed Haji Khalid.

Mhe. Mlinde alizungumzia suala la Kamisheni ya Utalii, na katika kumjibu Mhe. Spika, nitaomba niwajibu na Waheshimiwa wengine kama hivyo nilivyozungumza. Kwanza nimshukuru Mhe. Mlinde kwa ushauri wake aliyotupa na nimhakikishie kwamba maelezo yake aliyotupa kwenye utekelezaji wa dhana ya Utalii kwa wote kujidhatiti katika kuutangaza utalii ni kuangalia ni vipi tutafikia katika kupunguza viingilio kwa wazawa katika vivutio vya kitalii tunalifanyia kazi, tutaijibu kamati yake kwa sababu Wizara yangu inawajibika na kamati yake.

Kuhusu fedha zilizopangwa kuchangwa kuwa ni sawa na za mwaka jana. Hii ni kutokana na kutofikiwa kwa malengo hayo kwa mwaka jana. Hivyo tumeona kwa vile mwaka jana hatukuyafika malengo hayo tumeona bora tuyapange tena ili tujitahidi kuyafikia tukijaaliwa.

Mhe. Spika, Mhe. Mwenyekiti alizungumzia masuala mengi hasa masuala yanayohusiana na suala la Shirika la Magazeti. Katika suala hili alishauri serikali kutafuta njia za kulitafutia Shirika fungu la kununulia mitambo kwa kuchapisha magazeti yake hapa hapa Zanzibar badala ya kuchapisha Dar es Salaam suala ambalo pia lilichangiwa na Mhe. Saleh Nassor Juma.

Naomba kueleza kwamba, wizara imeuchukua ushauri huu na tutaendelea kuufanyia kazi ili kutafuta njia za kulipatia Shirika mtambo wa kuchapishia magazeti yake hapa hapa Zanzibar kwa vile hilo ni jambo muafaka na muhimu kwa maendeleo ya Shirika, kwani ni kweli uchapishaji magazeti Dar es Salaam mbali ya kuwa ni gharama kubwa pia hauleti taswira nzuri. Kwani Shirika hulazimika kulipeleka mapema na hata kukosa habari zilizofanyika nchini usiku wa mapema.

Mhe. Spika, napenda kuliarifu Baraza lako tukufu kwamba kwa sasa Shirika haliwezi kuchapisha magazeti yake hapa Zanzibar kwani hakuna hata kiwanda kimoja kinachochapisha magazeti; na viwanda vinavyodhaniwa kuchapisha magazeti ambayo huchapisha kalenda za taasisi mbali mbali havina mitambo ya kitaalamu ya kuchapisha magazeti, kwani magazeti huchapishwa na mitambo ya *Web offset* inayotumia karatasi za mzunguko ambayo huchapisha kwa karatasi za *sheet* ambazo gharama zake huwa ni kubwa na *process* yake kwa magazeti ya kila siku haiwezekani, kwani kasi yake ni ndogo kwa vile karatasi hulazimika kugeuzwageuzwa.

Mhe. Spika, niombe pia niitoe wasiwasi Kamati ya Baraza lako tukufu kuhusiana na mashaka waliyonayo ya kuongezeka kwa mishahara ya wafanyakazi kwa Shirika ikilinganishwa na mwaka jana. Aidha, ufafanuzi huo Mhe. Spika, nitakuwa pia najumuisha na Mhe. Fatma Mbarouk Said wa Jimbo la Amani.

Mhe. Spika, kuongezeka mishahara hiyo kama ilivyosomeka katika kitabu ni kwa kawaida, lakini kwa vile haikufafanuliwa katika kitabu ndio maana ikaonekana kama imepanda. Hivyo napenda kutoa ufafanuzi zaidi kuondoa utata huo kama ifuatavyo:-

Tofauti ya fedha za mwaka 2012/2013 mishahara ya mwaka wa fedha 2014 kwa taasisi zote za serikali imechanganywa na posho ambazo zinakwenda sambamba na mishahara, ambazo katika miaka iliyopita zilikuwa zikisomeka kama posho. Kwa maana hiyo, jumla ya shilingi 49,911,586 ambazo ni posho ziko ndani ya mishahara hiyo ikiwemo mchango wa asilimia kumi wa Shirika kwa wafanyakazi wa *ZSSF*.

Pili, jumla ya shilingi 5,214,000 za mishahara zimeongezeka ambazo ni ongezeko la mishahara za wafanyakazi waliorudi masomoni ambao baada ya kuongezeka kiwango chao cha elimu mishahara yao imepanda kwa mujibu wa viwango vilivyotolewa na Tume ya Utumishi serikalini. Wafanyakazi hao ni 6 akiwemo 1 mwenye *Master*, 1 mwenye *First degree*, 4 diploma, mmoja alikuwa likizo bila ya malipo ambaye anarudi kazini mwaka huu na ambaye pia ana Shahada ya pili.

Tatu, mishahara hiyo ni ongezeko la shilingi 78,720,000 kwa mwaka ambayo ni kwa wafanyakazi wapya 14 walio katika mchakato wa kuajiriwa kupitia Bodi ya Shirika hilo, pamoja na wafanyakazi watano ambao wanajaza nafasi za wafanyakazi waliohamishwa katika Shirika hilo na kupangiwa kazi katika taasisi nyengine.

Nne, ni posho la Naibu Mhariri Mtendaji ambaye katika kipindi kilichopita hakuwepo katika Shirika ambapo kwa jumla ya shilingi 11,340,000.

Mhe. Spika, kuhusu hoja iliyotolewa na Mhe. Saleh Nassor kuhusiana na kutayarishwa gazeti maalum litalotumia maandiko ya nukta nundu kwa ndugu zetu wasioona ni jambo muhimu na zuri, ila kwa vile kwa sasa hapajapatikana teknolojia hiyo hatua zinachukuliwa kuingiza magazeti yetu katika redio mbali mbali za serikali na za binafsi ili ndugu zetu wasioona wapate taarifa hadi teknolojia hiyo katika magazeti itapovumbuliwa.

Kuhusu gharama ya mtambo wa kisasa wa gazeti ni kama shilingi bilioni tatu. Jitihada binafsi za kuonana na Balozi mdogo wa China kuhusiana na suala hili nimezichukua na bado mazungumzo baina yangu na yeye yanaendelea.

Mhe. Spika, kuhusu hoja ya Mhe. Hassan Hamad Omar kuhusiana na watu kusoma magazeti na kisha kuyatumia visivyo kwa kufungia samaki au maandazi hilo si jambo zuri, na tunaahidi kuendelea kutoa taaluma kwa wananchi kupitia Gazeti la Zanzibar Leo. Ijapokuwa mtu kufanya hivyo ni haki yake kwa vile tayari gazeti hilo ameshasoma na kulilipia. Hata hivyo, shirika linaendelea kuhifadhi matoleo yote ya magazeti yake kwa njia ya karatasi na kwenye kompyuta ili kusaidia wananchi wanaotaka kufanya utafiti au marejeo ya masuala yaliyoripotiwa na magazeti hayo kwa Ofisi za Unguja na Pemba.

Kuhusiana na kutokuwepo kwa magazeti katika eneo la njia nne za Madenjani, Magazeti ya Zanzibar Leo yalikuwa yakipelekwa na kuuzwa na Ndugu Ali Abdalla Nassir ambaye alisema kuwa magazeti hayo yasipelekwe na wasomaji wanadai wapelekewe magazeti ya Tanzania Bara hususan magazeti ya udaku wakati sisi hatufanyi biashara hiyo, na hivyo tukalazimika kuhamishia kituo cha Mchangamdogo sokoni katika duka la madawa kwa Babu Ali Hamad kwa majaribio ambako ni sehemu ya Jimbo hilo hilo la Kojani. Baada ya ushauri wa muuzaji huyo nako pia ikiwa magazeti yatakuwa hayanunuliwi yatahamishiwa kwengine ikizingatiwa kuwa magazeti ni biashara hivyo yanafuata wateja.

Mhe. Spika, kuhusu hoja ya Mhe. Mohammed Haji Khalid ya kusimamiwa kwa mafunzo ya wafanyakazi wa Shirika ni ushauri muhimu na napenda kumhakikishia Mhe. Mohammed na Baraza lako tukufu kwamba litafanyiwa kazi kama ilivyopangwa ili kuinua viwango vya utendaji kazi wa Shirika.

Kuhusiana na suala la kuomba radhi kunapotokea makosa Shirika limekuwa likifanya hivyo ambapo katika matoleo yake kadhaa tumekuwa tukishuhudia, lakini binafsi nimuombe radhi sana Mhe. Mohammed Haji Khalid kwa kupewa chama ambacho si chake na Jimbo ambalo si lake. Hata hivyo, naomba nimhakikishie kwamba Shirika litaendelea na utamaduni wa kuomba radhi kila kunapotokea makosa lakini wakati mkubwa tuwe katika umakini wa kuzuia makosa hayo.

Mhe. Spika, tunamshukuru Mhe. Makame Mshimba kwa mchango wake kuhusu faida ya kufanya *promotion* ya utalii nje ya nchi, ni kwamba biashara *itembezwayo ndiyo iuzwayo*. Utalii ni biashara yenye ushindani mkubwa sana, na kwenye soko ndiko kwenye wateja, hivyo ni lazima twende sokoni kwenye

maonesho ya kitalii yanakofanyika tukautangaze utalii wetu, vyenginevyo hatakuja mtu hapa kwetu.

Juzi Mhe. Spika, nilikuwa na wageni ofisini kutoka China nchi ambayo kwa mwaka inatoa nje watalii milioni mia moja, wanasema wao hawajui kabisa kama kuna nchi ya Zanzibar na kama kuna nchi ambayo inatoa utalii mzuri kama huu. Walipokuja walinambia hii ni pepo kwa wao, walikuwa watu 12 nilikuwa na ahadi nao kuzungumza saa kumi jioni. Hata hivyo, baada ya kutembea maeneo mbali mbali ya Zanzibar tuliowahi kuzungumza ni watatu tu, wengine wote walibaki maeneo mbali mbali wakifaidi hali ya Utalii wetu. Kwa hivyo, wamenambia lazima twende katika mikoa yote ya China sisi wenyewe ili tukautangaze utalii wetu. Kwa hivyo, kuna umuhimu mkubwa wa kutangaza utalii nje ya nchi.

Mhe. Makame Mshimba alizungumzia hoja ya watembezaji wageni *Tour Operators.* Mhe. Spika, *Tour Operators* kazi yao kubwa ni kutangaza vivutio vyetu nje, kutafuta wageni na kuwatembeza. Kwanza katika hilo wanalipa mapato serikalini na wanaifanya kazi hiyo kwa gharama na ili kulipa gharama zao na kupata fedha ya kulipa kodi serikalini lazima waweke viwango fulani vya bei zao.

Sasa Mhe. Makame Mshimba na Waheshimiwa wengine akinambia niwaruhusu watu wengine ambao hawajagharamia kuleta wageni na wala hawalipii kodi serikalini maana yake ni nini? Moja hawa wasiolipa kodi watatembeza wageni kwa viwango vya chini, athari yake kampuni za *Tour Operator*s zitakufa na zikifa maana yake nchi yetu itapungukiwa na wageni na kodi serikalini nayo itapungua. Sasa kufanya hivyo ni kuua sekta ya Utalii hatuwezi, na baya zaidi ni kinyume na sheria zetu. Ombi langu kwa Mhe. Mshimba na Waheshimiwa wengine tuwashajihishe na kuwasaidia wananchi wetu kujiunga na kujisajili kama ni *Tour Operators.*

Mhe. Spika, kuhusu wageni kutembeza watalii hilo ni kosa, na hii ni kazi ambayo imepangwa kwa Wazanzibari. Kamisheni imeweka vigezo kwanza uwe na taaluma kutoka Chuo kinachotambulika cha mambo ya Utalii na uwe na kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi. Sasa sisi katika Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo hatuna dirisha la kutoa *Zan ID*. Vitambulisho vinatolewa kuanzia kwenye ngazi ya Sheha kwa hivyo, ni jukumu letu kuhakikisha kwamba vitambulisho hivi havitolewi ovyo ovyo na wasipate ambao si Wazanzibari ili kazi hizi wasizishike na badala yake washike watu wetu.

Mhe. Spika, kuhusu *Venta Club*, serikali imeshughulikia suala hili na kuna kamati ya kulishughulikia suala hili na ripoti yake imewasilishwa katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais tusubiri maelekezo ya ripoti yake.

Mhe. Spika, Mhe. Salmin Awadh alizungumza suala la takwimu za watalii wanaoingia nchini. Ni kweli hilo ni upungufu tumelifanya na nimewaagiza watendaji wangu waniandalie na nafurahi kwamba tayari Waheshimiwa Wajumbe wote washapewa taarifa hii ya *arrival* ya watalii kwa muda mrefu labda miaka kumi nyuma iliyopita. Kwa hivyo, wataweza kulinganisha hali ya watalii wanaokuja kila mwaka.

Mhe. Spika, kuhusu hoja ya Mhe. Wanu Hafidh Ameir aliyetaka kujua jitihada zinazofanywa katika kutangaza utalii wa ndani.

Mhe. Spika kuhusu suala la Utalii wa ndani wizara kupitia idara zake imekuwa ikiandaa shughuli mbali mbali za kushajiisha utalii wa ndani. Miongoni mwa shughuli hizo ni kuandaa ziara kwa wanafunzi katika maeneo ya vituo vya utalii. Aidha, Kamisheni ya Utalii imekuwa ikiendesha mashindano ya utalii ambapo washindi wa mashindano hayo hupata fursa ya kutembelea vivutio mbali mbali vya utalii, kulala katika hoteli za daraja la juu na kuwapatia majarida yanayohusu utalii.

Vile vile katika kushajihisha utalii wa ndani; Kamisheni ya Utalii kwa muda mrefu imekuwa ikiandaa michezo ya jadi kama vile mchezo wa ng'ombe na resi za ngalawa ikiwa na lengo la kurejesha michezo ya asili, ikiwa kama ni kivutio cha watalii na kushajihisha utalii wa ndani.

Mhe. Spika, napenda kumjibu Mhe. Hassan Hamad aliyetaka kujua wazalendo hawafaidiki na nchi yao kwa sababu kila eneo zuri limetengwa kwa Utalii. Mhe. Spika, napenda kumtaarifu Mhe. Hassan Hamad Omar kuwa fukwe na bahari ni mali ya Serikali na tayari tumeshayahifadhi maeneo hayo ni kuundwa kwa Kamati za Utalii za wilaya ambazo katika utekelezaji wa majukumu yake kutakuwa na jukumu la kusimamia matumizi bora ya ardhi yaliyokuwepo katika maeneo hayo.

Mhe. Spika, napenda kuchukua pongezi kutoka kwa Mhe. Salmin Awadh na Mhe. Asha Bakari kuhusiana na suala la Utalii na pia kwa kutusidia katika kuona kwamba kwa kuwa nguvu za kifedha zitatuwezesha kikamisheni ili kuweza kushindana kimataifa katika kuutangaza utalii.

Mhe. Spika, kwa upande wa Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa alitaka kujua vipi watembezaji watalii wanapata taaluma na jinsi gani hutoa maelezo yao

kwa watalii, kwani imebainika kwamba baadhi ya watembezaji hao hutoa maelezo ya kupotosha na sio sahihi, kwamba watembezaji hao hupata taaluma kutokana na vyuo wanavyosoma. Kikawaida Chuo cha Utalii Maruhubi kinatoa mafunzo hayo kwa watembezaji wapya kabla ya kutoa vibali vya utembezaji. Hata hivyo, tunakubali kwamba kuna watembezaji wachache wasio halali tunawaita mapapasi huwa hawana vibali vinavyotolewa na Kamisheni kwa kazi hiyo, na huwa hawajapata mafunzo ya utepembezaji watalii na nafasi ya kusoma historia ya visiwa vyetu. Mhe. Spika, kwa kushirikiana na polisi Kamisheni itaendelea kupambana na kuwasaka watembezaji hao wasiokuwa halali.

Kuhusu malipo ya ziada ya magari yanayochukua watalii wakati magari hayo tayari yana leseni. Mhe. Spika, suala ni kwamba leseni ni kwa ajili ya chombo chenyewe. Lakini *permit* na *sticker* ni kwa ajili ya huduma inayotolewa kwa wakati ule. Hii ni kwa mujibu wa sheria mama inayotolewa kwa wakati ule hii kwa ajili ya sheria mama ya utalii ya mwaka 2009 kifungu namba 15 kinatamka, yoyote anayefanya kazi ya kutoa huduma katika sekta ya utalii kuwa na kibali kinachotoka Kamisheni ya Utalii. Aidha kamati hutoa kumbukumbu kwa mgeni aliyechukuliwa na aina ya gari iliyotoa huduma hiyo ili kurahisisha ufuatiliaji wakati wa matatizo.

Mhe. Spika, kuhusu ushauri wa Mhe. Salma Mohammed kuhusu ushirikishwaji wa kamati za wilaya katika maamuzi ya vitega uchumi ni nzuri na tunaahidi kufanya kazi. Aidha suala la kuwa na kodi moja kwa hoteli baina ya Pemba na Unguja ni kwamba Kamisheni ya Utalii haihusiki na ukusanyaji wa kodi zinazotokana na mahoteli. Kwa hivyo, namuomba hoja yake isubiri wakati wa hoja ya Mhe. Waziri wa Fedha anayehusika na kodi yeye atakuja kujibu vizuri.

Mhe. Mussa Ali Hasssan kuhusu suala la wawekezaji kununua bidhaa za wananchi kwa mkopo. Ni kweli kadhia hii ipo na kwa muda mrefu sana. Hata hivyo, wasambazaji wa bidhaa mahotelini wamekuwa hawazitaarifu Taasisi za Serikali hadi pale matatizo yanapotokea na hivyo huwa hawajulikani nani wamemuuzia. Hata hivyo, wasambazaji hao wameshauriwa kuwa na jumuiya yao itakayosimamia shughuli zao na kuwa na mikataba wakati wa kufanya biashara hiyo. Wawezekaji kununua bidhaa kwa nchi za kigeni Mhe. Spika, suala hili tumelipokea na tutalipeleka katika taasisi husika.

Mhe. Spika, kuhusu suala la wananchi walioajiriwa katika Mahoteli jumla ya Wazanzibari ni 7499, kwa Tanzania Bara 3357 na wageni 603 wameajiriwa katika sehemu tafauti.

Mhe. Spika, napenda kumjibu Mhe. Suleiman Hemed Khamis katika kujua vikwazo vinavyoikabili Wizara kufanya Utalii Zanzibar uwe na bora kiuchumi kama vile katika nchi za Kenya. Mhe. Spika, tatizo kubwa ni fedha za utangazaji tunazopewa. Wenzetu wa Kenya tunaambiwa kwamba wanatumia karibu dola milioni kumi kwa mwaka kwa kutangaza utalii wetu sisi tunapata robo milioni yaani laki mbili na hamsini dola. Sasa katika hali hiyo kwa kweli kuutangaza utalii wetu utakuwa na matatizo.

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Ashura Sharif Ali alitaka kujua tathmini ya uwekezaji Zanzibar imefikia hatua gani. Mhe. Spika, kuhusu suala la utekelezaji litasimamiwa na mamlaka ya kiuchumi Zanzibar. Subiri wizara husika inakuja jibu lako utalipata kwa muafaka.

Kuhusu kunufaika kwa wananchi kiutalii, napenda kumjibu Mhe. Ashura Sharif kama ifuatavyo. Wananchi wanapata nafasi ya kuuza biashara zao Sekta ya Utalii waweza kujiajiri na kuajiri Sekta ya Utalii kupata huduma za kijamii kwa mfano kama huduma za Elimu, afya, Maji na kadhalika.

Kuhusu wananchi kufaidika wanapouza bidhaa zao kwa wawekezaji baada ya kukodisha au kuingia ubia Serikali inatumia vipi suala la ardhi kwa wananchi linapotea. Suala hili linasimamiwa na Wizara inayohusika na Ardhi pamoja na kituo cha uwekezaji. Mhe. Spika, napenda kumpongeza Mhe. Mwanaid Kassim Mussa alituombea na kusema Serikali iongeze fedha za utangazaji kwa lengo la kuimarisha shughuli za Utalii.

Mhe. Spika, Mhe. Makame Mshimba Mbarouk pia alizungumzia nyumba ya Sanaa Mwanakwerekwe. Naomba nimjibu, na wakati nikimjibu pia nitakuwa namjibu Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa, Mhe. Panya Ali Abdalla, Mhe. Suleiman Hemed Khamis kuhusiana na Baraza la Sanaa, Eacrotanal na Baraza la Kiswahili.

Mhe. Spika, Mhe. Makame Mshimba Mbarouk kuhusu nyumba ya Sanaa Mwanakwerekwe kwa sasa inafanyiwa matengenezo ya awamu ya kwanza ikiwa pamoja na kuliezeka upya paa jengine. Aidha Wizara kupitia Kamisheni ya Utamaduni na Michezo imepanga bajeti katika mwaka huu wa fedha kwa ajili ya kutengeneza matengenezo hayo.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi wizara katika Kamisheni ya Utamaduni na Michezo ina vikundi viwili vikubwa kikundi cha Sanaa cha Taarabu na kikundi cha ngoma za Sanaa za Maonesho ambayo wasanii wake ni waajiriwa wa kudumu. Vikundi vinavyotumika katika shughuli za Serikali kama vile

kupokea wageni mara nyingi ni vikundi hivyo na vikundi vilivyoajiriwa na vikosi.

Aidha kazi ya Baraza la Sanaa kimsingi si kuajiri vikundi vya sanaa bali ni kuviendeleza kuvisajili na kuvipatia mafunzo. Suala la uajiri ni la vikundi vyenyewe vya sanaa kujiajiri kama tulivyoona hivi sasa vikundi vingi vinajiajiri kama vile vikundi vya maigizo, sarakasi, sanaa za ufundi, tiba za asili na sanaa za maonesho.

Pia Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi alizungumzia suala la Eacrotanal hichi ni kituo cha utafiti wa Lugha za Kiafrika na si Chuo. Kutoendelea na shughuli hizo kumetokana na nchi wanachama kusita kutoa michango yao. Kwa upande wa matumizi ya shilingi 18 milioni, tulizopewa ni kuwa shilingi 15 milioni, ni fedha zinazotumika kwa kulipa baadhi ya mishahara ya wafanyakazi. Aidha baadhi ya wafanyakazi wengine ni fedha za uendeshaji wa kituo hicho zinazopatikana na fedha za ukodishwaji wa kumbi zilizomo kituoni hapo.

Mhe. Spika, kuhusu Baraza la Kiswahili walichangia ni pamoja na Mhe. Haji Faki Shaali nampongeza sana kwa mchango wake na ushauri wake alioutoa tutashirikiana sana mimi na yeye namna wa kuutekeleza na pia Wizara ya Elimu tutashirikiana katika suala hilo.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa tunakushukuru na kuhusu Baraza lako hili linatoa taaluma fasaha ya matumizi sahihi ya Kiswahili kupitia kwenye vipindi vya *Kiswahili lugha yetu* vinavyorushwa na *ZBC* Redio na *TV* kila wiki pamoja na machapisho yakiwemo vitabu, majarida na vipeperushi.

Mhe. Panya Ali Abdalla ushauri wake wa kuwatumia wakalimani tunapokwenda nchi za nje ni mzuri na tutakaa tutaangalia namna gani ya kuufanyia kazi. Mhe. Mohammed Haji Khalid tunamshukuru sana kwa michango yake kwa kweli michango yake mizuri na anaendelea kutuelekeza katika matumizi mazuri ya lugha ya Kiswahili tunamshukuru sana.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis kuhusu hoja ya utafiti wa viumbe baharini na madhara yake, ni programu maalum iliyopangwa na kuandaa bajeti yake ya shilingi milioni 8,415000 kwa mwaka huu wa fedha kwa hatua za awali. Programu hii inatarajiwa kuchukua miaka 3 kukamilika kuandikwa, baada ya hapo fedha maalum zitaombwa kwa ajili ya uchapishaji.

Mhe. Spika, Mhe. Makame Mshimba Mbarouk alizungumzia suala la michezo na naomba pia niwajibu Mhe. Salum Abdalla Hamad, Mhe. Hassan

Hamad Omar, Mhe. Asha Bakari Makame Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi, Mhe. Mahmmoud Muhammed, Mhe. Nassor Salim na Mhe. Salma Mohammed Ali.

Kwanza nawashukuru wote kwa michango yao na majibu yao ni kwamba Mhe. Makame Mshimba alitaka kujua fedha zinazotolewa na Mhe. Dr Aman Karume kwa chama cha Riadha ambazo hazikuwafikia walengwa. Ni kweli Dr Aman Karume alitoa fedha kuzawadiwa vyama vya Michezo vilivyofanya vizuri katika kiwango cha kimataifa ikiwemo chama cha Riadha kwa mujibu wa Uongozi wa chama cha Riadha ni kwamba fedha hizo shilingi milioni 100 walikabidhiwa chama cha Riadha, walikubaliana kutumia katika madeni yaliyokuwa yakikabili chama hicho ambayo yalitokana na ushiriki wao katika mashindano mbali mbali. Maamuzi hayo yalitokana na makubaliano ya chama hicho kwa wakati huo. Hata hivyo Baraza la Michezo linaendelea na utaratibu wa malalamiko yaliyopo yanafanyiwa kazi.

Mhe. Spika, Salim Abdalla Hamad aliuliza iwapo kuna mipango ya kuimarisha michezo kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu. Jibu ni kweli kwamba mipango hiyo ipo na tayari tumeanza vikao baina ya Wizara ya Elimu na wizara yangu na tayari tumeshaunda Kamati ya kushughulikia mambo hayo na kikao cha mwisho wanaandaa kalenda kwa ajili ya kufundisha hiyo.

Mhe. Hassan Hamad Omar alieleza juu ya maandalizi madogo ya timu zetu kutofanya vizuri katika mashindano ya kimataifa. Mhe. Spika, hili ni kweli kwamba maandalizi wakati mwengine huwa si mazuri kutokana na uhaba wa fedha. Kushindwa kwa timu zetu kufanya vizuri kutokana na maandalizi ya timu zetu hafifu yasiyokidhi haja ambayo yanasababishwa na ufinyu wa fedha kugharamia timu. Jambo ambalo linazikosesha timu zetu mechi za kirafiki za kimataifa na za kujipima nguvu na za kupata mazoezi.

Wizara yangu kulielewa suala hili tumelifanyia kazi kupitia Baraza letu la Michezo, tumeshajihisha wahisani na wadau wengine kupitia Kamati mbali mbali za kusaidia maendeleo ya michezo tunategemea kupitia Bajeti ya Serikali, na kupitia kikao hiki namuomba Mhe. Hassan Hamad Omar awe miongoni mwa wahisani hao.

Mhe. Spika, Mhe. Asha Bakari Makame alitaka ufafanuzi juu ya baadhi ya timu kukosa haki zake pamoja na kukiuka taratibu za kanuni za ndani ya mpira wa miguu wa ndani ya *ZFA.*

Mhe. Spika, Wizara ya Habari, Utamaduni,Utalii na Michezo tayari imeliagiza Baraza la Taifa la Michezo kukaa pamoja na Uongozi wa Chama cha Mpira wa Miguu *ZFA* kuhakikisha kwamba taratibu na kanuni za usimamizi wa mchezo huo zinafuatwa na hazipingwi ili kuhakikisha haki inatendeka.

Aidha Wizara imeagiza pia kuhakikisha kwamba malalamiko yote yaliyowasilishwa yanafanyiwa kazi kwa mujibu wa sheria na taratibu zinazostahiki. Na kwa heshima ya mama Asha Bakari mpenzi mkubwa wa timu ya *Mwenge Sports Club* ya Wete namuhakikishia mimi mwenyewe nitakwenda kukaa na uongozi wa mwenge kuwasikiliza kwa makini matatizo yao, na nitampa matokeo ya mkutano huo baada ya mwezi wa Ramadhani tukijaaliwa.

Mhe. Spika, Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi alitaka Wizara isaidie timu ziweze kupanda madaraja na kufanya vizuri. Ushauri huo tunauchukua na tutaufanyia kazi. Katika kipindi cha mwaka 2012/2013 yapo mafanikio mengi katika vyama na vilabu vyetu vya michezo kutokana na kufanya vizuri katika mashindano ya Kimataifa.

Hivi karibuni mwanariadha kutoka Zanzibar alishinda mashindano ya Arusha *International Marathon* yaliyoshirikisha zaidi ya nchi sita za ukanda wa Afrika Mashariki na Kati na kupata nafasi ya kwanza. Chama cha Riadha wamefanikiwa ushindi wa tatu kwa kupata medali za dhahabu katika mashindano ya mwaka huu ya vijana kwa nchi za Afrika Mashariki na Kati yaliyofanyika Uganda. Chama cha Judo kilifanikiwa kupata ushindi wa kwanza kwa wanawake na ushindi wa tatu wa jumla katika Mashindano ya Afrika Mashariki na Kati yalifanyika Zanzibar. Aidha timu yetu ya mpira wa miguu *Zanzibar Heroes* imefanikiwa kupata ushindi wa tatu katika mashindano wa *CECAFA* yaliyofanyika Uganda.

Mhe. Spika, Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa, alitaka kujua ni kwa nini idadi ya timu zetu kushiriki kimataifa zilipungua ukilinganisha na mwaka jana. Jawabu ni kweli kwamba idadi ya walioshiriki katika mashindano kwa timu zetu kwa michezo mbali mbali za kimataifa zimepungua ukilinganisha za mwaka jana. Hii inatokana na uhaba wa fedha na kukosekana kwa wahisani na wafadhili kugharamia timu zetu kushiriki katika mashindano mbali mbali. Hata juhudi zaidi zinafanywa ili kuongeza idadi ya washiriki wa timu zetu katika mashindano ya kimataifa.

Mhe. Spika, Mhe. Nassor Salim Ali aliuliza kuhusu mipango ya Serikali kujenga kiwanja kipya kwa ajili ya shughuli za Serikali. Ni kweli kwamba

viwanja vyetu vya michezo vinapata athari kubwa kwa shughuli mbali mbali hasa gwaride. Kwa hivyo, wizara yangu haikukaa kimya tayari utaratibu wa mashirikiano na wenzetu wa Jamhuri ya watu wa China umeshafanyika, na tayari tumeshatiliana mkataba baina ya Serikali na Serikali ya Jamhuri ya China ili kukijenga upya Kiwanja cha Aman.

Kuhusu mategenezo wa Uwanja wa Mnazi Mmoja tayari suala hili tayari limeshafanyiwa kazi kwa mashirikiano na Baraza la Manispaa, kwa vile eneo hilo ni miongoni mwa maeneo ya wazi yanayomilikiwa na Baraza hilo.

Mhe. Nassor Salim Ali pia aliuliza kwa nini Zanzibar imenufaika mara moja tu katika miradi ya *FIFA* ukilinganisha na wenzetu wa Tanzania Bara. Kuhusu mradi wa *FIFA* unahusisha uwekezaji wa nyasi bandia katika viwanja vya michezo. Sababu zilizopelekea kuwepo kwa kiwanja kimoja tu kinachonufaika na mradi huo hapa Zanzibar ni uamuzi wa *FIFA* wenyewe na *priority* zinazopangwa na *TFF* ambao ni wanachama wa *FIFA,* na niliwahi kumuita Mwakilishi wa *FIFA* kanda ya Afrika na Ofisi kwangu juu ya mpango wa Zanzibar. Jibu lao ni kwamba watatufikiria juu ya miaka inayokuja. Hata hivyo, wizara itabidi kushughulika nao katika suala hili.

Mhe. Spika, kuhusu uwekaji wa nyasi bandia katika uwanja ya Amani tayari wizara yangu imetenga fedha, kazi hiyo ambayo taratibu zake tayari zikiwemo za kumtafuta mjenzi wa mshauri muelekezi wa kazi hizi.
Mhe. Salma Mohammed Ali pongezi zako juu ya ujenzi wa jengo la Judo Pemba tumezipokea na tunawaalika Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi leo jioni saa kumi katika uwekaji saini wa shughuli ya ujenzi huu.

Mhe. Spika, Mhe. Makame Mshimba alipongeza kwenye ufanisi unaopatikana katika Hoteli ya Bwawani na kapendekeza kwamba wenye Ofisi wasiolipa madeni watoke. Tutaendelea kuwadai na wasiolipa tutawaondoa Mhe. Spika.

Mhe. Spika, Wajumbe wengine waliozungumzia Hoteli wa Bwawani ni Mhe. Salim Abdalla Hamad, Mhe. Asha Bakari Makame, Mhe. Mahmmoud Muhammed Mussa, Mhe. Fatma Mbarouk Said, Mhe. Saleh Nassor Juma na Mhe. Hamad Masoud Hamad.

Mhe. Spika, vyumba kumi vitafanyiwa matengenezo makubwa na vyumba arubaini matengenezo madogo madogo kama sehemu ya mifereji na maji machachu na maji safi. Baada ya kupata vyumba vya kupangisha kama 70 tutaanza kuitangaza hoteli. Kwa mwaka jana tumetengeneza vyumba 24 na sio 4, vyumba 4 matengenezo makubwa na 20 matengenezo madogo madogo.

Kuhusu ukuta wa Bwawani kuweka mawe makubwa na kupanda mikoko imepangwa kupanga katika bajeti hii na baada ya kupata ushauri.

Mhe. Asha Bakari na Mhe. Hamza Hassan Juma wafanyakazi wote wameajiriwa kihalali na wanathaminiwa na wanatambuliwa kuwa ni wafanyakazi wa Serikali. Michango ya *ZSSF* inapalekwa kama kawaida, kuhusu wafanyakazi wa Bwawani inawapatia wafanyakazi wake mikopo kwa upande wao. Lakini kuhusu mikopo ya Benki Wizara inasubiri maamuzi ya Serikali kuhusu khatma ya hoteli hiyo. Hivi sasa Serikali imo katika maandalizi ya kubinafsisha hoteli ya Bwawani. Khatma ya wafanyakazi hao haijajulikana kama watastaafishwa au watahamishwa maeneo mengine.

Sasa dhamana ya mikopo ya benki kunahitaji uendelevu wa kurudisha. Hata hivyo, suala hilo tutalishughulikia zaidi. Mazungumzo kuhusu hoteli ya Bwawani na mustakbali wake mazungumzo yanaendelea kama nilivyosema na karibuni hivi Serikali itatoa muelekeo uliokuwa sahihi.

Kuhusu Barabara ya Hoteli ya Bwawani mazungumzo yanaendelea na Wizara ya Miundombinu kupitia mfuko wa barabara juu ya matengenezo ya njia hii. Kuhusu hoteli ya Bwawani kuwa Chuo cha wanafunzi katika Chuo cha Utalii. Jibu suala hili linafanyika kwa sababu tunawapeleka wanafunzi mara kwa mara huwa wanakuja kufanya kazi zao.

Mhe. Fatma Mbarouk Said hoteli ya Bwawani ina wafanyakazi wangapi? Jibu hoteli ya Bwawani ina wafanyakazi 119 mshahara wao kwa mwezi ni shilingi 25 milioni laki mbili hamsini na tano elfu, laki tisa na sitini na nane pamoja na makato wa mishahara kwa mwaka ni milioni mia tatu na sabini na moja elfu mia sita na ishirini na tano. Mhe. Saleh Nassor Juma alishauri mapato yaingizwe kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali.

Kuhusu kuingizwa mapato katika mfuko Mkuu wa Serikali Wizara ya Fedha imekubaliana kwamba ituruhusu kukusanya mapato na kutumia kwa ajili ya kuendeleza hoteli. Mhe. Spika nimpongeze Mhe. Salma Abdalla kwa mchango wake katika Chuo cha Maendeleo ya Utalii.
Naomba pia niwajibu Waheshimiwa kama Mhe. Salmin Awadh, Mhe. Wanu Hafidh Ameir, Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa, Mhe. Husein Ibrahim Makungu na Mhe. Fatma Mbarouk waliochangia Chuo cha Maendeleo ya Utalii.

Mhe. Spika, mmong'onyoko wa Ardhi Chuo kinaendelea kushirikiana na Idara ya Mazingira katika Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kuhusu jengo hilo na kuonekana ni tatizo linalosuhu upande mkubwa kwenye eneo la

Chuo mpaka Mpigaduri. Ripoti yao ipo. Hata hivyo, Wizara mwaka katika mwaka huu utatafuta njia za kuweza kutatua tatizo hilo kitaalamu.

Kuhusu vijana kuwashajihisha kujiunga na Chuo ni moja kati ya mikakati ya kujitangaza kibiashara ukizingatia kwamba taaluma ya Utalii hivi sasa inatolewa na vyuo tafauti vya Umma na kibinafsi. Vile vile kumbukumbu zetu zinaonesha kuwa wanafunzi wenyewe sifa za juu kielimu wengi wao hawajiungi na fani ya Utalii. Inawezekana kwamba hawaelewi umuhimu wake. Kwa hivyo, Chuo kimeamua kuwashajihisha vijana wa maskuli ya Sekondari kuelewa umuhimu huo.

Kuhusu walimu kuwaongezea uwezo Chuo tayari kimeshafanya mapitio ya mpango wa maslahi ya wafanyakazi, na rasimu hiyo ya awali tayari imekwishawasilishwa katika Baraza la Chuo na Wizara ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mazingatio.

Mhe. Salmin Awadh alisema kwa nini mwaka huu jengo halikutengewa fedha. Jibu ni kwamba kwa makubaliano ya mkandarasi wa ujenzi ni kwamba jengo hilo litamalizika kwa mujibu wa bajeti iliyokwishapangiwa katika mwaka huu wa fedha. Hata hivyo, kupitia mradi unaoshughulikiwa na *ADB* Chuo cha Maendeleo ya Utalii kina mradi mkubwa wa ujenzi wa ghorofa nne wenyewe kugharamia shilingi zaidi ya dola milioni nne.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir, nimesema kwamba Chuo kinamejiwekea malengo madogo ya kufanya wakati Chuo kina uwezo mkubwa. Kutokana na mkakati wa Chuo kuongeza sifa za kujiunga na Chuo idadi ya wanafunzi itapungua. Hivyo kupeleka makusanyo kupungua. Kwani kiasi kikubwa cha makusanyo kinatokana na ada ya wanafunzi wanaojiunga na Chuo.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa, hoja ya kwamba Dr. Aman Karume ameagizwa kwamba barabara ya ndani ya Chuo ijengwe. Ni kweli Chuo kimefuatilia katika hatua mbali mbali kuanzia mwaka 2010 hadi mwaka huu katika mamlaka husika. Jibu la mwisho lililopatikana kutoka Wizara ya Mawasiliano na Miundombinu ni kwamba katika mwaka huu wa fedha mfuko wa barabara watatengeneza barabara hii. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu nakushukuru.

Na kuhusu, kuweka walimu wenye umakini na uadilifu mkubwa, suala hilo pia limechangiwa na Mhe. Fatma Mbarouk Said; jitihada za kuimarisha viwango vya taaluma kwa elimu imefanyika kupitia fedha za Serikali.

Vile vile Chuo kimo katika matayarisho kuandikiana na hati ya makubaliano baina yake na Chuo cha Utalii cha Kenya na vyuo viwili vya Utalii vya Mauritius ambavyo vimepiga hatua kubwa katika shughuli za Utalii. Makubaliano hayo yamekijengea uwezo Chuo kiweze kutambulika zaidi kitaifa na kimataifa. Pia Idara ya Utumishi Serikalini imetusaidia katika kuajiri walimu wenye sifa.

Mhe. Mwanaid Kassim usimamizi wa upatikanaji wa ajira kwa wanafunzi wanaomaliza Chuo cha Maendeleo ya Utalii. Chuo cha Utalii kinasimamia hilo kwa ukamilifu upatikanaji wa mazoezi ya vitendo katika matoli mbali mbali ya ndani na nje ya Zanzibar. Hata hivyo katika masuala ya ajira kwa wanafunzi wanaomaliza masomo yao Chuo kipo katika kuwasiliana na Idara inayohusiana na ajira kuhakikisha wanafunzi wetu wanapewa kipaumbele katika shughuli za ajira.

Mhe. Hamza Hassan Juma, alizungumzia suala la Shirika la Utalii. Naomba niseme kwamba ushauri wao tumeuchukua na tutaufanyia kazi. Lakini kabla ya kufikia hatua ile niseme kwamba tulifanya *study* kubwa kuhusiana na hali ya maendeleo ya biashara katika ushirika, na tukaona kwamba kama vile ilivyokuwa maduka ya ukoo yalivyovunjwa na bidhaa nje. Kwa hivyo na Shirika hili limevunjwa na ikaachia sekta binafsi ifanye kazi. Lakini hata hivyo ushauri ambao mara nyingi akinipa Mhe. Mwenyekiti wa Wenyeviti nitauchukua na nitaufanyia kazi.

Kuhusu mwananchi aliyetuchongea Nembo ya Serikali Baraza la Sanaa itamuweka katika kumbukumbu kwamba alifanya kazi kubwa, na kwa sababu alilipwa wakati wa kufanya kazi hiyo. Sisi kazi yetu kubwa ni kumuenzi kwamba alifanya kazi uzuri katika enzi zake.

Mhe. Spika, kwa vile jengo la Mji Mkongwe lilikuwa limekodishwa kwa mtu binafsi kwa muda wa miaka mingi nyuma, na kwa sababu muda wa kodi hiyo inamalizika kwa mwezi Agosti, tayari nimeshatoa maelekezo kwa barua kwamba kwa vile aliyekodisha ukumbi huu haonekani kuutumia vizuri kwa kuwapa wananchi utulivu, nimeelekeza mkataba wake usiongezwe na ukumbi huo urudi mikononi mwa Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale ambayo watashauriana namna bora ya kutumia vizuri.

Mhe. Spika, kuhusu wasanii wa zamani naomba nikiri kwamba hapajakuwa na mpango madhubuti wa kuwaenzi wasanii hawa ambao wako wengi sana sio tu mjini. Lakini na vijijini wako wengi kuna wapiga zumari maarufu ambao hawajulikani tena wengine wagonjwa na kuna wapiga msewe maarufu

ambao wagonjwa, kuna wachezaji maarufu sana leo wamezeeka, kuna wasanii wa msondo na ngoma ya kibati na aina mbali mbali ya wasanii.

Tunawashukuru Waheshimiwa Wajumbe hasa Mhe. Ismail Jussa na Mhe. Saleh juu ya suala hili na nakuhakishieni tutauna dawati la wasanii wa zamani ndani ya Kamisheni ya Utamaduni na Michezo ili kuwashughulikia wasanii wote akiwemo msanii wa uchoraji aliyefariki karibuni.

Mhe. Spika, Mhe. Bikame na Mhe. Hassan Hamad Omar walizungumzia kwa kupotea baadhi ya michezo maarufu kisiwani Pemba. Nashauri Mhe. Spika, Waheshimiwa hawa wakae pamoja na Mhe. Naibu Waziri washirikiane katika kufufua uazimishwaji wa mwaka kogwa wa Tumbe na Kojani ambao siku hizi hausherehekewi ni katika sherehe hizo tunaweza tukafufua michezo mingi ya asili.

Mhe. Spika, kuhusu hoja za Idara ya Habari Maelezo zimechangiwa na Mhe. Mwanaid Kassim, Mhe. Hassan Hamad Omar na Mhe. Saleh Nassor Juma napenda kuwaambia kwamba tayari kasoro zilizomo katika Wizara hiyo nambari 5 ya mwaka 1988, zimeonekana tayari hatua za kufanya marekebisho zinaendelea, ambavyo hivi sasa tuko katika hatua ya mwisho ya kuifanyia marekebisho.

Idara ya Habari Maelezo kutokuwa na ukumbi wa kuyafanyia mikutano liliulizwa na Mhe. Hassan Hamad Omar napenda kulieleza Baraza lako kwamba Wizara imeliona jambo hilo na kulipa umuhimu mkubwa wa kulipatia Idara hiyo fursa ya kutumia ukumbi wa Wizara uliopo Ukumbi wa Juu wa Baraza la Wawakilishi la zamani Mmazi Mmoja ambapo kila inapokuwa na mikutano yake hupata nafasi ya kuutumia.

Mhe. Spika, kuhusu michango ya Bodi ya Sensa ilivyoulizwa na Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi na Mhe. Mohammed Haji Khalid, Mhe. Suleiman Hemed Khamis majibu yake ni kwamba wizara yangu kupitia Bodi ya sensa ya filamu na sanaa za maonesho imejitajidi na itaendelea kuzikagua kazi zote za sanaa kabla ya kuoneshwa na kusikilizwa hadharani. Hata hivyo ushauri wao tunaupokea kwa kuzidisha juhudi.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe hivi tunamsikia Mhe. Waziri vizuri maana ndio anafanya majumuisho. Mimi nadhani tungemsikiliza ili iwe wepesi katika hatua itakayofuatia.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: (anaendelea) Mhe. Nassor Salim Ali alizungumzia kuhusu kuzingatia maadili katika

tamasha la *ZIFF* kama nilivyojibu katika suala la Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi zipitiwe sanaa zote kabla ya kuoneshwa. Hivyo kazi hiyo itatendeka kama ilivyo taratibu na kazi hiyo ilikaguliwa kwa sehemu iliyoletwa. Wizara yangu imechukua hatua za kuwataka Wahusika kuwapatia maelezo na pia tunaangalia namna gani ya kuwaadhibu.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis kuhusu kuporomoka kwa maadili hasa kwa vijana wetu kunakosababishwa na matumizi ya madawa ya kulevya ametaka kujua Bodi inaweza ikasaidia vipi. Suala hili tunalifanyia kazi kwa kutoa taarifa na maelezo mbali mbali katika vyombo vyetu vya habari na Bodi ya Sensa suala hilo linafanyiwa kazi vizuri.

Mhe. Spika, kuhusu hoja zinazohusu Idara ya Mipango Sera na Utafiti na Idara ya Uendeshaji na Utumishi. Mhe. Fatma Mbarouk Said na Mhe. Salmin Awadh na Mhe. Hija Hassan Hija majibu yake ni kwamba Bajeti iliyo sawa ni ile ya mwaka uliopita ni taasisi zinazojiendesha kwa ruzuku ambazo hizo kiutaratibu bajeti yake inatakiwa zipunguwe lakini kwa siku nyengine bajeti yake imeongezeka.

Hatma za wafanyakazi 6 wa *ZBC* ambao hawana vyeti na wako karibu kustaafu. Napenda kuliarifu Baraza lako ni kweli kwamba *ZBC* ina watumishi 6 ambao hawana vyeti na wanakaribia kustaafu kazi kwa kufikia umri wa lazima baada ya kutumikia chombo hiki cha habari kwa muda mrefu, lakini mishahara yao haiendani na muda wao wa Utumishi. Wizara kwa kutambua mchango wao na uzalendo waliouonesha tokea kuanzishwa kwa Idara ya televisheni hatimaye ZBC tumechukua hatua zifuatazo:-

Kwanza nimepeleka ombi la kuomba kubadilishiwa mishahara katika Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Katika mwezi wa Aprili tumepeleka ombi kama hilo kwenye Tume ya Utumishi Serikalini na sasa wametujibu kwamba suala hilo linashughulikiwa.

Mhe. Spika, kuhusiana na wafanyakazi wa *FTC* Mbweni, napenda kuliarifu Baraza lako kuwa tayari watumishi wenye elimu ya kiwango cha *FTC* wameanza kulipwa mishahara iliyo sawa na viwango vyenye Stashahada, baada ya serikali kuamua kuvitambua vyeti hivyo kuwa ni halali.

Mhe. Spika, kuhusu hoja zinazohusu Tume ya Utangazaji. Namshukuru sana Mhe. Naibu Waziri amezijibu vizuri.

Mhe. Rufai Said Rufai alizungumzia suala la Chuo cha Uandishi wa Habari. Majibu yake ni kwamba namuhakikishia Mhe. Rufai Said kuwa Wizara iko

makini katika kusimamia taasisi zake ikiwemo Chuo cha Uandishi wa Habari. Lakini pia nikubaliane naye kwamba; kuwepo kwa uhaba wa bajeti ni tatizo kubwa, suala hili linajitokeza takriban kwa taasisi zote zilizomo ndani ya wizara yetu. Hata hivyo, tunaahidi kuliongezea fungu la Chuo kadiri ya hali ya upatikanaji wa fedha inapopatikana.

Mhe. Spika, kuhusu hoja zinazohusu Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale. Hoja hii imechangiwa na Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, Mhe. Saleh Nassor Juma, Mhe. Ismail Jussa Ladhu, Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi, Mhe. Salma Mohamed Ali, Mhe. Suleiman Hemed Khamis, Mhe. Bikame Yussuf Hamad, Mhe. Fatma Mbarouk Said na Mhe. Rufai Said Rufai.

Mhe. Spika, nawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe kwa michango yao, ila nakubaliana na wazo lake Mhe. Makame Mshimba Mbarouk kwamba fedha tunazozipanga kwa makumbusho ni kidogo. Serikali imekuwa ikiongeza kima cha bajeti yake kila mwaka, hata mwaka huu wa fedha imeongezwa kutoka shilingi milioni 475 hadi shilingi milioni 679. Mhe. Spika, ushauri wake tunaupokea kwa mikono miwili, tunakubaliana na wazo lake alilotoa juu ya uwekaji wa sanaa za mikono na tumbuizo asilia katika uimarishaji wa shughuli za makumbusho.

Mhe. Spika, Mhe. Saleh Nassor Juma Mwakilishi wa Jimbo la Wawi yeye alieleza kwamba wizara haiko makini katika kuendeleza maeneo ya kihistoria katika maeneo ya Vitongoji. Mhe. Spika, napenda kumuhakikishia Mhe. Saleh kwamba wizara iko makini katika hilo; kwani eneo alilotolea mfano ni miongoni mwa maeneo ambayo yamepewa kipaumbele katika bajeti ya mwaka huu wa 2013/2014, tayari kuna kituo cha kutoa habari ambacho kitafanywa kwa *site museum.* Kwa kuanzia utafiti unafanywa kwa ajili ya kuiendeleza *site museum.*

Mhe. Spika, Mhe. Ismail Jussa aligusia juu ya kuenzi na kuendeleza maeneo ya kihistoria hasa kwa maeneo ya Beit Al Ajaib na Kasri ya Mfalme. Mhe. Spika, wizara inakubaliana na mawazo yake ya kuchukua hatua za kuyaenzi na kuyaendeleza maeneo yote ya kihistoria. Napenda kumuhakikishia Mhe. Mwakilishi kwamba natengenezo ya Beit Al Ajaib na yale ya *Palace Museum* yamekuwa yakiendelea kila tunapoingiziwa fedha na wizara ya fedha.

Mhe. Spika, naomba nimkumbushe Mhe. Mwakilishi kwamba wizara imekabidhiwa majengo mawili yaliyokuwa taabani. Moja ni Kumbusho Kuu na jengine ni Beit Al Ajaib, hali ya majengo haya yalikuwa taabani. Leo ukipita katika maeneo ya makumbusho ya Mnazi Mmoja kila mmoja anafurahi. Nilidhani Mwakilishi wa Mji Mkongwe angetupongeza kwa hilo.

Kuhusu Beit Al Ajaaib jengo linahitaji matengenezo makubwa bado, na wizara yangu inalifanyia kazi.

Mhe. Spika, tumezungumza na Serikali ya Oman na tayari wamewaleta wahandisi wao waje washirikiane na wahandisi wa Mji Mkongwe kuhusiana na mradi mkubwa wa matengenezo ya majengo haya mawili, jengo la Beit Al Ajaaib na Kasri, na tumekubaliana kwamba paandaliwe mradi maalum ambao kwanza utafanya *study* kubwa wa hali ya majengo yale na athari ya mazingira ya bahari. Pili paandaliwe michoro na *design* ya matengenezo. Tatu pawekwe mfuko maalum utakaoingiza fedha baina ya Serikali ya Zanzibar na Serikali ya Oman na washirika wengine; na nne pafanywe kazi ya matengenezo. Timu ya Oman imeondoka mwezi uliopita na kila sehemu ina kazi ambayo tumekubaliana kuifanya. Wakati hayo yakiendelea tutaendelea kutumia fedha zetu kufanya matengenezo mbali mbali. Mhe. Spika, hatukukaa, tunahangaika na tutahakikisha kwamba matengenezo hayo yamekuwa vizuri.

Mhe. Spika, Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi alizungumzia suala la kuyapima na kuyapatia hati miliki maeneo ya kihistoria. Mhe. Spika, jitihada ya Wizara ya kuyapima maeneo yale na kuyapatia hati miliki ni jambo la lazima, lakini pia ni la kupongezwa kwani majengo mengi ya serikali hayana hati miliki. Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale ina maeneo zaidi ya 80 yanayohitaji hati miliki na taratibu hizi zimeanza miaka 10 nyuma na zinaendelea kushughulikiwa. Tayari kuna maeneo saba ambayo yameshapatiwa hati miliki.

Mhe. Spika, kuhusu Uanzishwaji wa makumbusho mapya. Ni kwamba makumbusho matano yaliopo bado hayatoshi na kuna maeneo mbali mbali ambayo yanastahiki kuwa makumbusho na yanashughulikiwa.

Mhe. Salma Mohamed wa viti maalum alitaka kujua kwa nini maeneo mengi ya kihistoria yako mwituni? Ni kweli maeneo mengi ya kihistoria yako mwituni sio kwa upande wa Pemba tu, jambo linalochangiwa na ufinyu wa bajeti, lakini kwa msaada wa mfuko wa *MACEMP* na *TASAF* tumeweza kujenga *information centre* kwa maeneo ya Pujini, Chambani, Vitongoji, Mkumbuu na Chwaka Tumbe. Pia Ubalozi wa Marekani umesaidia makumbusho ya Chake Chake Pemba, Msikiti wa Micheweni na Shumba Mjini.

Vile vile Mhe. Spika, napenda kumpatia ufafanuzi Mhe. Salma Mohamed kwamba kuhusiana na usahihi wa bajeti ya Pemba kwamba ni asilimia 24. Usahihi ni kwamba Idara ya Makumbusho Pemba ilitengewa shilingi 33 milioni, lakini baada ya mkato wa meli zikapungua hadi shilingi milioni 18 na

zilizopatikana ni shilingi milioni 7.8 ambazo ni sawa na asilimia 42. Hata hivyo, kima hicho ni kidogo ndio maana mara hii hali hiyo imerekebishwa.

Mhe. Spika, Mhe. Suleiman Hemed Khamis aliuliza kwamba fedha zinazopatikana zinaweza kutosheleza kuimarisha maeneo ya kihistoria ambayo bado hayajaimarishwa? Jibu lake ni kuwa fedha hazitoshi na ndio maana tunatafuta fedha zaidi kwa kupitia mfuko wa serikali na pia kwa kupitia kwa wahisani wengine.

Mhe. Bikame Yussuf Hamad, alisifu jitihada za Idara katika kuyaimarisha maeneo ya kihistoria. Nikushukuru kwa hilo. Idara iko tayari kuwapokea Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa ajili ya kuwatembeza katika maeneo mbali mbali ya kihistoria ili kujifunza historia na utamaduni wa Zanzibar.

Mhe. Fatma Mbarouk Said, tunakushukuru kwa mchango wako kuhusiana na suala hili na tunakuahidi kwamba tutaendelea kuyaenzi na kuyahifadhi maeneo ya kihistoria.

Mhe. Rufai Said Rufai Mwakilishi wa Jimbo la Tumbe, aliomba kujua makumbusho ya Chwaka na Tumbe kama ilivyowahi kufanyiwa utafiti na mtaalamu kutoka Marekani bwana Geofrey. Ni kweli makumbusho ya Chwaka na Tumbe kwa vipindi mbali mbali yalifanyiwa utafiti na jopo la watafiti kutoka Marekani kwenye Chuo Kikuu cha Virginia akiwemo mtaalamu aliyeitwa bwana Geofrey kama alivyomtaja, utafiti huu ulianza mwaka 1997, 2000, 2004, 2006 na bado unaendelea.

Mhe. Spika, kwa kupitia utafiti huu serikali imefaidika kwani wananchi wa eneo la Chwaka na Tumbe walishirikishwa kikamilifu katika utafiti huu na kujipatia ajira ya muda na mambo mbali mbali yanayotokana na taaluma ya utafiti huo.

Mhe. Spika, kuna hoja mbili ambazo nazimalizia. Kwanza ni hoja inayohusu Zanzibar ama *Multiplex Company*. Imeulizwa na Mhe. Ismail Jussa Ladhu, Mhe. Viwe Khamis Abdalla, Mhe. Hija Hassan Hija, Mhe. Salma Mohamed Ali na Mhe. Suleiman Hemed Khamis.

Mhe. Spika, katika Uanzishwaji wa shughuli za *digital* kumekuwa na washirika watatu. Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, iliyochangia fedha nyingi za ununuzi wa mitambo, Shirika la *ZBC* lililochangia baadhi ya maeneo yake na kutumia baadhi ya miundombinu yake na hata wafanyakazi wake wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo waliochangia baadhi ya gharama za ndani na usimamizi wa sera.

Mhe. Spika, kwa kuzingatia hilo na baada ya mashauriano na Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, tumekubaliana kwamba *share* za kampuni zigaiwe katika utaratibu ambao umeingizwa kwenye kitabu, na mpaka kile kima ambacho kitakuwa kimerudishwa kugharamia fedha hizo kwa wizara ya fedha. *ZMUX* na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu na Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo itakaa tena kuangalia mgao wa fedha hizo ambapo *ZBC* watategemea kupata mgao mkubwa kidogo, kilichobaki kitawekwa katika mfuko wa *Zanzibar MUX* ili kuwa na akiba ya kuendeleza *digital* hapo baadae na fungu dogo la wizara ambalo litakwenda Hazina.

Mhe. Spika, kuhusu mkataba wa Agape kujenga minara na kuweka majenereta. Ushauri tuliopewa na kitengo kinachohusiana na mradi wa e-*government*, ni kwamba kwa vile kuna minara ambayo haina matumizi makubwa katika maeneo ambayo Agape walitakiwa wajenge minara, pia kulionekana kutakuwa na kupoteza fedha bure wakati minara ya serikali ipo tayari. Kwa hivyo, tukakubaliana tutumie minara ya e-*government* na ile ya Zantel badala ya kujenga minara mingine. Fedha zilizotengwa kwa ujenzi wa minara zikapangiwa matumizi mengine katika *addendum* ya mradi iliyotayarishwa. Kuhusu majenereta, vituo vyote vimepangiwa kuwa na majenereta ya akiba.

Mhe. Spika, kuhusu *quality* ya matangazo. Hivi sasa kwa kiasi kikubwa *quality* ya matangazo imeimarika kwa kutumia *microwave* na ambazo tokea mwanzo zilipangwa kuwa ni akiba. Mkonga utakapokuwa tayari hali ya matangazo itaimarika zaidi.

Mhe. Viwe Khamis Abdalla, kuhusu *channel* za *Z-MUX* kupotosha mila na maadili yetu. Ile sio sahihi tujitahidini kuingiza *channel* ambazo haziendi kinyume na maadili yetu. Hata hivyo, kama kuna *channel* unahisi huipendi, basi katika king'amuzi chetu kuna huduma ya kufunga *channel* kwa watoto, nakuomba uwasiliane na watoa huduma wa *Z-MUX* ili wakupatie huduma hiyo.

Mhe. Spika, Mhe. Hija Hassan Hija alizungumzia suala la matangazo ya *digital* kutoonekana Pemba, na pia suala hili lilizungumzwa na Mhe. Salma Mohamed Ali na Mhe. Farida Amour Mohammed. Mhe. Spika, niliwahi kusema hapa Barazani kwamba aina ya *digital* ilifanywa ili mawimbi yake yasafirishwe na mkonga, yaani *optic fiber*, hizi *microwave* ni za wakati wa dharura. Sasa kwa hali ya kutumia vifaa hivi vya dharura, mawimbi ya *digital* yanafika hadi Nungwi, ili yafike mpaka Pemba ni lazima yasafirishwe tena kwa kifaa cha dharura hadi Mkoani. Hali ya upepo mkali kwenye mnara wa

Nungwi unakifanya kifaa kigeuke juu kuyumba na kupoteza mawasiliano baina ya Mkoani na Nungwi na hivyo kutokea *no signal* mara kwa mara katika televisheni za Pemba. Kwa hivyo, Pemba sio kuwa matangazo ya *digital* hayafiki ila yanafika wakati mwengine katika televisheni inaonekana *no signal*.

Mhe. Spika, ili kuondokana na tatizo tumekubaliana na Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo na Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora, tuanze matumizi ya mkonga ili kuweza kusafirisha mawimbi ya *digital* Pemba kwa ufanisi zaidi. Kwa hivyo, Mkoani, Chake Chake na Wete wataendelea kupata matangazo ya kukatikakatika hadi mkonga utakapowashwa.

Hata hivyo, tokea juzi wahandisi wa Kampuni ya *Electronikka* ya Afrika ya Kusini, washirika wakubwa wa Agape wapo katika maeneo ya Nungwi na Mkoani, ili kuangalia ni vipi wanaweza kupunguza athari ya kuyumba kwa mnara wa Nungwi kwenye *microwave* iliopo Kichunjuu Pemba.

Mhe. Spika, Mhe. Suleiman Hemed Khamis aliuliza ni lini Kampuni ya Agape itamaliza kazi yake? Jibu lake ni kwamba inategemea uwashwaji wa mkonga ili wapate nafasi ya kuunganisha mkonga na *transmission* za *digital* ziliopo vituoni kote mpaka Jimboni kwake Konde.

Mhe. Spika, Mhe. Salma Mohamed Ali, alinishauri kwamba nifanye mambo matatu. Moja nipunguze bei ya king'amuzi kutoka shilingi 70,000 hadi shilingi 30,000. Mhe. Spika, king'amuzi hiki ni cha teknolojia ya juu kuliko vyote viliopo hapa Zanzibar na kwa bei ya soko havipungui shilingi 120,000. Kwa hivyo, sisi kuuza kwa shilingi 73,000 pamoja na bei ya muda ya mwezi mmoja tumefidia sana.

Jambo la pili ameniomba niwakopeshe wananchi na wafanyakazi. Mhe. Spika, king'amuzi chetu ndio pekee ambacho kinahudumia bure *channel* tatu, *ZBC*, *TBC* na *ITV* hata kama mteja hajalipia mwisho wa mwezi. Kupatikana kwa huduma hizo bure kutawafanya wananchi waliokopeshwa wasione umuhimu wa kulipia deni lao.

Jambo la tatu alilonishauri Mhe. Salma Mohammed Ali ni kuweka wiki ya *sale* au *promotion* ya ving'amuzi. Mhe. Spika, kwa niaba ya Uongozi wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo na kwa niaba ya Kampuni ya Agape naomba nikubaliane na ushauri wa Mhe. Salma Mohamed Ali kwamba kuanzia tarehe 28/07/2013 hadi tarehe 06/08/2013 mwaka huu kutakuwa na wiki ya *sale* ya *promotion* ya ving'amuzi vya *ZMUX* na bei ya

king'amuzi itashuka kutoka shilingi 73,000 hadi shilingi 48,000, ninawaagiza wanaohusika watoe matangazo juu ya wiki hiyo ya *promotion*.

Mhe. Spika, mchango wa mwisho ni kuhusu Shirika la *ZBC*. Shirika la *ZBC* limechangiwa karibu na Wajumbe wote. Naomba niseme kwamba kwanza nawashukuru sana kwa michango yao, naamini wameitoa kwa nia ya kujenga na bila shaka wana hamu ya kuona kwamba *ZBC* nayo inabadilika na kuwa na ufanisi. Nawapongeza sana kwa hamu yao hiyo, kwani inanipa moyo kwamba tuna wenzetu katika jukumu zito tulilopewa.

Mhe. Spika, nawaomba Waheshimiwa Wajumbe warudi kwenye *paragraph* ya 42, katika ukurasa wa 18 na 19 ya kitabu changu cha bajeti, juu ya maelezo ya muelekeo wa mageuzi makubwa ya *ZBC*. Uamuzi wetu wa kufanya mageuzi hayo ya Shirika sio utashi, lakini ni kwa sababu pana matatizo yaliyotusukuma kuelekea kwenye mageuzi hayo, na kwamba bado mageuzi hayajakamilika na hivyo matatizo bado yapo, na ndio maana tunaomba kushirikiana na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako katika kukamilisha mageuzi haya.

Kwa hapa naomba kumshukuru sana Mhe. Asha Bakari Makame mama yetu katika kuniombea muda wa kumaliza kazi niliyoianza, na kwa hivyo naomba sana kuidhinishiwa matumizi ninayoomba.

Mhe. Spika, moja ya mageuzi makubwa na muhimu tuliyofanya pamoja humu ndani ya Baraza, na niwashukuru sana wajumbe kwa hilo ni kupitisha sheria ya *ZBC* mwanzo wa mwaka huu, ambayo ndio kwanza sasa inaanza kutumika.

Mhe. Spika, alisema Mhe. Hamza Hassan kwamba Shirika lilikuwa linaendeshwa kwa amri ya sheria tu, kwa kweli lilikuwa na mapungufu mengi. Mhe. Spika, udhaifu uliopo katika uendeshaji wa Shirika tunauelewa vizuri, mapungufu ya vifaa uliopo shirikani tunaufahamu sana, na upungufu wa kibajeti na wataalamu tunauelewa. Mambo haya yanahitaji ushirikiano wetu pamoja, na tunaahidi mbele ya Baraza lako tukufu Mhe. Spika, Shirika la *ZBC* litajirekebisha.

Nataka niwaambie Waheshimiwa Wajumbe kwamba mmeona dalili kwamba viongozi wa Shirika wameanza kubadilika. Kwa hivyo, naomba tuendelee kwa pamoja tushirikiane ili Shirika tulibadilishe.

Mhe. Spika, katika hili tuna tatizo kwamba hivi sasa Shirika halina Bodi. Iliyokuwepo imemaliza, baada ya kumalizika *legal notice*. Tunashirikiana na

wenzangu serikalini kuunda Bodi mpya, nitahakikisha kwamba tunashirikiana na Bodi inayokuja ili kuona kwamba katika kipindi kifupi kinachokuja, kama alivyosema Mhe. Rais *ZBC* haiwi tiro. Hilo naahidi kulisimamia na kwa hilo tunahitaji sana kuidhinishiwa fedha tulizoomba.

Mhe. Spika, ni kweli hivi karibuni kulikuwa na jambo la kumdhalilisha Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais ndani ya *ZBC;* redio na televisheni yaliyokuwa yakifanywa na watangazaji mbali mbali wa Shirika hilo. Najua jambo lile liliwaudhi Wazanzibari na Watanzania wengi, nilikuwa napata simu nyingi kwenye simu yangu na kwenye *e-mail* yangu. Sasa Mhe. Spika, mtoto wako wa mtaani akimtovukia heshima Sheikh wa mtaa, basi lawama ni ya baba wa mtoto ndiye anayeonekana ana malezi mabovu na hulazimika kuomba radhi kwa wazee wenziwe.

Mhe. Spika, naomba kutumia fursa hii kumuomba radhi Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais na Wazanzibari wote walioudhika na hali hiyo, naomba niseme kwamba Katibu Mkuu wa Wizara alilikemea sana suala hili, Naibu Waziri Mhe. Bihindi Hamad na yeye alilikemea sana, na mimi mwenyewe nililikemea kwa maandishi na ninashukuru sasa hivi hali imerekebishwa.

Mhe. Spika, suala la mfanyakazi Juma Mmanga wa kituo cha *ZBC* Dar es Salaam. Ni kweli hasikiki siku hizi. Nakubaliana na Waheshimiwa Wajumbe kwamba ni mmoja wa watangazaji wazuri na ni mfanyakazi anayejituma na ana bidii sana. Kwa bidii aliyokuwa nayo Wizara imefikiria kufungua kitengo cha wizara Dar es Salaam ambapo angekuwa Mkuu wa kitengo cha wizara na pia mratibu wa kituo cha *ZBC* Dar es Salaam.

Kwa bahati mbaya kulitokea kutofautiana kwa tafsiri ya maana ya kumuweka mkuu wa kituo cha wizara Dar es Salaam ambacho bado hakijaanzishwa, uongozi wa *ZBC* ukadhani labda nafasi yake ya *ZBC* iko wazi, wakaamua kumuweka mtu mwengine. Hata hivyo, baada ya kuarifiwa hilo na mwenyewe akaja wizarani kuulizia ilikuaje, baada ya mashauriano na uongozi wa wizara nimeelekeza arejeshwe kwenye nafasi yake. Hivi sasa yuko likizo ya kawaida, na atakaporudi nawahakikishia kwamba ataendelea na kazi yake ya kwamba atakuwa Mkuu wa Kituo cha *ZBC* Dar es Salaam na wizara itakapoanzishwa tutampa.

Kuhusu mfanyakazi aliyehamishiwa eneo jengine bi Maryam kutoka sehemu yake ya kabla. Taarifa niliyonayo ni kwamba alikopelekwa ni eneo ambalo linahitaji utaalamu wake na kwamba yeye ndiye miongoni mwa wafanyakazi ambao pekee pale Shirikani mwenye utaalamu huo. Hata hivyo, kwa sababu sijawahi kuonana naye uso kwa uso, ningemuomba Mhe. Ismail Jussa

amuelekeze aje wizarani kesho asubuhi tutazungumza naye, na kama haridhiki na sehemu aliyonayo basi tutashauriana na Shirika arudi katika sehemu ambayo alikuwa akifanya kazi.

Mhe. Spika, kituo cha Bungi kimekamilika kwa takriban kazi zote, isipokuwa umeme haujaingizwa ndani ya nyumba tu za wafanyakazi, jambo ambalo linashughulikiwa na Idara ya Majenzi waliopewa *tender* ya kujenga nyumba hiyo, tutalisimamia ili limalizike.

Mhe. Spika, nakubaliana na Waheshimiwa Wajumbe kwamba posho wanalolipwa wafanyakazi wanaokuja hapa Barazani kutoka *ZBC* ni ndogo, lakini angalau sasa inapatikana, mwaka jana ilikuwa haipatikani. Kwa hivyo, angalau imepatikana nilidhania labda Mhe. Bi Hindi nilimpa kazi hii angepongezwa, lakini hamkumpongeza hata kwa jitihada aliyofanya kwamba sasa wameshapata. Kwa taarifa niliyonayo wananidai, zamani walikuwa wananidai mimi vikao viwili au vitatu, lakini kwa kikao hiki wananidai. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Waziri amefanya kazi kubwa katika hili, nampongeza nilimpa yeye alisimamie.

Kuhusu maoni ya Waheshimiwa Wajumbe, kwamba fedha wanazolipwa ni ndogo. Tunakubaliana nalo tutalisimamia na kwa vile shirika limeshakuwa ni la kujitegemea, linapewa uwezo wa kukusanya na kutumia nitaiagiza Bodi itakayoundwa suala hili walisimamie.

Mhe. Spika, kuhusu deni la hati miliki, ni deni ambalo tumepanga kulilipa katika robo ya pili ya mwaka huu wa fedha, baada ya kuanza kukusanya kile tunachotoa huduma kwa wateja wetu.

Mhe. Spika, kuhusu mnara uliojengwa wa Tigo. Mnara huu ni mali ya Tigo na umewekwa pale katika jitihada za kuongeza mapato ya Shirika. Malipo yanayopatikana ni dola 1,000 kwa mwezi na tayari dola 12,000 zimepatikana zimeshalipwa na zimeshaingia katika mfuko mkuu wa Hazina, tayari Waziri wa Fedha, Mhe. Omar Yussuf sasa hivi keshazikabidhi.

Mhe. Spika, kuhusu kipindi cha fakhari ya Zanzibar, kilichosifiwa na Mhe. Rais wa Zanzibar, nimeambiwa kwamba hakikupigwa marufuku, isipokuwa kinaangaliwa uwezekano wa kukiimarisha zaidi kwa kushirikiana na kipindi cha Mwanakwetu. Kuhusu suala la kutakiwa wanawake kutovaa hijabu. Haa! Mhe. Spika, suala hili sio sahihi, maana yake wanawake wenyewe ndio wale na hijabu zao wanazo.

Mhe. Spika, nawashukuru wote walioipongeza *ZBC* kwa kufanya kazi kwa bidii katika mazingira magumu. Naomba niseme kwamba ZBC ina ukata mkubwa wa fedha, kama walivyosema wenzangu ukilinganisha na Shirika la *TBC;* Serikali ya Jamhuri ya Muungano inaliwezesha sana Shirika. Sisi kwa kweli bajeti tunayoitenga kwa ajili ya shirika haiwezi kumudu na zaidi kwa shughuli nyingi tulizonazo. Kwa hivyo, vijana na viongozi wa Shirika wanafanya kazi kubwa katika mazingira magumu na bado tuendelee kushirikiana ili kuhakikisha kwamba Shirika hili tumeliendeleza.

Mhe. Spika, vile vile tunamshukuru sana Mhe. Haji Faki Shaali; Mjumbe wa Baraza la Mapinduzi kwa kuliomba Baraza la Wawakilishi kufikiria kutenga bajeti mwaka ujao. Mimi Mhe. Haji Faki naona mwaka ujao ni mbali. Mimi nadhani baada ya kikao hiki iko haja na Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, kukaa na kuangalia ni vipi kuanzia kikao kijacho cha Baraza, Baraza liwajibike kulilipa Shirika la *ZBC.*

Mhe. Spika, nawashukuru wote kwa michango waliyonipa. Nimejitahidi na ninakushukuru sana kwa kunipa muda wa kujibu hoja za Waheshimiwa Wajumbe mbali mbali, nimejitahidi sana kujibu. Naamini kwamba kwa nyuso nilivyoziona basi Wajumbe wameridhika na hoja nilizozitoa.

Wizara hii ni wizara ya wananchi wetu wote, wadau wa utalii wanaitegemea wizara hii. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk na watu wake. Wadau wa michezo, Mhe. Mshimba ni mwanariadha mzuri sana, kwa hivyo naamini kwamba atatuunga mkono. Mhe. Ismail Jussa Ladhu watu wako wa Mji Mkongwe watalala usiwe na wasi wasi, na Waheshimiwa Wajumbe wote waliochangia kwa njia moja au nyengine tunawashukuru kwa michango yao.

Baada ya hayo Mhe. Spika, nakushukuru na kwa heshima kubwa naomba kutoa hoja. *(Makofi).*

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, nichukue nafasi kumshukuru Mhe. Waziri na Naibu wake kwa jitihada ya kufanya majumuisho na kujaribu kujibu hoja. Niwahoji basi Waheshimiwa Wajumbe wale wanaokubaliana na hoja hii ya hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo wanyanyue mikono.Wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, kwa kuwa Baraza limejadili na kuikubali hotuba ya bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo. Sasa naomba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Matumizi ili kuvipitisha vifungu vya matumizi vya Wizara yangu.

KAMATI YA MATUMIZI

FUNGU 31 - KAMISHENI YA UTALII

Kifungu 0201	Utawala Unguja	1,202,000,000
	Jumla ya Fungu	**1,202,000,000**

FUNGU 42 - WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, UTALII NA MICHEZO

Kifungu 0701	Idara ya Habari Maelezo	18,000,000
Kifungu 0702	Tume ya Utangazaji	44,000,000/=
Kifungu 1101	Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale	210,000,000/=
Kifungu 1208	Kamisheni ya Utamaduni na Michezo	48,580,000/=
Jumla ya Fungu		**320,580,000/=**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, kama nimesikiliza vyema kifungu 0704 Shirika la Utangazaji Zanzibar halikutajwa. Kwa hivyo, naomba maelezo.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, maelezo.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, kasma 0704 Shirika la Utangazaji Zanzibar na Katibu Mezani ametoka Tume ya Utangazaji, ambayo ni milioni 44,000,000/=, lakini akaruka akaenda Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale na akaacha kifungu 0704 Shirika la Utangazaji Zanzibar na hiyo hakuisema ambayo milioni 280,000,000/=

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, hapa inaonekana kuna fedha zilizotengwa na kuna zero zero, labda Mhe. Waziri atuambie tu kwenye Shirika la Utangazaji hatukuisoma kwa sababu hakuna fedha zilizotengwa kwa ajili hiyo, isipokuwa huku kuna Sauti ya Tanzania Zanzibar.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba katika kifungu hicho 0704 hakuna kitu, kwa sababu hivi sasa limekuwa Shirika na hivyo kinachokusanywa kinaingia kwenye mfuko wake na wala hakiingii kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali. *(Makofi)*

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, lakini Mhe. Waziri ametuomba shilingi milioni 280,000,000/= kwenye kitabu chake. Sasa tupitishe wapi au atuambie tuende wapi tukazione hizi milioni 280,000,000/= ambazo ametuomba. Mhe. Mwenyekiti, hizi ina maana yeye.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, bado sijakufahamu vizuri.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, ametuomba tumuidhinishie kukusanya shilingi milioni 280,000,000/= Shirika la Utangazaji Zanzibar. Sasa anasema zimewekwa kwenye mfuko wake, basi atuambie tukazione wapi kwenye matumizi, na wakati hapa ndipo kwenye kifungu cha kukusanya na yeye ametuomba tuidhinishe Mhe. Mwenyekiti, naomba ninukuu hotuba ya Mhe. Waziri.

Hotuba ya Mhe. Waziri ukurasa wa 21 unaeleza hivi:-

> “Ili Shirika la Utangazaji Zanzibar liweze kutekeleza malengo yake yaliyojipangia katika mwaka wa fedha 2013/2014 naomba liidhinishiwe jumla ya shilingi bilioni 2.1 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na kukusanya shilingi milioni 280,000,000/=”.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, kwa kawaida ni kwamba hizi fedha zinazoingia hapa ni fedha ambazo zinaingia kwenye Mfuko wa Hazina ndizo fedha ambazo zime-*appear* hapa kama ni *revenue* ya serikali.

Kwa mfano, Hoteli ya Bwawani inakusanya na inatumia na wala huwezi kuidhinisha.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri, kwanza fedha hizi zilizoombwa zinatoka moja kwa moja kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali ndivyo unavyokusudia kusema.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, vipi?

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri, fedha hizi zilizoombwa hapa bilioni 2,100,000,000/=, kwamba hizi unatueleza kuwa zinatoka moja kwa moja kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali na wala haziingii kwenye kasma za hapa.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, ukurasa gani?

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri, ukurasa wa 21 *paragraph* ya 46. Maana hoja ya Mhe. Mjumbe ni kwamba huku hakuna fedha ambazo zimetiwa kwenye *vote book*, lakini hapa umeomba fedha ziidhinishwe.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, shilingi bilioni 2.1.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri, ndio shilingi bilioni 2.1.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, bilioni 2.1 zinatoka kwenye ruzuku na tunaziona mbele huko.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, nataka nimshukuru Mhe. Hija Hassan Hija ambaye anayo hoja tena ya msingi, ambapo inatokana na maombi ambayo ameliomba Baraza Mhe. Waziri.

Lakini nataka niseme kwamba hili fungu la matumizi kwa sababu shirika halijaweza kujishika sawa sawa ni kwamba serikali bado inaendelea kulilea hili shirika na ndio maana limeombewa matumizi ya shilingi bilioni 2,100,000,000/=. Hata hivyo, hizi milioni 280,000,000/= ambazo Shirika watazikusanya, na kwa kawaida fedha za Shirika huwa haziingii kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali.

Kwa hivyo, nafikiri Mhe. Waziri aliziombea hizi kwamba ziidhinishwe, lakini hazikupaswa kuwepo hapa kwenye kitabu, kwa maana hiyo Mhe. Mjumbe anayo hoja ya msingi. Kwa kweli hizi hazikupaswa kuwepo kwenye kitabu hichi kuidhinishwa kwamba tuzikusanye, isipokuwa yeye alikuwa aombe matumizi tu. Mhe. Mwenyekiti, nadhani ni kama *typing error* kwa mujibu wa uandishi na utaratibu wa kibajeti. Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana na maelezo ya Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwamba ni hoja yangu ya msingi hasa nilikuwa natafuta makusanyo ya Mnara wa *TIGO* dola 1,000 ambayo kwa *rate* ya leo ni milioni 19 na zaidi sasa tuzione wapi? Kwa

hivyo, hiyo ndio hoja yangu ya msingi na ningetegemea nizione hapa zimekusanywa kwa ajili ya *ZBC*, na Mhe. Waziri amekiri kwamba fedha zimeingia kwenye *ZBC*, basi anioneshe dola 1,000 kwa mwaka na sijui zimeanza lini, lakini zinaingia kwenye fungu gani? *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, fedha hizo dola 1,000 nilivyosema mimi ni kwamba tayari zimeshalipwa na zimeingia kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali na huo ndio uhakika ambao ninao na risiti ninayo na kila kitu ambacho kinaonesha hivyo kwamba zimekusanywa.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora, labda tupate maelezo zaidi.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. mwenyekiti, anachosema Mhe. Waziri ni sahihi anaposema kwamba fedha zimelipwa, lakini fedha hizo zitaingia kwenye ule mfuko wao kama wanaokusanya ni Shirika basi zitaingia kwenye Mfuko wa Shirika.

Sasa mimi nadhani fedha hizi madhali wameonesha hapa watakusanya milioni 280,000,000/= inawezekana fedha za makusanyo ya mwaka huu unaomalizika za hizo kodi ya Mnara wa *TIGO* zimeingia kwenye fungu kama hili. Sasa kama zilikuwa zinakwenda kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina maana yake zitakuwa zimekwenda kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina, kama zilikuwa zimebakia kwenye Shirika kwa ajili ya matumizi yao, maana yake zitakuwa zinafanana na hizi milioni 280,000,000/=.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli Mhe. Waziri amesema pale kwamba risiti zipo na mimi nafikiri hilo ni suala la baadaye. Lakini hivi milioni 280,000,000/= hapa kama ni fedha za Shirika ambalo linajiendesha au limeruhusiwa rasmi, basi hazikupaswa kuwekwa hapa kuombewa ruhusa ya makusanyo ndani ya Baraza hili.

Hata hivyo, ile hoja yake bado naikubali kwamba ni ya msingi kama alivyosema Mhe. Waziri, lakini zitakuwa zimeingia kama wakati ule mwaka uliopita fedha za makusanyo zilikuwa zinakwenda Hazina na ninakubaliana na Mhe. Waziri kwamba ziko Hazina, lakini kama zilikuwa zinatumika kwenye Shirika, maana yake zitakuwa ziko kwenye fungu kama hili ambalo limeainishwa hapa na wala halikupaswa kuwepo hapa. Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Hija Hassan Hija, sijui kama umefahamu.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, tusicheleweshe muda ni vyema Mawaziri wanapozungumza wajue kwamba wanazungumza na Wawakilishi, kwa sababu ili uwe Mwakilishi basi afanye utafiti ndio awe Mwakilishi. Kwa hivyo, wasijaribu kupanga maneno, ili hatimaye ikaja ikaonekana kwamba tunavutana, Mhe. Waziri wa Fedha yupo na mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Fedha na vyanzo vya fedha vya Wizara ya Fedha vinajulikana kwamba viko katika sehemu mbali mbali angetusaidia. Hilo ni (a)

(b) Mhe. Mwenyekiti, labda Mhe. Waziri angenipatia mkataba baina ya *TIGO* na *ZBC* na risiti ambayo nitaridhika kwa sababu mimi nafanya utafiti sana Mhe. mwenyekiti na wala asijaribu kujibu kwa ajili ya kuficha wingu la nyevule kumbe kuna mvua. Sasa labda anipatie mkataba wa *TIGO* na *ZBC* ambao umeidhinisha makusanyo hayo na hiyo risiti ambayo anayosema ipo.

Vile vile Mhe. Waziri wa Fedha atusaidie matatu haya mapato haya ambayo ni dola 1,000 kwa mwezi na umeanza lini maana mwaka mmoja, na milioni 19 na zaidi na hapa hatuyaoni na ukiniambia labda Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Waziri mwenyewe hajui. Maana yake yeye anamsaidia tu na yeye ndiye mwenye hili fungu, sasa Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora anasema labda pengine maana yeye mwenyewe hajui na pale anayo timu nzima, basi atusaidie na timu ile pale iandike na ilete hapa.

Mhe. Mwenyekiti, tunafanya utafiti wa kina kwamba hapa kuna mazonge.

Mhe. Mwenyekiti: Mimi kama nimemfahamu sawa sawa Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora anachosema ni kwamba makusanyo haya kwa kuwa hili ni Shirika hayakupaswa kuwemo humu na kuyataja sio ile au tatizo, lakini ile kuonesha kwamba ni sehemu ya mapato basi hayakupaswa kuwepo hapa.

Sasa kwa sababu ni Shirika ingekuwa ni idara basi ingeingia kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina na ingebidi sasa ioneshwe kwenye mapato kwamba hayo ndiyo mapato yanayokadiriwa kupatikana. Lakini kwa kuwa ni Shirika inatajwa tu na wala hayaingii kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina, kwa sababu zinazoingia kwenye buku hili kama ni sehemu ya mapato zinaingia kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina. Kwa hivyo, kwa Shirika unazitaja tu na zinaingia kwenye *accounts* zao za Shirika na wamepewa uwezo wa kukusanya na kutumia nadhani ndio hivyo.

Waheshimiwa Wajumbe, kama kuna hoja nyengine katika hiyo, lakini nadhani hali iko hivyo kwa kiasi nilivyofahamu. Sasa kama si kweli

kilichokusanywa huko na hilo ni suala jengine ambalo Mhe. Waziri atatusaidia.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, mimi ninayo risiti ya tarehe 17 Mei, ambayo inaonesha kwamba *TIGO* imelipa dola 12,000 na zikaingizwa *BoT* na baadaye zikawa *transferred* kwenda Hazina na risiti ninazo na kwa hili sina wasi wasi.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri, kwa hiyo zimekwenda Hazina sio kwenye *accounts* za Shirika, maana hapa ndipo inapokuja tatizo. Sasa kama zimekwenda Hazina ilipaswa ziingie kwenye buku hili, lakini kama zingekwenda kwenye *accounts* za Shirika hazikupaswa ziwemo kwenye buku hili. Kwa hivyo, risiti unazo lakini fedha zimekwenda Hazina nadhani hapa mufanye utaratibu Mhe. Waziri wa Fedha azitoe fedha hizo ziende kwenye Shirika nadhani ndio utaratibu. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba sheria mpya ambayo imetungwa na Baraza la Wawakilishi imeanza kufanya kazi tarehe 17 Juni na hiyo ndio inayoipa mamlaka Shirika kukusanya na kutumia mapato yake yenyewe na risiti niliyonayo ya tarehe 17 Mei, mukitupa fedha za kutumia *ahlan wasahlan* tunazitaka, lakini kisheria haiwezekani. *(Vicheko/Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, nafikiri sasa iko wazi kwamba Sheria ya Shirika ilikuwa bado haijafanya kazi, hivyo fedha zilibidi ziende Hazina. *(Makofi)*

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, mimi naishukuru serikali kwa umakini. Lakini kuna haja ya *PAC* kuliangalia hili jambo, maana yake sheria inayofanya kazi hapa ni Sheria ya Fedha na Kanuni zake. Kwa hivyo, nashauri *PAC* iangalie, ili kumsaidia Mhe. Waziri wa Fedha na inawezekana kwa sababu *EPA* walikwenda na risiti gunia 10, lakini fedha hazikuingia Hazina. *(Makofi)*

Sasa kuwa na risiti na ukadhani zimeingia Hazina sio ushahidi. Kutokana na hali hiyo, nashauri kwamba *PAC* ifanye kazi na imsaidie Mhe. Waziri wa Fedha na isijekuwa ni ile *EPA* kwamba imeingia risiti gunia zima lakini hakuna fedha. Mhe. Mwenyekiti, tuendelee. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, hiyo kazi ya *PAC* hatutoi amri hapa, isipokuwa *PAC* wanayo hiari yao kutizama huko. Tunaendelea. *(Makofi)*

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Mwenyekiti, na mimi naomba muongozo kidogo kwenye hotuba ya Mhe. Waziri kwenye Kampuni ya Uunganishaji Maudhui *ZNEWS page* ya 31 kuna mgao wa hisa, ambao ni makusanyo nayo hayo, kwamba 60 *percent* ya Wizara ya Fedha na Wizara inapata 20 *percent* na ZBC 20 *percent*, na wala *ZBC* sina tatizo nayo tayari nimeshapata maelezo. Lakini nataka kujua hii 20 *percent* ambayo inaingia kwenye Wizara hatuioni kwenye kitabu cha makadirio, hivyo nataka kujua inaingia wapi? *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri, nadhani umemfahamu.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, naomba arudie kidogo.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Mwenyekiti, katika hotuba ya Mhe. Waziri *page* ya 31 kuhusu Kampuni ya Uunganishaji Maudhui *ZNEWS* kuna mgao wa hisa, ambapo Ofisi ya Rais Fedha na hiyo sina *reference* nayo, lakini Shirika la Utangazaji nimeshapata maelezo na nimeshafahamu. Vile vile kuna mgao wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo , ambayo ni 20 *percent*. Kwa hivyo, nataka kujua haya makusanyo yanaingia wapi? *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri, nadhani umemfahamu na labda utusaidie.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, nafikiri hivi sasa tuko kwenye vifungu na Mjumbe anapouliza anapaswa aseme na kifungu. Sasa hoja ambayo Mhe. Mjumbe ameiuliza hivi sasa basi jioni inaingia pahala gani na kwenye kifungu gani, kwa sababu tukienda hivi itakuwa hatumalizi kupitisha vifungu.

Pili tulikuwa tumeshamaliza kupitisha hivi vifungu na Mhe. Hija Hassan Hija alichouliza ni kwamba ameona baadhi ya kifungu hakina fedha ndio tukarudi na tulipaswa kumaliza swali la Mhe. Hija Hassan Hija na halafu hii hoja ya vifungu iwe imekwisha.

Kwa hivyo, mimi nawaomba sana Waheshimia Wajumbe, kwamba tuzingatie utaratibu, vyenginevyo tutakuwa tunaogelea tu na wala hatujui tunaogelea kwenye kifungu kipi. Mhe. Mwenyekiti, atakapofika pahala hiyo hoja yake ina mankiti ya kuulizwa mwahala mwengine itajibiwa, lakini kwa hapa nadhani tulikuwa tumeshamaliza Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, nafikiri anachoeleza Mhe. Waziri ni kusaidia kitu tu kwamba tuwe tunaendelea na pia tuwe makini pale

kifungu kinachohusika kama kuna Mjumbe anayo hoja, basi awahi hapo na tukipita tena kufanya *reverse* inakuwa kidogo ngumu, maana hii ni sawa sawa na ndege ambayo iko hewani ukifanya *reverse* inaanguka. Kwa hivyo, tuendelee na Mhe. Mjumbe tafuta kifungu kinachohusika. *(Makofi)*

FUNGU 31 – KAMISHENI YA UTALII

Kifungu 0201	Utawala Unguja	1,397,522,000/=
Kifungu 0301	Ofisi Kuu Pemba	230,478,000/=
Jumla ya Fungu		**1,628,000,000/=**

FUNGU 42 – WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, UTALII NA MICHEZO

Kifungu 0201

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi hii. Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nikichangia Shirika la Utangazaji nilisema kwamba nitazuia kifungu kuhusiana na deni la haki miliki. Vile vile wakati Mhe. Waziri alipokuwa akitoa maelezo hapa nilimsikiliza vizuri na alisema kwamba kuanzia mwaka huu wa fedha ndio watalipa deni lile.

Mhe. Mwenyekiti, Afisi ya Haki Miliki inatarajia kufanya mgawayo wa fedha hizi Agosti mwaka huu, na Wizara ya Katiba na Sheria imeshatupa mualiko rasmi Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kwenda kushuhudia mgawanyo huo. *(Makofi)*

Sasa nataka Mhe. Waziri anihakikishie hapa kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, ni lini kabla ya mgawanyo huo kufanyika atalipa deni la Shirika la Utangazaji kwa Afisi ya Haki Miliki? *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru ni kweli kwamba Mhe. Wanu Hafidh Ameir na mimi nilimjibu kutokana na hali halisi tuliyonayo na wala sikuweza kumdanganya kama ningeweza kulipa kesho, kwa sababu ningekuwa ninamdanganya na kulidanganya Baraza hili, jambo ambalo ni kosa.

Kwa kweli nilichomuahidi ni kwamba kwa sababu kuanzia tarehe 17, Juni Shirika sasa ndio linaanza kazi rasmi na tunayo madeni mengi sana na tumepanga kuyapunguza hayo. Sasa kwa umuhimu wa chombo hichi ambacho Mhe. Mjumbe anakizungumza basi tunasema kwamba tutajitahidi

katika robo ya pili ambayo inaanza Oktoba. Kwa hivyo, watustahamilie na tutajitahidi mwezi wa Oktoba, basi malipo yote tutahakikisha tunalipa Afisi ya Haki Miliki.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa Waheshimiwa Wajumbe, wakati walipokuwa wakichangia walimmwagia sifa sana Mhe. Waziri, basi na mimi sitaki kumtia doa na ninaamini kwamba deni lile atalitilia maanani na atakwenda kulilipa, pamoja na kutilia maanani kuwa kudhulumu fedha zile wanawadhulumu wasanii wanyonge sana akina Halikuniki na wenzake kupata kile ambacho wanakifanyia kazi kutokana na jasho lao. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, naomba tuendelee nikiamini kwamba Mhe. Waziri atalipa deni. *(Makofi)*

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nilizuia fungu hili na kusema kuwa huenda nikalizuia na nikaondoa shilingi yangu, sasa nataka niirejeshe atakaponipa majibu mazuri.

Mhe. Mwenyekiti, nilihuzunika sana na nilisema kwa masikitiko makubwa sana kuhusu ndugu zetu hawa watu wa *ZBC* pato ambalo wanalolipwa ni dogo na halafu isitoshe wanakopwa. Lakini kwa kweli Mhe. Mwenyekiti maelezo aliyoyaeleza Mhe. Waziri alikiri hapo na akasema kwamba atafuatilia, na mwaka jana nakumbuka Mhe. Mwenyekiti nilieleza pia sasa ile *history* inajirejea tena.

Sasa leo nataka kumhakikishia Mhe. Waziri kuwa *ZBC* si wa kufikia hali hiyo ya kuwa masikini wa kukosa kulipwa hawa haki yao ya hiyo ya shilingi 5,000/= wanayokopwa na halafu wakaongezewa. Mhe. Mwenyekiti, naomba majibu mazuri, ili Mhe. Waziri apate aendelee basi aniambie kuwa kauli ile ya kuwa nitafuatilia sitaki, isipokuwa nataka aniambie kwamba tukipitisha hapa leo basi hawa watu wanalipwa mafao yao ya nyuma na pia wanaongezwa. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, naelewa *concern* ya Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, kwamba yeye ni mmoja katika mpiganaji wa haki za watu sana. *(Makofi)*

Katika suala hili ninachomuahidi ni kwamba kama kuna madeni ya nyuma, kwa sababu mimi kumbukumbu nilizonazo ni kwamba tumewalipa mpaka tarehe 25 mwezi huu, ndipo niliposema pale ninawadai na wala hawanidai na huko nyuma walikua wanadai vikao viwili vitatu na tumepiga hatua.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hili kama kuna madeni basi tutahakikisha wanalipwa na wiki hii nitajitahidi walipwe kama tulivyozungumza na Ofisi ya Baraza na kikao lini mwisho kama tarehe na nimezungumza na Mhe. Rashid akaniambia kinaweza kufika tarehe 10 mwezi ujao, basi kama ni hivyo nitalipa mpaka tarehe 10 mwezi ujao kikao hichi. *(Makofi)*

Kwa hivyo, naomba anipitishie na wiki hii tukijaaliwa tutauliza Ofisi ya Baraza na kama ikiwa tarehe 10, basi Mhe. Mwenyekiti mpaka tarehe 10 tutawalipa na kuhusu kuwaongezea ninaomba tuje tuzungumze katika kikao kijacho nitahakikisha kwamba wameongezewa. *(Makofi)*

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, amekiri kuwa atawalipa Mhe. Waziri wiki ijayo na wala sina tatizo nalo moja hilo.

Lakini kauli ya kuongezewa ananiambia tutalizungumza kwenye kikao kijacho. Sasa mimi naendelea kulizuia fungu hili mpaka kikao kijacho nimuachie, ili kupata kuona haki ambayo imetendeka.

Je, Mhe. Waziri atakuwa radhi na hali hiyo? Kama atakuwa radhi basi mimi niendelee na shilingi yangu mfukoni na wala nisiiachie hapa, isipokuwa aniambie kuwa wiki ijayo na nitaridhika sana Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu huyu Mhe. Waziri ni mkweli kama anavyotusifu na sisi, kwani Mhe. Waziri ni mtu kweli, mzuri na anawapenda wafanyakazi wake na siri zao tumezipata sisi kwamba anawapenda sana, basi hata hili ashindwe kuwaongezea *at least* angalau kuwatilia angalau shilingi 20,000/=.

Mhe. Mwenyekiti, naomba anipe jawabu zuri, ili niweze kumruhusu na huu ni mwezi Mtukufu wa Ramadhani Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri, hebu rudia yale majibu uliyotoa wakati ulipotoa maelezo hapa, maana yalikuwa majibu mazuri sana. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, nilisema kwamba nitajitahidi kwamba kwa vile tunatajariwa kuanza kukusanya mapato katika kipindi hichi, basi Shirika litakuwa na uwezo wa kuwalipa vijana. Kwa hivyo, tutahakikisha kwamba tunashirikiana na Bodi kuwaongezea. Kwa hivyo, hilo ndilo nikasema kwa sababu hayo si maamuzi yangu kama Waziri, na lazima nishirikiane na Bodi ya Shirika na itakuwa ninakwenda kinyume na Bodi ya Shirika jambo ambalo ni kosa kisheria. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, ndipo pale niliposema kwamba kikao kijacho Bodi itakuwa tumeshaunda na tayari tumeshashauriana na Bodi kwamba lazima wataongezewa tukijaaliwa. Kutokana na hali hiyo, naomba anistahamilie kwamba nitahakikisha kuwa nitawalipa mpaka mwisho wa kikao hichi, lakini baada ya kushauriana na Bodi wataongezewa tukijaaliwa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, nadhani sasa umesikia vizuri, maana hii ni pamoja na masuala ya taratibu.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze kwa masuala haya alijibu kweli pale vizuri lakini nilitaka nimsikie mimi mwenyewe kuwa ananitamkia mimi Mjumbe niliyetoa hoja. Nimshukuru sana Mhe. Waziri na tupo naye pamoja tutafuatilia hili suala baada ya makusanyo. Ahsante sana.

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, wakati nikichangia kwa maandishi nilitaka kujua suala zima la kauli au tamko la Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika kuendeleza michezo, kwa kuufanyia ukarabati uwanja wa Mnazi Mmoja kwa ajili ya kujenga michirizi ya maji na kujenga ule uwanja. Tamko lile au kauli ile bado haijatekelezwa.

Je, ni lini kauli ile ya Mhe. Rais wetu mpendwa itatekelezwa?

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Ni kweli Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Nassor Salim ambaye ni mdau wa michezo mkubwa alilizungumza hili. Tatizo ni kwamba kiwanja anachokizungumza kipo chini ya Mamlaka ya Manispaa. Mimi tu Idara ya Habari na Watu wangu wa Kamisheni ya Utamaduni kuanza kwenda pale na ma-*bulldozer* itakuwa ni mtihani kidogo.

Ninachomuahidi kwamba tutakaa pamoja na Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu, leo Waziri muhusika hapa bahati mbaya amedharurika. Tukae tuangalie namna gani tutalitekeleza agizo la Mhe. Rais. Hatuna tatizo hata kidogo. Kwa vile kipo chini ya Mamlaka hiyo naomba tupe muda tuendelee kushirikiana. Kimsingi tutalizungumza lakini hatujafika pahali pa kulitekeleza.

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Mwenyekiti, kwa vile Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo, amesema kwamba atashirikiana na Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Ikulu na kulifanyia kazi suala hili, kwa sababu suala la michezo lipo katika Wizara yake, kwa hivyo kwa majibu yake haya na mimi nina imani kwamba kazi hii itatekelezwa. Tuendelee Mheshimiwa.

Kifungu 0201	Idara ya Mipango Sera na Utafiti	180,000,000
Kifungu 0301	Afisi Kuu Pemba	628,234,000
Kifungu 0401		

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, uliponiuliza sasa hizo hoja nyengine, nikakwambia vifungu vipo vingi tutafika tu.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba nimshukuru sana Mhe. Waziri kwa kuwa muwazi kuja kutujibu hoja zetu. Kwa sababu hiyo nafikiri kwa upande wangu mimi hoja nyingi nyengine zitakuwa zimejibika. Lakini kuna suala moja kwa hapa, lile nililozuilia shilingi mia halijafika, wakati wake ukifika nitasimama. Hapa nilikuwa nina hoja ambayo niliiulizia, kuhusu suala zima la kukabidhiwa Agape matangazo ya dijitali.

Mhe. Mwenyekiti, nimemsikiliza kwa kina Mhe. Waziri alipokuwa akizijibu hoja zangu kuhusu kutotekelezwa kwa masharti mbali mbali ambayo yalikuwemo katika mkataba ule, na nikahoji ufanisi wake. Katika mchango wangu pia niliuliza ingawa sitaki katika hilo aingie maana sitaki kumfanya aingie katika mtihani wa kuteleza baina ya watendaji wake wepi wana maslahi gani katika mambo haya mpaka wametukwamisha mpaka leo. Lakini nimepata matatizo Mhe. Mwenyekiti katika majibu yake katika baadhi ya vifungu.

Katika nyaraka mbali mbali, namuhakikishia Mhe. Mwenyekiti kwamba sizungumzi kwa maneno tu, nyaraka zote za Agape na maelezo yao na utafiti wao waliofanya ninazo hapa. Inaonesha Mhe. Mwenyekiti, kwamba kulikuwa na masharti mbali mbali. Katika niliyoyataja ilikuwa ni pamoja na kwanza kujenga vituo vipya viwili Wete na Kitogani.

Katika majibu yake Mhe. Waziri kasema kutokana na kutofika huduma kule na minara ipo katika maeneo mengine ingeweza kutumika minara inayohusika na *E-Government* kupitia Mkonga wa Taifa.

Vile vile kulikuwa kuna suala la majenereta. Lugha aliyoitumia ni kwamba limo na litafanyiwa kazi. Sijui kama huo mkataba unatakiwa ukamilishwe ndani ya muda gani. Lakini vile vile Mhe. Mwenyekiti, katika masharti yaliyokuwemo mle ndani ilikuwa ni pamoja na kuhakikisha kwamba wanaweka mitambo ambayo inaitwa *digital* DVBT2 ambayo ingewezesha 100% *coverage* wanavyosema katika maelezo yao ya visiwa viwili Unguja na Pemba, ingawa Pemba bado haipati matangazo haya.

Kwa hivyo, yapo masharti mengi Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu katika kifungu sitaki nirejee tena katika kuchangia ambayo yanaonekana kwamba hayakutimizwa katika suala zima la utekelezwaji wa mkataba huu ambao uliahidiwa kwamba ungekamilika ndani ya siku 90.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema katika mchango wangu, uliahidiwa mradi huu ungekamilika mwisho wa Disemba, ukaahidiwa mpaka mwisho wa Februari haukukamilika, sasa hivi tuko mwezi wa Julai unamalizika, tunaingia mwaka mwengine wa fedha, bado wananchi wanalalamika juu ya huduma kwamba hazipatikani.

Sasa nilikuwa nataka Mhe. Waziri anisaidie. Kwa sababu katika mikataba hii na *recommendation* nyingi zilizowekwa, moja katika watu ambao aliwaleta Mhe. Waziri kampuni kutoka Kenya ilikuja kuzifanyia tathmini zile kampuni mbali mbali ambazo zilikuwa zimeomba. Waliagiza kwamba ile kampuni waliyoi-*recommend* Agape, itekeleze masharti yake kwa mujibu wa maandishi waliyopeleka wenyewe kwenye Wizara.

Sasa nataka maelezo ya Waziri, kwa vile Agape inaonekana imeshindwa, Wizara yake ina mpango gani juu ya makubaliano hayo yaliyokuwa yamefikiwa baina yao na Agape? Ahsante.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru. Si kweli kwamba Agape imeshindwa katika mkataba ambao tumekubaliana. Sisi tumekubaliana na Agape kwamba ajenge mitambo, *infrastructure;* na mpaka tarehe 8 Januari karibu *infrastructure* zote zipo tayari. Kutokana na tatizo moja la kwamba tulivyokubaliana, mwanzo tulikubaliana kwamba *design* za *project* ni kwamba tutumie mkonga, nimesema mara ya tatu kwamba ndiyo chombo cha kusafirishia mawimbi. Tokea Januari wanatuuliza Agape mkonga uko wapi, mkonga haujawa tayari, anatusubiri sisi na mpaka leo mkonga haujawa tayari.

Tukamlazimisha Agape lazima aweke vifaa ambavyo vitawezesha dijitali kuanza. Kwa hivyo tukamlazimisha *a-improve capacity* za *microwave*. *Microwave* ambazo tulidhani kama ni *backup* zilikuwa *only 8 channels*. Lakini sisi tumeahidi 36 *channels* tusingeweza kuanza na *8 channels*, kwa hivyo tukalazimisha *a-improve capacity* ya *microwave* kwa vituo vyote, akafanya hivyo.

Ninachosema kwamba Mwenyekiti, mtambo mkuu uliokuwepo pale *headed in* ni DVBT2, *consultant* amethibitisha hilo. Unaoweza kuchukua matangazo ya *High Definition* kutoka *Standard Definition* ya hivi sasa, hilo halina tatizo.

Tutafanya marekebisho kwa sababu tutatumia mkonga, wenye mkonga ni *E-Government* wakatwambia mkijenga minara mengine mwahali mwengine mtatulazimisha sisi tupeleke *Optic fiber* katika minara yenu. Kwa hivyo tafadhilini tumieni minara ambayo sisi tuna hakika nayo ambayo *optic fiber* imeshafika. Tukafanya ajenda kwamba badala ya kujenga minara kwa sababu minara ambayo *E-Government* anayo tayari imeshafika *optic fiber*, tungejenga kwengine labda Wete kwengine, ingebidi sasa yeye na watu wa *E-Goverment* watapata tabu ya ku- *extend* mpaka maeneo ambako hayapo. Kwa hivyo kwa vile minara ambayo tayari inayo *optic fiber* tukamlazimisha badala ya Wete kenda Konde, badala ya Kizimkazi tukaenda Muyuni. Kuhakikisha tunakwenda mwahali ambamo *optic fiber* imo.

Hilo halikuwa na tatizo, ukosekanaji wa matangazo ni kwa sababu hiyo ni kwamba nimezungumza *technically* kwamba sisi tunasafirisha kwa *microwave* mpaka Nungwi. Mnara wa Nungwi unayumba sana *microwave* iliyopo Kusini Pemba ile iliyokuwepo juu haioni, inakwenda inaona inaondoka kwa sababu ya myumbo mkubwa. Ndio sababu iliyofanya Pemba kuwa na *no signal* mara nyingi. Unguja hakuna *no signal*, wanaonesha king'amui chetu Mhe. Salmin Awadh anaangalia ni kizuri hakina matatizo hata kidogo.

Nadhani Waheshimiwa Wawakilishi wenzangu hapa mmoja juzi alinambia kibovu. Sasa nasema kwamba kinafanya kazi vizuri. Tumezungumza na Mhe. Waziri wa Fedha mwenyewe yupo pale ananisikiliza, tulikubaliana, Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora tumekubaliana kwamba tuwashe *optic fibre* ili tupate chombo cha kusafirishia mawimbi yetu ili Pemba na Unguja kuwe na *efficiency* ya dijitali. Tatizo tulilonalo ni kwamba sasa hivi yupo bwana Agape anasubiri sisi tupeleke *optic fiber* kwenye vituo ili aweke vifaa vya kuunganisha *optic fiber* na *transmitter* zilizokuwemo kwenye vituo vyote sita Muyuni, Masingini, Nungwi na Mkoroshoni, Konde na Kichunjuu. Kwa hivyo anatusubiri sisi Mheshimiwa.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, naendelea kumshukuru Mhe. Waziri kwa maelezo yake lakini bado nina matatizo. Hili la Mkonga na *fiber optic* na *E-Government* sitaki kuliingilia, nakumbuka kuna hoja yangu inaning'inia kwako Mwenyekiti, naisubiri Wizara ya Fedha kwa hamu sana tukijaaliwa. Nakumbuka umeniahidi utaisimamia, kwa hivyo sitaki kuingia huko kabisa. Lakini nataka nikubali kwamba hata katika nyaraka ambazo nimebahatika kuzipata kwamba lilikuwa ni jukumu la Wizara ya Habari kwa niaba ya serikali kuweka haya baadhi ya mambo ambayo Agape ayapate ili atekekele masharti yake. Kwa hivyo huko sitaki kuingia.

Swali langu litakuwa moja tu kwamba Serikali hii, Mhe. Mwenyekiti, ni moja. Itakuwa ni jambo la ajabu kwamba Ofisi ya Uratibu ya SMZ imefeli, sitaki kuamini kwamba Mhe. Mohammed Aboud kafeli, kwamba iwe kinachofanywa na sehemu moja serikali mkono wa pili wa serikali haujui. Kwamba vipi mmejikubalisha katika mkataba ambao una siku maalum, ambao unategemea mahitaji kutoka sehemu nyengine ambayo hayajakamilika mpaka leo. Tukisema kama serikali hii inatupeleka katika matumizi mabaya ya fedha za walipa kodi Wawakilishi wa wananchi tutakuwa tunakosea Mhe. Mwenyekiti?

Mhe. Mwenyekiti, hoja juu ya maeneo ambayo naomba anisaidie kwangu mimi si muhimu sana ingawa katika kutajwa vimetajwa vituo hivyo Wete na Kitogani lakini hilo si muhimu kwangu mimi. Mimi ninachohitaji hii *analysis* iliyofanywa na *Thornhead Engineering System Ltd* ya Kenya, wameileta wao kuja ku-*survey* na wao waka-*recommend* Agape, ilikuwa inasema kwamba katika Agape kwamba *"They are offering a system network of six sites to cover the whole Zanzibar and Pemba Islands"*, ningetaka hilo Waziri kwanza anithibitishie kama hilo linafanyika.

Lakini jengine sitaki kurejesha mjadala huu nataka kurudia tena katika kifungu changu cha msingi ambacho nimekisimamia. Mhe. Mwenyekiti, katika suala la matangazo baina ya Pemba na Unguja kuna hoja aliyonijibu yeye sasa hivi hapa, kwamba mawimbi yanatoka hapa yakifika Nungwi yana matatizo. Lakini kuna *transmission* mbili katika visiwa hivi na tangu wakati huo wa *analogue* ilikuwa hivyo hivyo kuna *transmission* ya Unguja na kuna *transmission* ya Pemba. Hata hilo wameli-*consider* wao. Mheshimiwa waraka mwengine ambao umeandaliwa na wao A*gape* na *Electronikka Africa* kuwapelekea Wizara matatizo yao.

Katika ukurasa nafikiri wa pili wanasema *"To upgrade the present Masingini and Chake Chake analogy transmission to digital DVB T2"*. Hilo ni moja lakini sitaki kusema sana kwa sababu ya muda Mhe. Mwenyekiti. Hili la pili muhimu sana.

La pili katika mengi yaliyoorodheshwa zinafika hoja kumi mimi nataka kuzisema hizi mbili tu, inasema kwamba, *"To provide 15gb gain Antennas for each transmission site, this will guarantee 100% coverage over the Islands."* Hoja yangu Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba katika vifungu hivi ukitizama kwanza ilikuwa zote mbili zipewe nguvu, ya Masingini na ya Chake Chake. Ili kama ilivyokuwa tunakotoka kwa *analogue* kwamba matangazo ya Pemba na Unguja kila moja ina sehemu yake ya kurushia matangazo na ahakikishe kwamba matangazo hayo yanawafika wananchi wote.

Masharti haya Mheshimiwa sijui kama wamewakwaza wao Wizara au ni kushindwa kwa Agape. Hoja yangu ipo pale pale kwamba vipi masharti ya Mkataba huo yameshindwa kutekelezwa na kwa nini bado tuing'ang'anie kampuni ambayo inaonekana imeshindwa kazi. Kama ni serikali ndiyo iliyoshindwa kuwapa mahitaji yao ambayo yangepelekea kukamilisha upande wao wa mkataba basi serikali itwambie hapa kwamba iliingia katika mkataba bila ya kushauriana na vikundi mbali mbali au mikono mbali mbali ya serikali ambayo ilipaswa itekeleze mahitaji yake ndipo mkataba huo uweze kutekelezeka. Waziri anisaidie au serikali kwa ujumla inisaidie katika hili.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, kwanza vituo sita vyote vimewekwa vifaa kama alivyosema eneo la Muyuni, ipo Kusini Unguja anajua, Masingini imewekwa vifaa, Nungwi imewekwa vifaa, kituo chengine ni Chunjuu, Mkoroshoni na Konde. Mtambo mkuu umewekwa Rahaleo imejengwa kwa ajili hiyo. Kuhusu *capacity* ya *system* iliyokuwepo Masingini na Mkoroshoni vile vituo viwili ndio *hub* ya kila kituo, kikiharibika Masingini Unguja yote imefeli, na hivyo hivyo ikiharibika Mkoroshoni. Pana antena ambazo zimekuwa *upgraded* kuliko maeneo mengine.

Mhe. Mwenyekiti, mimi mwenyewe nafuatilia kwa karibu na sidanganyi katika hili. Nina maarifa kidogo ya kujua wapi kipo kituo. Kwa hiyo namuhakikishia Mhe. Mjumbe kwamba hatujafanya kosa katika hili. Masuala madogo madogo ya kuhakikisha kwamba tunakwenda vizuri hayo ni mambo ya kawaida katika *technical work* yoyote ile hata hao waliotangulia hata Wajerumani wanatwambia sisi tulichukua miaka minane hatujapata *perception* 100% ya dijitali. Sisi Mheshimiwa tumeanza *just* mwezi wa 10, mwezi wa pili tayari dijitali Zanzibar tulidhania watu wanatupongeza, angalieni nchi nyengine labda Sychelles, Mauritius, Comoro, miaka mingapi wamechukua kabla hawajaanzisha dijitali sisi *only four months* kwa kweli tunahisi tumefanya kazi kubwa.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, sitaki nimsumbue hata kidogo Waziri huyu ambaye ni mpenzi mkubwa wa mama yangu Bi Asha Bakari Makame, na kwa sababu alitulilia hali sana jana Mhe. Bi Asha kwamba tumpe nafasi na Mhe. Waziri akalitambua hilo akapongeza katika hotuba yake mama yake kwa kumuombea. Kwa hivyo nataka nimuhakikishie kabisa kwamba sina nia ya ukaidi wala kukwamisha mjadala huu.

Mhe. Mwenyekiti, ili niruhusu tuendelee nasema, Mhe. Waziri atakuwa analijua hilo kwamba katika hiyo *analysis* tunayoisema ambayo iliangalia *HUAWEI*, wengine waliotoa mapendekezo humu wamo *Dexing Digital*

Technology lakini katika hii Agape ilikuwa inasema, *"Delivery period is 90 days after signing the contract"* na nyaraka hizo walimpatia wao Wizara huyu *consultant* waliyemleta kuja kuzihakiki ili awape ushauri Wizara. Mimi nilikuwa nataka atuhakikishie kama *90 days* tumeshavuka *from the day of the signing of the contract*. Kwa sababu aliomba sana mimi basi angalau anambie mambo mawili moja kwamba haya mambo ya mawimbi, kwa sababu katika kitu ambacho hakipendezi Mhe. Mwenyekiti, nchi hii ina visiwa viwili pacha, kunapokuwa kuna upande mmoja una huduma na upande mwengine hakuna huduma inawafanya wale watu wa kisiwa chengine wajihisi kwamba wale ni watoto wa kambo. Sisi tuna matatizo yetu tele Unguja katika mradi huu huu lakini kule Pemba wana matatizo makubwa sana. Sasa angalau anambie mambo mawili ili niruhusu tuendelee.

Moja, kwamba anambie katika kushughulikia matatizo kwa sababu kama kungekuwa kuna matatizo Nungwi Agape ni wataalamu walipaswa wafanye *survey* wayajue yote hayo kabla hawajaingia mkataba. Ukisha kujikubalisha kwenye mkataba maana yake umesha-*survey* mambo yote ndio ukaji-*commit* kufanya jambo hilo. Kwa hivyo anambie lini wanategemea suala hili litamalizwa na wananchi wa Pemba wataona kama wanavyoona wenzao wananchi wa Unguja. Ingawa na sisi tunaona kwa kusuasua lakini angalau tumeshapiga hatua, hilo moja.

Lakini la pili, anihakikishie kwamba atalifuatilia kwa kina hili, kwa sababu nalisema kwa kulizungumza hapa, lakini zipo taarifa nyengine kwamba kwa sababu lile nililolisema kwenye mchango kwamba kuna mgongano baina ya uongozi wa Wizara ambao ulitaka kuokoa fedha kwa kutaka Agape iliyokuwa na fedha kidogo na watendaji wa Shirika ambao walikuwa na kampuni yao mfukoni waliokuwa wakiitaka, na kwamba sasa kuna kufanyiana hujuma. Sasa walipeleleze hili, isijekuwa mradi huu hawaendi mbele kwa sababu kuna hujuma ndani baina ya watu ambao kampuni yao ya mfukoni haikufanikiwa. Kwa sababu hiyo, nataka afuatilie sana suala la uongozi wa Shirika kutaka kuandaa mkataba mwengine na Star Times wakati huku itabidi ulipwe huo, na wakati huo huo tayari serikali imeshaingia makubaliano na Agape.

Kwa hivyo, haya mambo mawili yafuatiliwe. Moja anambie lini Pemba nao hili suala la Nungwi na Mkoani litamaliza ili matangazo yafike vizuri. Leo ndugu zetu wa Pemba wanatwambia nyie mnafaidi huko sisi hatufaidi kuona matangazo ya Baraza letu la Wawakilishi.

La pili anambie kwamba kama kuna harufu yoyote ya hujuma baina ya sehemu mbili hizi aifuatilie na baadaye atupe majibu katika Baraza hili kwa niaba ya wananchi wa Zanzibar, kwamba asikubali watu kutumia nafasi zao

kukwamisha suala ambalo linapelekea huduma mbovu kwa wananchi wa Zanzibar kwa sababu tu watu wamekosa *percentage* zao katika mifuko yao. Naomba Mheshimiwa anihakikishie hayo mawili halafu tutaendelea.

Mhe. Spika: Lini na hili la matatizo ya mivutano kulifuatilia ili kujua hali halisi.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, suala la lini gumu kidogo. Kama nilivyosema kwamba *efficiency* itapatikana baada ya mkonga kukamilika lakini wakati haya yanaendelea, Ofisi ya Katibu Mkuu imewasiliana na Agape, imeleta wahandisi wao wengine kutoka Afrika ya Kusini leo tokea jana wapo Nungwi, na kikosi chengine kipo Kichunjuu kupunguza *impact* ya mnara katika matangazo. Sisi Mhe. Mwenyekiti, linatughasi sana, tunajitahidi kupunguza hiyo athari. Ninachomuomba kwamba mpaka keso asubuhi ninaweza nikampa taarifa hizi jitihada ambazo zipo katika *field* hivi sasa zinazochukuliwa kupunguza athari. Tunafanya kazi 24 *hours* kuhakikisha kwamba tumepata. Lakini hili la *fiber optic* bado tunashauriana na Mhe. Waziri wa Nchi Fedha na Mhe. Waziri wa Nchi Utawala Bora, akinambia kesho kutwa, akinambia baada ya wiki moja na sisi tutapiga mbio kuhakikisha tunaweka kila kitu sawa ili *effeciency* iwe iko asilimia 100.

Mhe. Spika: Mheshimiwa kuna maelezo zaidi?

Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Habari naomba kidogo niongezee lile suala la msingi ambalo Mhe. Ismail Jussa Mwakilishi wangu wa Jimbo la Mji Mkongwe alilotaka maelezo.

Nataka niseme kwa kifupi ni kwamba tatizo la picha Pemba ili liweze kutatuka kwa 100% *solution* yake ni kukamilisha *fiber optic*. Sasa hivi tunatumia *macrowave* na iko kwenye mnara. Kwa kule Pemba pale Nungwi ndio mnara wanaotumia kuelekea *signal* Pemba pana upepo mkubwa sana. Wenzetu Agape pamoja na ma-*engineer* wetu wamekubaliana kwamba waishushe ile *macrowave*, badala ya kukaa juu zaidi waishushe chini kili kupunguza ule upepo na ile *signal* kupotea kwa upande wa Pemba.

Lakini tumegundua kwamba *solution* yake ya kudumu ni kuweka *fiber optic*. Tayari tumeshawasiliana na kitengo cha *E-Government* wana vituo zaidi ya sabini wanataka kutupelekea *fiber optic*, lakini tumewambia kwamba vituo vya mwanzo waanze ni hivi vya *television*. Nina imani Mhe. Mwenyekiti,

kwamba katika wiki moja au mbili zijazo tutapata hasa utaratibu wao wa kazi unaanzaje kwa wenzetu wa kitengo cha *E-Government*.

Pili ambalo nataka nimsaidie Mhe. Jussa kwamba Agape wameshamaliza kazi kwa asilimia 91. Tumewaomba wenzetu wa Wizara na ma-*engineer* wao wafuatilie *component by component* kwa mujibu wa mkataba wetu tuone kwamba kiasi gani wamekamilisha chini ya asilimia 91 inaonekana wamekamilisha.

Tatu nataka nimsaidie Mhe. Jussa na Waheshimiwa Wawakilishi wengine kwamba sisi serikali kwa upande wetu tumemlipa Agape kwa asilimia 75 tuone kwamba hatulipi tu, tunalipa kwa mujibu wa kazi zilizokamilika. Bado tunazo pesa za Agape na tutaendelea kumlipa kwa mujibu wa kazi iliyokamilika.

Namuomba sana Mhe. Jussa kama kuna maelezo ya ziada ambayo atakayoyahitajia sasa hivi sio Wizara tu inayofuatilia mradi huu pamoja na Wizara ya Fedha pamoja na Wizara ya Utumishi wa Umma, sote kwa pamoja tunaufuatilia mradi huu ili tuweze kuona mradi umekamilika kwa wakati na kwa *quality* na kwa mujibu wa mkataba.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, hoja hii imechukua muda mrefu lakini naamini kama Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Matumizi unathamini kwamba tunafanya haya kwa maslahi ya wananchi katika kuzilinda haki zao na fedha zao. Nashukuru na maelezo ya Mhe. Waziri mwenyewe wa Wizara lakini sasa hivi Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, akiahidi kwamba anafanya hiyo kazi ambayo yawe ndio maelezo yangu ya kufungia kwamba masharti ya mkataba ule yatafuatiliwa na kuhakikishwa kwamba yanatimizwa kifungu kwa kifungu yote yaliyokuwemo mle ndani na *component* zake zote.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu tuna kawaida moja, huwa tunapewa maelezo na huwa tunayaweka, tuseme kama ni angalizo, kwamba tuendelee lakini baadaye Baraza hili kwa niaba ya wananchi lije lipewe taarifa. Lakini mara nyingi tukishakupitisha Bajeti Mawaziri huwa wanasahau, wanaona tena kazi imekwisha, yanatiwa mkobani tena tunangoja tuje kuulizana mpaka mwakani. Mhe. Mwenyekiti, kama unavyojua kwamba tuna kikao kimoja tu cha kuja kuhoji tena katika Kamati ambacho kipo mwakani mwezi wa Machi.

Kwa hivyo, nilikuwa naomba hili kwa sababu ni suala linalowagusa sana wananchi na limeshazungumzwa sana, na nina hakika serikali inajua hivyo kwa sababu na wao masikio yao yapo huko nje, kwa hivyo tuje tupewe

maelezo juu ya ukamilishaji wa mradi huu ambao kama nilivyosema ilipaswa ukamilike ndani ya siku 90 lakini mpaka leo umekwama. Sasa kama walikuwa wamekwamisha wao kwa sababu ya *E-Government* yake Mhe. Omar Yussuf Mzee (Waziri wa Nchi, Fedha) akifika na yeye atakuja kutujibu. Ninachosema kwamba tunahitaji tuone.

Pili, sikupata majibu lakini sitaki majibu tena, namwambia tu Mhe. Waziri namtanabahisha tena afuatilie suala la hujuma. Kama watu wameweza kufikiria kuingia mkataba na Star Times katika kuwa na Kituo cha *Digital* wakati serikali tayari imeanzisha kituo chake cha dijitali inaonekana kuna watu kama tunavyosema wana maslahi yao, hawakuridhika na masuala haya na wanaweza kukwamisha kwa makusudi tu ili kwa ajili ya kumkomoa Waziri au kuikomoa serikali au pengine Katibu Mkuu, kwa sababu tu kafanya maamuzi kinyume na maslahi yao.

Kwa hivyo nasema na haya sitaki tena anyanyuke Mhe. Waziri, nasema tuendelee lakini afuatilie yote hayo. Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana.

Mhe. Asha Bakari Makame: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwanza nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuwezesha kutufikisha leo kuigawa nusu ya Ramadhani Mwezi Mtukufu na Mwenyezi Mungu atujaalie tuimalize.

Mhe. Mwenyekiti, sina nia ya kuzuia fungu wala sitakuwa na nia hiyo. Kwanza nimshukuru Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri ambayo ameyajibu katika masuala ambayo nimechangia. Lakini pia nimshukuru sana Mhe. Waziri ni mwepesi sana wa kusoma mazingira ya kila Wizara nimpongeze sana, lakini nataka anieleze tu nilizungumza kuhusu hawa vijana wetu waliomo ndani hawa kwamba wapate posho maalum, kalizungumza kwa jumla lakini katika hayo madeni waliyokuwa wanadai lakini hili posho maalum bado sijalisikia. Hebu Mhe. Waziri wangu sifa zote ninazokupa basi angalau wasaidie hawa vijana wapate hili posho maalum, kwa sababu na wao ni miongoni mwa wanaopata shida kukaa humu, baada ya Spika, anapokaa pale kwamba haendi pahala popote, sisi tunatokatoka Mhe. Mwenyekiti nikusifu sana unapokaa pale, ni mtu pekee ambaye unahimili kipindi cha kuanzia asubuhi saa tatu mpaka saa nane au kuzidisha wakati. Nikupongeze sana Mheshimiwa.

Lakini wa pili ni hawa vijana wetu, ukitoka wewe wanakuja hawa vijana wetu sisi angalau tunachupachupa, basi nawaombea posho maalum na ipo hapa kwenye mambo ya Utumishi na Uendeshaji, ipo nakuomba Mhe. Waziri.

Mhe. Mwenyekiti: Posho maalum si kwa Spika, kwa vijana hawa.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti nilidhania labda na Spika umo kumbe. Mhe. Mwenyekiti ninakushukuru nayaelewa mazingatio ya Mhe. Asha Bakari ni mama yetu Barazani kwa hivyo anaangalia matatizo ambayo vijana wetu wa *camera* ambao wanasimama sana. Basi kama nilivyolichukua lile naomba ahadi kwamba nitazungumza na Bodi tuliweke katika utaratibu ambao na wao wapate posho maalum kwa kazi yao ngumu watu wa *camera*, narudia kwamba watu wa *camera* ndio ambao wanasimama kwa hivyo nitaahidi hivyo.

Mhe. Asha Bakari Makame: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti kwa majibu ambayo Mhe. Waziri amenijibu lakini mimi nina ushauri kidogo nitamuomba sana Mhe. Waziri hayo mafungu yao ya posho maalum lilete huku Baraza la Wawakilishi, ili wasipate usumbufu wa kuja kukaa na madeni tena huko kama madeni yaliyokuwepo, namuomba sana Mheshimiwa ni ushauri mzuri huo asiukatae, ni ushauri ambao utakuwa haumsumbui yeye wala haiwasumbui Wizara au Idara husika inayowalipa hawa vijana. Ninakuomba sana Mhe. Waziri lichukuliwe posho lao hawa maalum liletwe huku wakati wa vikao wapate posho lao lisiwekwe tena likawa ndio madeni yaliyokuja yakazuka hayo madeni mengine ninamuomba sana Mheshimiwa waziri.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti kumbuka tulifanya safari ya Baraza ukanichukua Ghana tulichojifunza Ghana ni kwamba Bunge la Ghana lina Idara ya Habari, mimi nitafurahi sana kwamba Ofisi ya Katibu wa Baraza itashughulikia maposho ya vijana hawa kwa kweli mie mtanisaidia sana.

Mhe. Asha Bakari Makame: Kanifurahisha Mhe. Waziri Mhe. Mwenyekiti, pamoja kwamba kuna ugumu wake, lakini ni vyema kwa sababu Waziri wa Fedha yupo hapa ni vizuri wakakubaliana na Waziri wa Utumishi ni vizuri likakubalika. Kwa sababu tufanye kitu ambacho kinaweza kikasaidia sio kusumbua.

Na hawa vijana wetu kwa kweli wana haki za msingi kabisa. Mimi likishakubalika hilo lakini kwa sababu umetiliwa bajeti yako Mhe. Waziri ni vizuri kwanza ile bajeti yako ikawa *transferred* huku vijana wetu ikawa kila wakati wa kikao wakalipwa bila ya kupitia Idara yao itasaidia Mheshimiwa. Sina zaidi ya hayo mkae mlizungumze Mhe. Waziri ili muelewane. Baada ya hayo sina nia ya kuzuia kifungu ilikuwa nipate maelekezo na mimi nitoe ushauri wangu.

Mhe. Mwenyekiti: Ni maelewano ya pamoja na ofisi yangu maana msinitwishe mzigo halafu mkaja mkanidai ikawa sina fedha, kwa hivyo ni suala la kukaa pamoja. Ila niseme tu kwamba uwezekano wa jambo upo, kwa sababu tulikuwa tunawalipa wale mafundi mitambo wakati ule tuliokuwa tunawaazima TVZ, tulikuwa tunawasaidia posho fulani. Kwa hivyo na hili tulitizame labda katika mtizamo kama huo, lakini ni suala la kukaa pamoja.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti na mimi nataka nikushukuru lakini vile vile nataka nimshukuru sana Mhe. Waziri kwa mujibu wa ufafanuzi alivyokuwa akijibu hoja zangu zilikuwa chache kabisa. Sasa niliwahi kutoa ushauri kwa Mhe.Waziri na huu hakuweza kunitolea ufafanuzi; na ushauri wangu ulikuwa katika suala zima la matatizo yanayojitokeza katika ZBC hasa kutokana na uchakavu wa vifaa mbali mbali na ukosefu wa vifaa mbali mbali. Na vile vile nilieleza kwamba tulipoondoka katika Idara tukaja katika Shirika hatukujiandaa na kutafuta *capital* ambayo tungeliingia hasa katika zile nguvu za Shirika inavyotakiwa kuanzishwa. Na ukiangalia Mhe. Mwenyekiti haipendezi hata kidogo kuona kwamba vyombo vya habari binafsi vinafanya kazi kwa ufanisi mkubwa ukilinganisha na vyombo vyetu hivi vya taifa. Kwa hivyo wananchi wanakuwa wanajiuliza sana kwamba ina maana watu binafsi wanaweza kuendesha shughuli zao vizuri kuliko taasisi za serikali.

Sasa nilimshauri Mhe. Waziri na nikajaribu kusema kwamba tatizo la mfumo wetu wa bajeti kwamba tunachangia bajeti hizi za Wizara wakati tayari ile bajeti kuu ambayo tumeshapitisha yale mafungu kitu ambacho hatuwezi tukaondoa fungu upande mmoja ukapelekwa upande mwengine. Hili ingawa niliomba Kiti chako tujaribu kukaa kama Kamati ya Uongozi tuangalie namna gani tunaweza tukarekebisha ili pale ambapo panapohitajika kutiwa nyama tuweze kufanya hivyo huko siku za mbele.

Sasa hoja yangu iko hapa, Mhe. Mwenyekiti ili ZBC isiwe tiro kama alivyotaka Mhe. Rais, na Mhe. Waziri hapa alikariri kauli hiyo je, yuko tayari kuandaa *paper* na kuipeleka kwenye *cabinet*, lakini vile vile kumuomba Mhe. Waziri wa Fedha ambaye ndio mkuu wa nchi kuipa mtaji ZBC ili ikaweza kukamilisha yale mambo ambayo yanayohitajika ili ZBC baadae tunapokuja mwakani tusiizungumze katika kasoro za uchakavu wa vifaa tuangalie masuala mengine ya kiutendaji. Sasa hili Mhe. Waziri kwa bahati mambo yalikuwa mengi hakuwahi kulitolea ufafanuzi labda ningelipata maelezo ya ziada.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti ni kweli kwamba Mhe. Hamza alizungumza suala hilo ni kwamba serikali

iliunda Tume ya kulichunguza Shirika la ZBC na ripoti yake imewasilishwa serikalini tukaijadili kwa upana katika *cabinet*. Yale yote ambayo yanaathiri *efficiency* ya Shirika yalizungumzwa na wataalam wakatupa *feed back* kubwa, kwa hivyo serikali inajua nini sasa hivi inahitaji. Na tayari kuna mambo yanaanza kufanyiwa kazi. Mfano serikali ina mpango wa karibuni kabisa wa kujenga studio mbili mpya za kisasa moja Karume House na moja Mkoroshoni Pemba kwa shilingi zaidi ya bilioni moja hizo zitatoka katika mfuko mkuu wa serikali. Kufanya hivyo ni kuhakikisha kwamba ZBC iwe na uwezo wa kutosha wa zana za kisasa kwa kufanya shughuli zake. Lakini kama nilivyosema kabla kwamba ZBC inahitaji *reform* kubwa yenye wafanyakazi wengi, kwa hivyo hayo ni mambo ambayo Bodi mpya ambayo inakuja ndio mambo ya msingi ambayo yatayashughulikia. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti wa Wenyeviti asiwe na wasiwasi ni kwamba serikali ishafanya kazi kubwa kuhusu kulichunguza Shirika na tushaijadili kwa muda mrefu katika serikali na kuna mapendekezo ambayo yametolewa, serikali imeshayapitisha tunaanza kuyafanyia kazi.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti kwa kweli ninamshukuru sana Mhe. Waziri na kwa kuwa hili suala tayari limeshazungumzwa kwenye *cabinet* na yametoka maelezo ya kitaalam naamni serikali sasa hivi wamo katika kuyafanyia kazi. Sasa ni dogo tu ambalo nataka kupata ufafanuzi ambalo ukiacha hayo mageuzi makubwa ya baadae ambayo tunataka kufanya ndani ya Shirika letu la ZBC, lakini kuna suala ambalo limo ndani ya uwezo wao suala la *scheme* ya hawa wafanyakazi wa ZBC sijui hili ambalo ninaamini kwamba bila ya kuliingiza katika ile *package* kubwa ambayo itakuwa na gharama kubwa lakini alau hili la kuandaa hii *scheme* ambayo itaweza kuwapa moyo na kuwatia motisha vijana kuweza kutumia maarifa yao katika kuboresha utendaji katika ZBC, jee hili la *scheme* labda Mhe. Waziri ana mpango nalo gani.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti ni kweli kwamba wafanyakazi wa ZBC wana maslahi madogo tumeliangalia hilo na hata hiyo *comprehensive report* hilo nalo lilizunguzwa. Kwa hivyo ni suala la Bodi, kwa hivyo Bodi ikikaa miongoni mwa shughuli zake za mwanzo ni kufanya *restructuring* ya wafanyakazi kuangalia nani ataiwafiki, nani yuko wapi na kwa kiwango gani cha mshahara ambacho na maposho mengine atalipwa.

Kwa hivyo hiyo ni kazi ya Bodi ambayo tukishaiteua ndio miongoni mwa majukumu ya mwanzo ambayo watayasimamia kwa kushirikiana, na watafanya mapendekezo yao basi wataipelekea Ofisi ya Utawala Bora,

Kamisheni ya Utumishi wa Umma kwa ajili ya ku-*approve* na watu wapate mpunga wao watumie Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti nadhani Mheshimiwa sahibu wangu, mwalimu wangu Waziri wa Utumishi wa Umma anazisikia hizi hoja zetu na ninamuomba na hili ninamtaja kwa makusudi kwa sababu maslahi mengi yanakuwa yanazunguzwa yanakwama katika Utumishi wa Umma. Sasa Mheshimiwa Mwenyekiti kwanza tunakuomba mwakani bajeti ya Utumishi wa Umma ukiweke mwisho kabla ya Wizara ya Fedha ili, hayo ni mapendekezo ya baada lakini kitu ambacho ninachokiomba sana Mhe. Mwenyekiti tumeshazungumza sana suala zima la maslahi ya wafanyakazi wa ZBC, sasa mimi nadhani Mhe. Waziri mimi ninamuamini sana, ni mtu ambaye mchapa kazi mzuri alifanyie haraka basi *at least* na hiyo Bodi aifanyie haraka na ile Bodi si vibaya wakaja wakachungulia hizi *hansard* zetu *at least* wakaona kwamba hawa Waheshimiwa ambao mara nyingi wanatumwa na hao wananchi miongoni mwao wakiwa wafanyakazi wa ZBC wanatekelezewa vipi haya maslahi yao.

Mhe. Mwenyekiti chombo hiki kikifanya kazi vizuri, Mhe. Mwenyekiti kwa kweli nchi yetu itakaa pazuri sana. Ninakushukuru Mhe. Mwenyekiti naomba tuendelee.

Kifungu 0401 Utumishi na Uendeshaji	996,494,000
Kifungu 0402 Chuo cha Habari	305,000,000
Kifungu 0403 Mchango wa Gazeti la Zanzibar Leo	856,000,000
Kifungu 0404 Chuo cha Maendeleo ya Utalii Zanzibar	420,000,000
Kifungu 0701 Idara ya Habari Maelezo	

Mhe. Subeit Khamis Faki: Kuna kifungu 0501 Sauti ya Tanzania Zanzibar, nasema kuna vifungu naona keshaviruka haya tuendelee mbele tutakutana huko usoni.

Kifungu 0701 Idara ya Habari Maelezo	273,660,000
Kifungu 0702	

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti ninashukuru kunipa nafasi ya pili kwa leo kuhusiana na fungu hili la Shirika la Utangazaji Zanzibar. Samahani Mwenyekiti nimekimbia hoja yangu katika Shirika zamani.

Kifungu 0702 Tume ya Utangazaji	173,000,000
Kifungu 0703 Idara ya Habari Maelezo Pemba	40,000,000

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti ninakushukuru na nimshukuru Mhe. Waziri kwa jinsi ambavyo anatujibu masuala yetu nilipozungumza Shirika la Utangazaji Zanzibar ZBC nilikuwa na hoja maalum juu ya wafanyakazi wetu ambao ni mafundi, mafundi hawa bila ya wao hakuna matangazo Zanzibar. Nikasema kwamba ni kweli elimu zao ni za ufundi Mikunguni *form four* miaka 1970. Lakini hadi hii leo bado wana maslahi madogo sana jambo ambalo linawafanya mafundi wetu kuondoka nchini, nikatoa mfano kwamba mmoja kastaafu juzi hapa Zanzibar lakini amekwenda Tanzania Bara na analipwa mshahara mara nne ya fundi aliyepo hapa Zanzibar, sasa naomba maelezo Mhe. Waziri akizingatia kwamba hawa ni mafundi ndio ambao wanaongoza mitambo yote ya Zanzibar na ndio wanaotoa mafunzo kwa wafanyakazi wengine kwa sekta hiyo ya Utangazaji.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti ni kweli Mhe. Hija alizungumza suala hili na ninajua kwa nini analizungumza yeye mwenyewe ni muhitimu wa Chuo cha Ufundi cha Karume, kwa hivyo anajua athari za wahitimu wa aina yake wanaopata matatizo. Sasa tatizo hili limejitokeza Wizarani, kuanzia Shirikani na sisi hatujalikalia kitako tumelisimamia, tumewaandikia barua wenzetu wanaohusiana na kufanya *promotion* ya wafanyakazi kuanzia tarehe 14 Februari, nina barua hapa imeandikwa, kuna barua nyengine ya tarehe 18 Februari, imeandikwa na barua ya tarehe 4 Februari na tarehe 18 Julai, yote haya ni mawasiliano baina ya kwanza Shirika, Wizara na Wizara. Kwa hivyo ninachomuomba afahamu na akubali kwamba bado katika Wizara tunalishughulikia, na kwa mawasiliano mazuri na Wizara inayoshughulikia Utumishi wa Umma tunaamini kwamba watapatiwa haki yao.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti kwanza nataka nikubaliane na Mhe. Waziri kwa maelezo ambayo ameyatoa. Kwanza nataka nitoe taarifa rasmi kwenye Baraza hili tukufu kwamba vyeti vya FTC kama cha Mhe. Hija serikali kwa kipindi kama cha mwaka mmoja sasa nyuma inatambua rasmi kwamba cheti kile kina *level* ya diploma rasmi inatambua hivyo. Na taasisi nyingi ambazo zina watumishi wanaotoka katika chuo hicho wanalipwa maslahi yao kwa mujibu wa *standard* ya cheti hicho cha diploma. Kwa hivyo nataka nimhakikishie Mhe. Hija na Waheshimiwa wengine kwamba vyeti hivyo serikali imevitambua rasmi na baadhi ya taasisi zimeweza kutekeleza hilo toleo; kwa maana ya agizo na wanapata maslahi yao.

Lakini jengine nataka nilizungumzie kwa wafanyakazi ambao wana *experience* kwa muda mrefu katika kuitumikia nchi hii. Kama nilivyosema katika bajeti yangu kwamba kwenye bajeti hii serikali imetenga karibu shilingi milioni mia tano kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya wafanyakazi ambao wana uzoefu kwa muda mrefu lakini hawana shahada ambazo zinaweza zikawapa kipato kizuri. Lakini kwa hawa mafundi wa Shirika la Habari sasa hivi ni lazima wafuate lile toleo kwa sababu toleo limetolewa kwa serikali nzima; kwamba kila mwenye mtumishi ambaye ana cheti cha *level* ya FTC basi alipwe katika ngazi ya diploma, kwa hivyo hilo limemalizika sio hoja tena.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti ninakushukuru kwamba FTC sasa diploma ingawa mimi nimepita ninashukuru sana, lakini nasema hivi Mhe. Mwenyekiti tusiangalie kwa mtazamo wa karibu, mimi ninamfahamu sana Mhe. Waziri wa Utumishi na naamini kwamba ana nia safi, watu wetu hawa ambao wamebakia 5 kati ya 5 wanastaafu mwakani. Na kwa tabia ya serikali yetu kwamba jambo dogo lina miaka 5, maana yake watastaafu na mshahara ambao hautawasaidia kiinua mgongo. Mhe. Mwenyekiti watumishi hao waliandika barua tangu tarehe 7 Novemba 2011 mwaka juzi wanalalamika. Katibu Mkuu kupitia bwana Joseph J. Kilangi akawajibu tarehe 27 Novemba, 2011 mwaka juzi kwamba suala lako linashughulikiwa litapata ufumbuzi karibuni. Miaka 3 karibuni, maana yake nini? Maana yake kwamba watastaafu mwakani wenzetu hawa hawana haki yoyote.

Mhe. Mwenyekiti mimi naomba Mhe. Waziri wa Utumishi achukue juhudi maalum za dhati kabisa nje ya toleo la serikali kuwamalizia matatizo yao hawa wafanyakazi watano; ambao kwa kweli ndio Zanzibar kwenye matangazo ni hawa ili tusisubiri hilo toleo la serikali kwa jumla tukawapoteza. Nasema kwamba mmoja amestaafu juzi amekimbia familia iko Unguja ameenda Dar es Salaam lakini anapewa laki sita, na hao watano waliobakia mwaka jana walikuwa wanapewa 274000 lakini wamepunguziwa mshahara sasa hivi wanapewa chini ya 274000. Mhe. Mwenyekiti namuomba Waziri wa Utumishi kwa hivi kama ambavyo mengine anatusaidia hebu atoe tamko kwa hili maalum, na serikali ikubali kwa hili maalum tuwaenzi hawa watu wetu, vyenginevyo hawa watashindwa sasa hivi wao ndio walimu pale ZBC. Mimi nina digrii yangu nikienda sifanyi kazi mpaka yule bwana anipe mafunzo.

Naomba tamko la serikali kwa hili tuwasaidie. Na kuwaenzi watu watano si jambo kubwa Mhe. Mwenyekiti, naomba Mhe. Waziri tusaidie. Wana cheti cha *form four* cha Mikunguni sio FTC kama mimi na Mhe. Said Ali Mbarouk

ni Mikunguni lakini ni cheti cha maana tokea mwaka 1970. Mhe. Nakuomba unisaidie, naomba kauli yako Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mheshimiwa ninakubaliana na Mhe. Hija nitalichukulia kwa umakini na ukaribu zaidi ili wanyakazi hao waweze kupata maslahi yao.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti ninakushukuru na mimi kunipa fursa hii. Nilipochangia nilimuuliza Mhe. Waziri kuhusu suala la redio kutosikilikana kule kisiwani Pemba, na bahati nzuri nimefuatilia hili suala mara nyingi sana nilikuwa ninamfuata yeye mwenyewe nikimwambia, lakini Mhe. Waziri alikuwa ananambia kwamba kapeleka wajumbe wake ili kufanya utafiti redio inasikilikana. Lakini na mimi nimekwenda kufanya utafiti mpaka nimerudi jana Pemba mimi Sauti ya Tanzania Zanzibar kwa Pemba haisikilikani labda unasikia kuchemka tu, ama kwa kuchemka kama watu wanaopika mikate shaaaa lakini haisikilikani chochote, na kama utapata neno moja basi huwezi kupata neno la pili.

Sasa ninaomba Mhe. Waziri atueleze ni lini wananchi nao watafaidika? Sisi tusiwe ringi ya nyuma kila siku watu wa Pemba. Kwa hivyo naomba na sisi tufaidike, kwa sababu ringi ya nyuma maisha inakaa nyuma haisogei mbele. Kwa hivyo namuomba atueleze kama ni lini wananchi wa Pemba watafaidika na kusikia japo hiyo redio kwa sababu televisheni haipatikani lakini hii redio angalau watu huwa wanafaidi nayo haipatikani. Cha kusikitisha ni kwamba Zenji FM inasikika, Bomba FM inasikika, Chuchu FM inasikika lakini redio ya serikali haisikilikani inachemka tu kama watu wanachoma mikate. Ni lini hasa tutafaidika na sisi?

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti sijui Mhe. Subeit alikwenda wapi kufanya utafiti huo maana kuna siku hapa alichangia vizuri siku ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Kufika hapo nje kapelekewa *message* na watu tumekusikia unachangia vizuri sana hongera. Na watu wake wapo Micheweni. Sasa sijui alikwenda Micheweni ipi? Mimi ninavyoelewa Pemba inapatikana, *medium wave* inafanya kazi inapatikana na FM inapatikana. Sasa kama alikwenda Micheweni ya Kenya sawa, lakini Micheweni ya Pemba inafika ZBC.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti kwanza mimi sifanyi masihara, nasema kwa ukweli kabisa tena niko *serious*. Mhe. Mwenyekiti, labda tukamchukulie redio tuje tumkusunyie hapa ambazo kuwa tumesharudi nazo ukiwa hapa unasikia lakini ukifika kule hupati chochote, zipo hapa tunazo kama tumkusanyie tuje tumpe au tuende pamoja sisi na yeye

tukafungue pamoja hiyo redio halafu tusikie. Sisi tunachotaka ni kwamba watu wafaidike matunda yao ya Mapinduzi, wapate redio kama wanavyopata huku, haisikilikani redio kule kusikia kule kuchemka si kusikia, watu hawapati kitu chochote, yachemka tu redio na kule kuchemka sio kusikia, kusikia ni kusikia lile linalosemwa.

Mhe. Mwenyekiti, sisi hapa sasa hivi tupo Baraza la Wawakilishi, watu wanataka kusikia Wawakilishi wao wanafanya nini hawapati, wakipata neno moja la pili halipatikani tena, unaweza ukasikia neno moja basi la pili hupati tena, atuambie mafundi wake na yeye mwenyewe watajitahidi vipi kuhakikisha kama redio inasikilikana Pemba?

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, siku aliyonambia Mhe. Subeit kwamba Pemba redio haipatikani, niliagiza Mhandisi wa ZBC Redio aende Pemba na akaenda kwa ndege, akafanya *survey* kutoka Kusini mpaka Kaskazini Pemba. Jibu ambalo amenileta ni kwamba ZBC inapatikana, sasa kama amenidanganya mimi niko tayari baada ya Baraza kufungwa mimi na yeye Mhe. Subeit, twende tukaangalie hali halisi huko.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana Mhe. Waziri, tayari mimi na yeye tufanye safari tuende na tuchukue redio yetu tuende tukafungue tusikilize.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi nilipokuwa nikichangia katika Shirika hili la Utangazaji nilikuwa nikiwatetea hawa wafanyakazi ambao kwa kweli msingi wa Shirika hili ni kuwa na watu wataalamu ambao huwa wanaendelea kututoka siku hadi siku kwa kwenda katika mashirika mengine.

Na Mhe. Waziri, alinijibu nashukuru kwa kunipa moyo, na kama alivyotanguliza yeye mwenyewe kusema huu ni mwezi wa Ramadhani na tuko katika kumi la maghfira, na kweli Mwenyezi Mungu atughufirie makosa yetu tuliyoyafanya kwa kujua na kwa kutojua. Lakini vile nilitaka hapa niingizie kwamba hii ni ahadi aliyoitoa Mhe. Waziri, kwamba ataitekeleza na Mwenyezi Mungu anasema *waaufu bil ahad innal ahada kaana mas-uula*, kwa hiyo namuomba sana Mhe. Waziri, hilo aweze kulizingatia, kwa sababu Mwenyezi Mungu anatuhimiza tutekeleze ahadi zetu na hakika kila ahadi tutaulizwa, kwa hiyo sina pingamizi na hilo nasubiri utekelezaji.

Mhe. Mwenyekiti, pia nilieleza jinsi tunavyopenda chombo chetu hiki kukiangalia lakini vipindi vyake bado vinaonekana ni vile kwa vile ambavyo

vinatuchosha sisi kuviangalia, lakini lengo letu *ZBC* ikuwe ili tuweze kufaidika wananchi kwa kuona vipindi vinafuatiliwa na kubadilika mara kwa mara ili tuweze kukipenda chombo chetu hiki. Lakini hapa sikupata jawabu nzuri na nilitoa mfano katika utangulizi pale asubuhi inapofunguliwa ZBC, *qur-an* kila siku panasomwa mahala pale pale ambapo yule anayesoma ni Sheikh mkubwa na ana uwezo wa kurikodi tena sehemu nyengine na nyengine ili tukaweza kufaidika, namuomba Mhe. Waziri, aweze kunipatia ufumbuzi ni lini basi tutaweza kufanikiwa kuviboresha hivi vipindi vyetu ili tuweze kufaidika na *ZBC* yetu?

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, namshukuru Mhe.bi Panya, kwanza ninamuahidi kwamba ahadi niliyoitoa kuhusu Juma Mmanga nitaisimamia, hiyo haina matatizo. Na suala la kuimarika kwa vipindi hilo pia naomba nimshukuru tena Mhe. bi Panya, kwa kweli huwa hasubiri hapa Barazani, maneno haya ameshaniambia mara nyingi tukiwa kabla ya bajeti kwamba rekebisha kidogo, rekebisha hivi namshukuru sana na mara zote anaponambia basi naenda kwa watendaji wangu na kunatokea *improvement* kidogo, lakini kwa sababu amelizungumza suala hili katika eneo zito basi mimi nitakaa na watendaji wangu kuona namna gani tutarekebisha na tutaimarisha mambo ya matangazo katika vipindi vyetu vya redio na *television,* namuahidi hiyo na Ramadhani yote hii.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru na kwa kuwa wenzangu wengi wameweza kusema sifa za Waziri huyu kwamba kila tunapomshauri jambo anafuatilia, na kweli ushahidi kwa sababu mimi hata zile dhikri ambazo zinatiwa asubuhi niliwahi kumwambia Mheshimiwa basi Mtume huyu katamani maji tu hakutamani mambo mengine kwa kuwafanyia watu wake, nikahisi mara tumeletewa maulidi ya homu, mara kasida nyengine, nikafarijika nikajua kweli anafuatialia. Kwa hivyo sina pingamizi tuendelee.

Kifungu 0704	Shirika la Utangazaji Zanzibar-Unguja	1,900,000,000/=
Kifungu 0705	Shirika la Utangazaji Zanzibar- Pemba	200,000,000/=
Kifungu 1101	Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale Unguja	

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, katika mchango wangu niligusa sana eneo hili na namshukuru Mhe. Waziri kwa ufafanuzi wake na akasikitika kwamba sikupongeza alivyolipamba jengo la Makumbusho pale Mnazi Mmoja, basi naomba nichukue fursa hii kuweza kumpongeza kwa kazi

nzuri aliyoifanya. Lakini kasahau tu wakati tulipokuwa katika Kamati nilipongeza nikayataja hayo yaliyokuwa yamebakia.

Mhe. Mwenyekiti, nilizungumza kwa jumla kuhusu haja ya nchi yetu kutunga sheria yake kwa kuyatunza majengo haya, nashukuru katika maelezo na kwa sababu katika mchango wangu nilijikita katika mifano miwili ambayo ipo katika Jimbo langu; wa Jumba la Beit el Ajaaib na Makumbusho ya kasri ambayo kaahidi kwamba itafanyiwa kazi hasa kwa sababu sasa kuna mazungumzo na Serikali ya Oman, na kwa sababu tuna ushirikiano wa pamoja na sehemu ya sheria yetu ambayo inatuunganisha, sasa mimi nilikuwa nataka maelezo kwamba haya mazungumzo yapo katika hatua gani katika kuyatunza haya, kwa sababu hali yake ni mbaya.

Mhe.Spika, mimi ninaweza kusema kwamba au mimi khofu yangu kubwa sana ni kwamba nikitizama jengo lile la Makumbusho ya kasri lilivyo, lile la Beit el Ajaaib kwa sababu lilipata maswaiba ya kuanguka upande mmoja labda ndio rehema yake kwamba sasa angalau litakuwa linatizamwa kwa karibu, lakini pale pana makumbusho ya nchi, wageni wakija wanatembelea na pale mbele ukitizama na hasa pale pana Ofisi ya Baraza la Mapinduzi, ukiona ule uchafu na kifusi kinachopita pale mbele ambacho kimekaa miaka hakitengenezwi kimekaa tu, pamoja na hali yenyewe mbaya pale, dari lilivyo kwa ufupi Mhe. Mwenyekiti hali hairidhishi kabisa. Sasa nilikuwa ninataka nisaidiwe imefikia hatua gani? Kwa sababu nina khofu yasije kuwa kama ile nyumba iliyokuwa ya Mkuu wa Wilaya Pemba, iliahidiwa vile vile na Serikali ya Oman tukaambiwa sijui imefikia wapi.

Sasa na haya ninataka aniambie kwamba isije kuwa tunaacha kufanya wajibu wetu kwa kungojea hili ambalo hatujui litachukua miaka mingapi na ukizingatia kwamba miradi hii imeshaombewa fedha sana, sasa ninataka anisaidie hasa haya majengo haya mawili ambayo yapo katika Jimbo langu. Mengi nimeyatembelea yote hayaridhishi lakini haya mawili hasa, haya mazungumzo yapo katika hatua gani na tunakusudia kufanya nini? Vile vile hasa tukizingatia anayeingia Zanzibar kwa njia ya bahari kwanza anayakabili haya katika sura na taswira ya nchi yetu.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, ukweli kwamba Mhe. Jussa, amekuwa akikerwa sana na hali ya matunzo ya Makumbusho. Ilikuwa tukizungumza sana mimi na yeye katika hili na huwa tunalifuatilia sana. Lakini ukweli ulivyo ni kwamba majengo haya mawili yalijengwa kwa teknolojia ya kizamani sana na bahati mbaya au nzuri inakuwa *subjected* na mandhari ya bahari yenye upepo wa bahari mkubwa. Na *study* ndogo iliyofanywa ni kwamba maji ya bahari yanaingia

katika zile *sewage system* yanafika mpaka chini ya majengo yale. Kwa hiyo inahitaji umadhubuti mkubwa wa kuyashughulikia, kupiga rangi juu juu tu kidogo haisaidii, itakuwa kama unatia dawa kwenye kiganja, inataka marekebisho hasa na hilo lengo letu Wizarani, tufanye *study* kubwa; *comprehensive study* kuangalia majengo haya yana uwezo gani, *life time* yake ikoje na kuyanusuru vipi.

Mhe. Mwenyekiti, hivyo tumezungumza na wenzetu wa Oman, tumeanza na Balozi hapa, akaleta wataalamu wake wahandisi tumekaa nao kwa muda, wameshafanya *feasibility study* na wameondoka na ripoti wamekuja tena wamekaa na wahandisi wetu. Kwa hiyo tulivyokubaliana kama nilivyosema kwamba la msingi tutafanya *study* kubwa majengo haya mawili halafu tutaandaa *design*, halafu tutazitafuta fedha tutafanya matengenezo. Tumekubaliana kwamba tuhimizane sisi tumepewa kazi tunafanya na wao wamepewa kazi wanafanya, na baada ya muda mfupi tunakuja tunaunda kamati baada ya mwezi mtukufu wa Ramadhani tutakutana pamoja kwa kushughulikia majengo haya mawili.

Mhe. Mwenyekiti, mimi katika maeneo ambayo hayanipi raha kubakia vile yalivyo. Hivyo namuomba Mhe. Jussa, tuendelee kuhimizana sote tunalishughulikia. Lakini wakati huo huo tunatumia bajeti yetu *other charges* tunayopewa kuhakikisha kwamba yale matengenezo madogo madogo hatusubiri mradi mkubwa, kwa sababu ukiacha kutia dawa katika kidonda kidogo huko mbele unaweza kupata jaraha kubwa. Kwa hiyo pamoja na hali hiyo hatusubiri mradi mkubwa lakini tunajaribu kutengeneza.

Kwa hiyo tunategemea baada ya Ramadhani kumaliza wenzetu wanafunga na sisi tunafunga mawasiliano yataendelea, tumekubaliana kuwa tuwasiliane mara kwa mara kwa ajili hiyo. Mkurugenzi wa Makumbusho anafanya kazi hii pamoja na Mkurugenzi wa Mji Mkongwe kwa hapa Zanzibar na wao wana timu yao tunafanya kazi kwa pamoja.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hiyo hili tunalisimamia lakini tunaendelea kufanya kazi katika kuhifadhi makumbusho; ni *icon* ya historia ya Zanzibar na lazima yawepo.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa maelezo ya Mhe. Waziri. Mimi nataka nitahadharishe jambo moja, nakubali maelezo yake yote, lakini sikubali na katika hili simlaumu yeye wala siulaumu uongozi wa Wizara yake uliokuwepo hivi sasa, lakini ni matokeo ya miaka mingi ya kuyatupa na kutoyashughulikia. Mhe. Mwenyekiti, ni tatizo la kutokuwa na utamaduni wa utunzaji wa vitu vyetu, wala tusiende mbali pale pale chini ya

majengo haya tumekabidhiwa bustani ya Forodhani ambayo haiko kwake lakini hebu tukaitazame ilivyokuwa chini ya Aga Khan na baada ya kurejeshwa Serikalini, hata majani yameshapiga njano yote, mwanzo yalikuwa yaking'ara kwa rangi ya kijani kama Chama cha Mhe. Mohammed Aboud.

Sasa tuna tatizo la kutosimamia utunzaji wa vitu vyetu baada ya kukabidhiwa katika mikono yetu. Sasa mimi nimuombe kama nilivyosema sitaki kumlaumu yeye na uongozi wake kwa sababu wameyakuta haya, lakini ukisema mandhari ya bahari na upepo wenye chumvi Mhe. Mwenyekiti, tangu yalipojengwa yamekaa kwa miaka pale, lakini yalikuwa yakitunzwa, kwa sababu mambo yale huwezi ukangoja mpaka liharibike ndio ukatengeneze, na wahenga wametufundisha vizuri sana wanasema *usipoziba ufa utajenga ukuta*, sasa kama hizi nyumba hatuzizibi hizi ndio inakuja kuporomoka kama lilivyoporomoka mwaka jana Beit el Ajaaib.

Mhe. Mwenyekiti, sasa kwa sababu yuko yeye na ni Waziri makini tumemsifu sote humu na uongozi wake basi ajitahidi wakati wanashughulikia haya makubwa ya kungoja mradi huu basi angalau na utunzaji uwe unaendelea. Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema, kasema ukitia rangi haitoshelezi, ni kweli na kama anazungumzia athari yake ni kwamba kuna maji yanayopenya chini kule, kuna mradi ambao mpaka leo tunapewa maneno tarehe tu kila siku, mradi wa kukamilisha sehemu ya pili ya kujenga uzio au ukuta ule wa bahari katika eneo lile mpaka Mizingani, na nikasema ikiwa mkono wa Serikali haufanyi kazi na mwengine utakuwa haufanyi kwa sababu haushirikiani pamoja, kwa hiyo ninachosema aufanyie kazi lakini angalau Mhe. Mwenyekiti, basi ile mandhari ya usafi, maana yake unaingia mle mavumbi yaliyojaa unasema humu mna wafanyakazi wa kazi ya kusafisha? Haya na ni majengo ambayo yanatembelewa na wageni wetu sana, lakini hata rangi na kama rangi hatuna basi hata chokaa inatushinda?

Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia majengo yale inafika pahala, kuna taa kajitolea mfanyabiashara binafsi ni aibu, taa tu zile za nje pale, kajitolea mfanyabiashara binafsi kuziweka basi hata ile kuwashwa utaona siku moja zinawaka siku mbili haziwaki, hatushughuliki na vitu kama hivyo. Sasa nilikuwa ninauomba uongozi wake wafanye kazi ambayo wamewekewa pale. Tunapopiga kelele katika maslahi yao lakini na wao wawajibike katika maeneo hayo. Sasa nasisitiza tena kwamba utunzaji angalau kuyapa sura na haiba ya kuvutia wakati tunangoja matengenezo makubwa na ukamilishaji wa miradi mengine ya Serikali ambayo ikikamilika itahakikisha usalama wa majengo yale. Baada ya maelezo hayo ninasema tuendelee.

Kifungu 1101 Idara ya Makumbusho na Mambo
ya Kale Unguja 609,408,000/=

Kifungu 1102

Mhe. Salma Mohammed Ali: Mhe. Mwenyekiti, wakati ninachangia nilizungumzia kuhusu hali mbaya ya Makumbusho Pemba na vile vile nilizungumzia tafauti iliyopo ya asilimia 24 na 94; Makumbusho Pemba ina asilimia 24 na Makumbusho ya Unguja ina asilimia 94. Mhe. Waziri, wakati wa majibu aliniambia kwamba asilimia 24 ilitokana na baada ya mkato wa meli. Mhe. Mwenyekiti, mimi sina tatizo hapa kwa sababu sote tunajua umuhimu wa meli. Lakini suala langu hapa kwanza lipo katika ile asilimia 94 ya Unguja wao hawakuchangia katika ule mkato wa meli? Na vile vile nilitaka nielezwe katika bajeti ya mwaka huu Makumbusho Pemba imetengewa asilimia ngapi ya bajeti yote ya Makumbusho? Lakini Mhe. Mwenyekiti, na jawabu hiyo sikuipata namuomba Mhe. Waziri anisaidie.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na naomba nimjibu Mhe. Salma Mohammed, kwamba ni kweli Unguja asilimia 94 ni mishahara 74 ni *other charges*. Fungu hili limekuwa kubwa kwa sababu baada ya kupata mtafaruku wa kuanguka kwa jengo la Beit el Ajaaib, ikabidi ahakikishe tunapata fedha za kuhama pale, kwa hiyo hali ilikuwa mbaya, watu wamezuiwa kupita, hatuna uhakika wa hali halisi itakavyokuwa, kwa hiyo ikabidi tukahangaikahangaika kuhami pale, kwa hiyo naomba aelewe hilo, kwa sababu tulikuwa na tatizo kubwa limetokea ikabidi tuchukue pesa ndio hizi za Unguja zikawa nyingi ni kwa sababu ya janga ambalo tulipata kubwa ambalo lazima ilibidi tulihami.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu suali lake la pili naomba radhi kwanza kwamba sikumjibu, kwamba mara hii tumepanga bajeti ya maendeleo ya 230,000,000/=; katika hizo Unguja tutatumia 125,000,000/= na Pemba tutatumia 105,000,000/= kwa hivyo ukipiga mahesabu ya chapu chapu hapo kiasilimia utakuta kama ni asilimia 40. Sasa *proportional* nadhani itakuwa Pemba tumeifanyia haki zaidi, kwa hivyo ajue kwamba yale makosa yaliyotokezea mwaka jana basi kibajeti tumeyarekebisha.

Mhe. Salma Mohammed Ali: Mhe. Mwenyekiti, bado ninaomba ufafanuzi zaidi kwa Mhe. Waziri, hizi pesa za *Other Charges* hazina utaratibu maalum hata zikachukuliwa za Pemba zikaongezewa Unguja za Unguja zikapelekwa Pemba, ninamuomba Mhe. Waziri, anifahamishe.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, kuna utaratibu mzuri sana uliowekwa na Wizara ya Nchi Fedha,

inayohusiana na *allocation* ya bajeti baina ya Pemba na Unguja, na haiwezekani kuna utaratibu pale unaoitwa *Intergrated Financial Management System* ambao ndio unaingiza mafungu ya fedha katika taasisi mbali mbali. Kwa hiyo haiwezekani kwamba fedha ambazo zimewekwa kwa Pemba zirudi Unguja. Sasa kilichofanywa ni kwamba hili la Unguja tulihangaika kupata pesa ili kulitunisha kwa sababu ya janga tulilolipata, kwa hiyo haikuchuliwa Pemba ikaletwa Unguja abadan, kwa sababu taratibu za kihazina hazikubali na mwenyewe mkali sana katika mambo hayo Mhe. Waziri.

Mhe. Salma Mohammed Ali: Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli Makumbusho Mhe. Mwenyekiti, ni muhimu kwa sababu pia ni kivutio cha watalii. Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa sina nia ya kumzonga Mhe. Waziri, ingawa sikuridhika sana lakini naomba tuendelee.

Kifungu 1102 Idara ya Makumbusho na Mambo ya kale 70,000,000/=
Kifungu 1101

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Nilipokuwa nikichangia katika habari ya michezo na utamaduni, nilizungumza kama kuna michezo mingi imekufa siku hizi; ikiwemo mchezo wa ng'ombe, mchezo wa kuogelea, mashindano ya ngalawa na madau na ule mchezo wa bao la kete. Na nikatoa mfano kama zamani kulikuwa na mzee mmoja Kichanjani kule akiitwa mzee Kahatan, wale walikuwa wakitoka Kojani wakija Kichanjani wakija kucheza bao tu la kete na tukisikia katika redio. Lakini Mhe. Waziri, aliposimama hapa kujibu hakunijibu hapa, nilipochangia mimi akanijibu mwaka kogwa wa Kojani, nimechangia hapa Mheshimiwa naomba unijibu, unijibu katika sehemu hii ni lini michezo hii itarejeshwa katika kujenga afya na ajira?

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba Mhe. Hassan Hamad, alipokuwa akilizungumza suala hili alizungumzia kuhusu kuimarisha michezo ya jadi ambayo ina mnasaba sana na Jimbo la Kojani. Jimbo la Kojani Mhe. Mwenyekiti, ni eneo ambalo lina utamaduni mwingi. Sasa mimi nilipomjibu ni kwamba mambo haya yana chanzo chake. Nilipokuwa naenda katika mwaka maeneo ya Kojani na Tumbe, shughuli hizi za michezo mbali mbali inashindanishwa na wananchi kabla ya kufika siku ya mwaka, kwa miezi ya nyuma walikuwa wanafanya *reharsal* ya mashindano mbali mbali ili kuweza kushiriki. Sasa ilipobuniwa kuadhimisha mwaka Tumbe na Kojani ile *spirit* ya kufanya mazoezi kwa ajili ya mashindano imepotea ndio ukweli wenyewe. Sasa mimi nikamwambia kwamba Mhe. Naibu Waziri hapa ndio mwenye *desk* hilo, tushirikiane baina yake na Mhe. Naibu Waziri hapa tuangalie

namna gani tutafanya mbinu, na sisi Wizarani tutasaidia kuhakikisha kupitia Kamisheni ya Utamaduni na Michezo tuimarishe vuguvugu la mwaka wa Kojani, kwa kufanya hivyo yale ambayo yalikuwa yakifanyika mwanzo zile shughuli mbali mbali za michezo zingeliweza kuibuka zaidi. Kwa hiyo hilo tu ndio jambo ambalo litaweza na bado nasimamia kauli yangu, lakini kama ana hoja nyengine zaidi ya hiyo niko tayari Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mhe. Mwenyekiti, nimemfahamu sana Mhe. Waziri, lakini nataka ajikite kadri ilivyo, kwa sababu Mwaka Kogwa wa Kojani ni mwaka ulikuwa mashuhuri sana lakini tarehe hizi kutokana na wenzetu kusoma elimu ya dini ya kiislamu umepigwa vita kiasi, sasa kuna maadhimisho tu ya wazee kufika ile siku. Mimi niko katika mambo ya kuogelea na bao la kete, mchezo wa ng'ombe, hata Muasisi wa Nchi hii Marehemu Mhe. Abeid Amani Karume alikufa kwenye mchezo wa bao, sasa ninamuuliza Mhe. Waziri, ni lini atairejesha michezo hii, ukija kunipa jawabu yako sina matatizo tutaendelea.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba tushirikiane na Mhe. Mwakilishi nikimaliza tu Baraza baada ya sikukuu ya sita yeye ndiye anayesherehekea zaidi kuliko hii ya mwanzo, basi niko tayari kushirikiana mimi na Naibu Waziri hapa, tukutane pamoja tuandae mikakati gani ya kurudisha vuguvugu la michezo hii hasa ya ng'ombe. Pale Chwale ni kweli ilikuwa ni kitovu chake, kwa hivyo tukitafute kiwanja kimoja pale, tutasaidiana kukijenga sisi na yeye kiwe ndio kituo cha mchezo wa ng'ombe, tutafute makabili, atajua yeye makabili wapi tutapata, tujenge mabigili anajua namna ya kujenga mabigili yeye, basi tafuta ng'ombe wale kipole wa siku hizi aliosema Mhe. Mohammed Masoud kipole hawapo tena, lakini atatafuta kipole wengine, basi tutakwenda kufanya mchezo wa ng'ombe na michezo mingine hatuna wasi wasi na hilo.

Mhe. Hassan Hassan Omar: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru sana jibu alilonipa Mhe. Waziri, sasa hivi nimeridhika, baada ya kumaliza mwezi wa mfungo wa Ramadhan tutafanya hiyo kazi.

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, wakati nikichangia sekta ya michezo nilizungumzia suala zima la *FIFA Goal Project.* Mhe. Mwenyekiti, mbali na majibu ya Mhe. Waziri, lakini fedha zile *FIFA* huwa inatoa kwa ajili ya Tanzania nzima, yaani Tanzania Bara na Zanzibar ndio inaunda Tanzania. Mhe. Mwenyekiti, na hata katika masuala haya kutoa fedha zile wenzetu nilisema kwamba wamefanya miradi minne, tumepata mradi mmoja ambao ule wa Gombani, na nikamwambia kwamba ipo haja ya kulifanyia kazi suala hili ili na sisi Zanzibar tuweze kufaidika na mradi ule.

Mhe. Mwenyekiti, wenzetu wamejenga ofisi nzuri ya kisasa kwa ajili ya mradi ule wa *FIFA Goal Project,* lakini wenzetu au Chama chetu cha Mpira wa Miguu Zanzibar *ZFA* hakina ofisi na inapanga leo pale kesho pale. Kwa hivyo kwa kutumia fedha hizi za *FIFA Goal Project* ipo haja ya kukaa na *TFF* ili na wao *ZFA* wapate ofisi angalau watulie na wapumue. Ahsante.

Mhe.Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, nikishukuru na najua mazingatio ya Mhe. Jazira katika suala hili. Kama nilivyosema katika jibu langu kwamba mimi nimelifuatilia suala hili kwa upana sana na tukakutana ofisini hapa Zanzibar *VIP* ya Amani mimi pamoja na Rais wa *TFF* na Mwakilishi wa *FIFA* kanda ya Afrika tulizungumzia kwa upana suala hili, lakini bado jibu lao ni kwamba *Zanzibar is not an Independent State,* na kwa hivyo misaada ya *FIFA* kwa Zanzibar moja kwa moja haiwezekani mpaka tupitie mgongo wa *TFF*. *TFF* wana *priority* zao nyingi, wana viwanja vyao vingi, kwa hiyo tulibahatika kupata kile cha Gombani nikawaomba watusaidie wakati huo tunatafuta angalau kile cha Amani tulifanya mkutano kusudi pale baada ya kwenda kuwatembeza pale Kiwanja cha Amani, lakini bado wakanambia Mheshimiwa tunasikitika bajeti yetu mara hii haiwezekani, kwa hivyo zungumzeni na *TFF* katika suala hili.

Kwa hviyo, Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Mjumbe aelewe kwamba tunachukua hatua; hivi sasa vijana wangu wa *ZFA* wako Dar es Salaam kuzungumza na *TFF* kuhusu masuala hayo angalau kuangalia tutapata kitu gani katika suala hili. Kwa hivyo, bado hatukulikalia tunalisimamia kama alivyosema Mhe. Waziri wa Kazi lazima tulisimamie.

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante Mhe.Mwenyekiti, mbali na maelezo ya Mhe. Waziri, lakini nadhani ipo haja Mhe. Mwenyekiti, kupitia kamati yako ya kudumu ambayo inashughulikia masuala haya ya michezo pamoja na yeye na mimi tufanye safari twende kukutana na *TFF* tukiambatana na *ZFA* ili kusuluhisha suala hili.

Mhe. Mwenyekiti, tatizo hili ni kubwa bila ya kulifanyia kazi nadhani pesa zile sisi hatutafaidika. Mheshimiwa baada ya kusema hayo nakushukuru tuendelee.

Kifungu 1201 Kamisheni ya Utamaduni na Michezo 1,312,204,000/-
Kifungu 1202 Baraza la Kiswahili 95,000,000/-
Kifungu 1203 Mchango wa *Eacrotanal*

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia katika sehemu hii niliona kwamba kuna wale *member states*

ambao walikuwa wanachangia Jumuiya hii sasa wamesha-*collapse*. Kwa hivyo, nilikuwa namuomba Waziri kwa sababu nilikuwa sijafahamu vizuri anieleze vizuri. Na kwa bahati mbaya tu hakupata kunijibu suala langu nililomuuliza hapa. Hivyo nilitaka Mhe. Waziri anieleze kwa kina kwa nini Jumuiya hii inataka kuhaulishwa na kupelekwa katika Jumuiya ya Afrika ya Mashariki, na kwa sababu ile kwanza ilikuwa ni hadhi kwa Zanzibar kupewa kituo kile. Kwa nini sasa hivi kihaulishwe na kupelekwa Afrika ya Mashariki?

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba Mhe. Fatma mbarouk alichangia kwa maandishi suala hili, na nadhani nilipokuwa namjibu Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi Mheshimiwa na yeye nilimtaja, nilidhani naye kwamba aliridhika na majibu yenyewe, kwa hivyo hakuridhika namuomba radhi. La msingi ni kwamba kituo kile kilianzishwa miaka mingi na tangu kianzishwe wanachama wake hawashughuliki nacho, nchi zote zile ambazo zilikuwa wanachama tulikubaliana tuanzishe wakawa hawatoi michango, hawahudhurii mikutano, kwa hivyo kukabakiwa na *Eacrotanal* jina lakini hakuna *activities* yoyote ya *Eacrotanal* ambayo ilikuwa inafanya kazi.

Kwa hivyo, miaka mingi sisi tukawa tunalea jengo, tuna jengo tunalilea lakini hakuna tunachokiona, sasa tunaona hakuna sababu ya kuendelea kulea jina wakati mwenye jina hayupo tena amefariki. Kwa hivyo, la kufanya kwa sababu tumeanzisha ile Jumuiya ya Kiswahili ya Afrika Mashariki, na sisi Zanzibar ndio tumekubaliwa kuwa wenyeji wa kituo hicho tukaona badala ya majengo yale yamekaa tu pale kwa jina la *Eacrotanal* tubadilishe matumizi sasa yawe Kituo cha Jumuiya ya Kiswahili Afrika Mashariki.

Kwa hivyo, tumefanya hivyo kwa sababu kituo chenyewe kimsingi hakipo, wanachama wenyewe wameingia mitini, tunakuwa sisi tuna majengo ambayo tume-*brand Eacrotanal*.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Mhe. Mwenyekiti, kwa majibu mazuri ya Mhe. Waziri sasa kwa kuwa kituo hiki kinapelekwa katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Je, kutakuwa na masharti yoyote ambayo watawekewa na vile vile je, serikali itapata faida gani?

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwamba masharti yoyote kwanza kuna mkataba ambao ndio tunakubaliana nimesema humu, kuna *headquarters agreement* ambayo tunajadiliana baina ya sisi Makao Makuu ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Lakini kuna fursa ambazo pia zinapatikana, lakini la kwanza tutapata nafasi ya vijana wetu wengi kufanya kazi pale kama nchi mwenyeji,

kama ambavyo katika nchi nyengine ofisi za Jumuiya ya Afrika Mashariki zinakuwa wanapata fursa ya watu wao kufanya kazi. Lakini kubwa ambalo tunalipata sisi tunajinasibu, na ndio ilivyo kama ndio wazawa wa Kiswahili katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kwa hivyo, tutapata nafasi pana zaidi ya kukiendeleza Kiswahili chetu katika nchi nyengine za Afrika Mashariki, na hilo kwetu sisi ni jambo kubwa.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, namshukuru Mhe. Waziri kwa kunipa majibu hayo mazuri na nasema tuendelee.

Kifungu 1203 Mchango wa *Eacrotanal* 21,000,000/-
Kifungu 1204 Baraza la Michezo la Taifa

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kabla sijaingia hapo naomba kidogo Mheshimiwa nikariri maelezo ya Mhe. Waziri kwenye kitabu chake katika hilo Baraza la Taifa la Michezo kifungu cha tatu chini, "Kuimarisha vyama vya michezo katika ngazi zote kwa kuvipatia vifaa vya michezo".

Mhe. Mwenyekiti, nilipochangia ukurasa wa 54 kwenye Baraza lake la Michezo hili nilichangia suala la riadha. Katika suala la riadha kulikuwa na masuala mawili hapo, suala la kwanza kuhusu habari ya uchaguzi nilitaka Mhe. Waziri anitamkie ni lini tutaweza kufanya uchaguzi kwa nia nzuri tu, kwa kuwa rasimu tushapitisha tayari mpya.

Lakini suala la pili hapo hapo nilisema suala la fedha ambazo walizitoa Mhe. Rais Mstaafu, Amani Abeid Karume sikupata jibu kwa hizo fedha, na hiki ni kipindi cha pili tuangalie *hansard*, ninazisema zile fedha ambazo hawa vijana wetu wanavyojitahidi Mhe. Mwenyekiti, katika kutuletea jina zuri na sifa kwa Zanzibar, lakini leo wanapopata fedha zile za kutunzwa ili ziwaendeshee katika mambo ya kuendelea na shughuli zao nzuri hatimaye Mheshimiwa zinafikia kwenye mifuko mingine.

Sasa ningemuomba Mhe. Waziri anieleze fedha zile kazichukua nani? Na fedha zile ziko wapi na lini zitapatikana ili kurejesha kwenye mfuko wao wenyewe wanariadha wetu ili tufikishwe pahala pazuri. Mhe Mwenyekiti, nasubiri jibu zuri nimwachie kifungu chake.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli Mhe. Mwanariadha maarufu Mhe. Makame Mshimba alizungumza hilo suala. Sasa majibu yake ni kwamba lini uchaguzi wa Chama cha Riadha utafanyika hili ni jukumu la chama chenyewe sisi wizara hatuna

mamlaka ya kuwaambia fanyeni kesho au keshokutwa. Kwetu sisi kuna Mrajis wa vyama vya michezo, ikiwa chama tutakiona kwa muda mrefu hakijafanya uchaguzi tutamwambia atakifuta tu, kwa hivyo ni juu yao wenyewe wakae na chama chao siku yoyote wakitaka kufanya uchaguzi watuarifu Mrajis aende akaone kwamba huu uchaguzi uko salama na hauna matatizo si tatizo, laa wanataka pesa kidogo kusaidiwa basi walete maombi tutaangalia mfuko wetu kama upo hakuna tatizo Mheshimiwa.

La pili suala la fedha ambazo zilikabidhiwa kwa ahadi aliyotoa Mhe. Dr. Karume. Naambiwa kwamba shughuli hii ilikuwa mwaka 2006. Maelezo niliyopewa na watendaji wangu ni kwamba siku hiyo ya tukio basi viongozi waliokuwepo wa Chama cha Riadha walikabidhiwa shilingi zao milioni moja, kwa sababu zote zilikuwa zao, kwa hivyo ziligaiwa na wao wakapata *share* yao. Sasa walivyozitumia kama wamezigawa, kama wamezifanyia kazi basi ni juu yao na viongozi wenyewe wa vyama vyao.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru sana kwa maelezo ya Mhe. Waziri, lakini vile vile nimshukuru sana na Katibu wa Baraza, nafikiri atakuwa kama yupo keshajua utaratibu wa kuweza kuhimiza lini uchaguzi ufanyike. Lakini Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri kawa muwazi ameeleza ukweli, kwa maana hiyo uwazi wake unatudhihirishia kuwa kuna viongozi wao kazi yao kuchukua fedha za wavuja jasho ndio maana yake katika michezo kama hiyo. Hiyo ndo maana ya maelezo yake Mhe. Waziri ili tukitaka tusitake tukubaliane nalo. Nimuunge mkono kwa kauli hiyo kukubali kama viongozi walikabidhiwa fedha na Rais halafu wao hawakuzifikisha kwa walengwa walizitia mfukoni na wakazila, Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli inasikitisha na naomba sana hao watu wachukuliwe hatua mara moja ipasavyo kwa mujibu wa sheria ili waweze kufikishwa katika vyombo vya sheria na kurudisha pesa hizo. Mhe. Mwenyekiti, naomba tuendelee kwa hilo.

Kifungu 1204 Baraza la Michezo la Taifa 147,000,000/-
Kifungu 1205

Mhe. Shadya Mohamed Suleiman: Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipompelekea Mhe. Waziri mchango wangu kwa maandishi nilitaka kujua kuhusiana na suala zima la jengo la studio lilioko Rahaleo. Mhe. Mwenyekiti, jengo hili siku za nyuma lilikuwa likikodishwa kwa shughuli za maharusi, sasa nilikuwa nataka nijue ni kiasi gani cha mapato kilichopatikana.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, sijui kama nimemsikia vizuri, lakini mchango wake alionileta leo asubuhi ni kwamba ukumbi ule utatumikaje vizuri zaidi na kwamba

ulikuwa umekusudiwa kutumika katika kushughulikia vijana wetu kurekodi sanaa zao. Sasa je, ndivyo ulivyotumika au sivyo? Ndivyo nilivyofahamu. Sasa kama ni hivyo ni kwamba baada ya ujenzi wa ukumbi ule kama amefuatilia vizuri kitabu hiki ni kwamba mwaka huu tumetenga fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa mbali mbali vya kurekodia sanaa. Kwa hivyo, tukipata fedha hizo ndivyo ambapo ukumbi huo utakuwa utatumika vizuri sana, na ndio lengo kwamba vijana wetu kuja kurikodi pale sanaa zao mbali mbali.

Sasa wakati huu ambapo shughuli hiyo haijaanza tulianza shughuli ndogo ndogo pale Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wakanishauri kwamba zisitumike. Kwa hivyo tukashauriana na wenzangu tukawaaambia hapana tutumie, sasa tutafanya shughuli pale katika ukumbi mkubwa labda wa mikutano ya kiwizara, semina za wizara, lakini sio shughuli za rusha roho na maulidi, mambo hayo tumeshauriwa na Wajumbe wa Baraza na tumekubaliana kwamba tufanye.

Kwa hivyo, saa hizi shughuli ndogo ndogo zinazofanyika ni hizo tukisubiri ununuzi wa vifaa ambavyo tumevibajeti tukipewa tu pesa tutanunua ili vijana wetu waweze kutumia kama vile ambavyo Mhe. Rais wa Zanzibar aliwaahidi vijana hawa wa muziki.

Mhe. Shadya Mohamed Suleiman: Mhe. Mwenyekiti, mchango wangu kusema kweli kwa Mhe. Waziri ulikuwa ni maswali na yalikuwa ni maswali mawili. Moja ni hilo nililomuuliza kuhusiana na mapato ya ukumbi huo, na jengine lilikuwa ni hilo kuhusu watu wa sanaa wanaorekodi. Kwa hivyo, tuendelee.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi tena na hapa wala sitaki nimzonge Mhe. Waziri wangu nataka nimsaidie ushauri tu. Katika mchango wangu nilizungumza kero ambayo imeshatuchosha, na yeye kaithibitisha kwamba ishamkera sana na nashukuru katika majibu yake kalizungumza suala la kupigwa mziki katika kumbi zilizo wazi, na kwa Mji Mkongwe nilitaja kuhusu usia katika Ngomekongwe na katika eneo la Bwawani. Haidhuru nimwambie pia hivi sasa apite maeneo ya pale tulipozowea sisi kupaita Ras Shangani, kuna mkahawa mmoja pale unaitwa moja, mbili, tatu; pale pamefunguliwa mkahawa lakini ukipita saa za mapema kama saa nne, tano mpaka sita nyumba ambayo ina varanda tu kunapigwa muziki kageuza mkahawa, kwa hivyo kuna matatizo.

Sasa alipokuwa akinijibu hoja hii kasema kwamba kuna tatizo la kisheria, haidhuru kuna hatua za kiutawala ambazo alizichukua na mimi nathibitisha,

na kwamba alitembelea akatoa maagizo, na maagizo yake kwa muda mrefu yalisimama. Lakini Mheshimiwa tulifika pahala ikawa kila jambo mpaka aingie Waziri tu itakuwa kazi kubwa sana, hawa tuliowapitishia bajeti wanafanya kazi gani? Baraza la Sanaa. Sasa hili nataka nimwachie aendelee kulifanyia kazi na watu wake ili nisije nikalisahau kwa mara ya sita katika Baraza hili. Lakini nataka kumsaidia katika sheria tu ndio maana nimenyanyuka. Alisema kwamba kuna tatizo la kisheria nataka kumkumbusha tu kwamba tumepitisha hapa sheria ya *Public Health Act* Mhe. Mwenyekiti na wewe shahidi. Sheria ile nilisimamia hapa na tukairekebisha na Mhe. Mwanasheria Mkuu katika marekebisho tuliyoongezea Baraza la Wawakilishi kuongeza kifungu kinachohusu upigaji wa muziki katika maeneo kama hayo, na ghasia katika maeneo mbali mbali na tukakubaliana kwamba inajumuisha katika sehemu ya bughudha kwa watu.

Kwa hivyo, nilikuwa namuomba tu kwamba wakati ule sheria tunasema ifanyiwe marekebisho, kwa sasa hivi sheria ya *Public Health Act* katika suala la uchafuzi wa mazingira katika kutumia miziki yenye ghasia tayari sheria ile imepitishwa, imeshasainiwa kwa hivyo atumie sheria ile na Baraza lake la Sanaa.

Na niwaombe Baraza la Sanaa kupitia kwake wasingoje Waziri tu watamuangusha Waziri wetu, wafanye kazi yao tuliyowaajiria na tunawapitishia vifungu vya matumizi hapa.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Mwenyekiti, nataka uhakikisho huo wa Mhe. Waziri kwamba atasimamia Baraza lake lifanye kazi hii sasa isiwe kila kitu yeye, lakini pili aitumie sheria hii ya *Public Health Act* kutekeleza hili ili wananchi wangu wa Mji Mkongwe wapate raha kama wanavyopata wananchi wa maeneo mengine wakiwemo wa Gando Mheshimiwa ahsante.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Kwa kuwa Mhe. Jussa yeye ni Mwanasheria bahati nzuri, kwa hivyo namshukuru kwa kunikumbusha kuhusu hii sheria ya *Public Health Act*, hivyo tutairejea na tutaitumia na nitazidi kuwasimamia watu wangu wa Bodi ya Sanaa kuhakikisha kwamba tunasimamia vizuri shughuli hizi za upigaji wa muziki katika jamii.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nachangia hapa nilisema suala la nyumba, sasa pengine Mhe. Waziri amesahau kunijibu suala hili kuhusu habari ya nyumba ile ya sanaa pale haiko katika hali nzuri kwa kweli haileti taswira nzuri. Sasa naomba kidogo anisaidie Mhe. Waziri katika kunisahau kwake kulikuwa na lengo la kuwa

binadamu kapitikiwa au ndio kanisahau tu kuwa nisije nikampiga buti. Mhe. Mwenyekiti, naomba ufafanuzi.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, inaonekana leo swahibu wangu daku imempita kidogo, suala hili nililijibu kwa hivyo labda alikuwa kidogo swaumu ishaanza kumchukua. Nilisema kwamba, wizara katika mwaka unaomalizika imefanya matengenezo makubwa ya awamu ya kwanza, paa lote lilikuwa linavuja tumeliezua na tumeliezeka. Kwa hivyo, hatua inayoendelea sasa ni ya matengenezo mengine madogo madogo. Juzi nilikuwa na Balozi Mdogo wa Japan tukalizungumzia suala hili ili kuifanya kuwa bora zaidi na kulimaliza lile paa, lakini kimsingi hapo ilo hatujafika pahali lakini hili la kutumia bajeti yetu na mwaka huu pia tumetenga fedha kwa ajili ya matengenezo ya nyumba hiyo.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, nimshukuru Mhe. Waziri kwa ufafanuzi huo, kweli ameeleza suala la paa lakini nilitaka kujua je paa ndio iwe paa tu huku chini katungenezwi. Sasa namshukuru sana Mhe. Waziri amesema kuwa na huko chini wataendelea kutengeneza kwa mujibu wa bajeti ambayo hii tunayokwenda nayo.

Lakini Mheshimiwa suala hili hili kulikuwa na msanii hapa japo alinijibu kwamba watamuweka kwenye kumbukumbu, lakini je, Mhe. Waziri inatosha tu kuwa mtu huyu tumuweke kwenye kumbukumbu hivi hivi tu bila ya jambo jengine lolote, kumtafutia kitu ambacho maisha yake asisahau na yeye kama alivyotuwekea sisi hizi nembo zetu. Naomba hapo akishanijibu hapo jibu zuri naomba tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Hebu hilo suala mfuate ofisini utajua namna yake, umetaka kuhusu matengenezo ya jengo tuendelee.

Kifungu 1205 Baraza la Sanaa na Muziki	42,000,000/-
Kifungu 1206 Bodi ya Sensa na Sinema	38,000,000.-
Kifungu 1207 Kamisheni ya Utamaduni na Michezo	

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia kuhusu utamaduni nilisema utamaduni wa Mzanzibari unaendelea kutoweka siku hadi siku, kwa sababu inaonekana sasa utamaduni wetu tunaiga tamaduni za nje, kwa sababu tuna vijana wetu sasa hivi wanaume wanasuka nywele, wanavaa herini na utamaduni huo haukuwa wa kwetu. Nikamuomba sana Mhe. Waziri aangalie vyema sheria za nchi ili zinaeleza nini katika utamaduni wetu huu, kama zina mapungufu basi tuweze kuzirekebisha ili utamaduni wa Mzanzibari uendelee kudumu na kuja

kurithisha vizazi vyetu. Hili Mheshimiwa sikupata kulisikia kwa hivyo nilikuwa naomba Mhe. Waziri anielezee, na hasa ukizingatia tukikosa utamaduni wetu tutakuwa ni masikini hali tutakuwa tumeutupa utamaduni wetu na hatatukuwa na cha kuwarithisha watoto na wajukuu. Naomba ufafanuzi Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli Mhe. Mjumbe alizungumzia suala hili, lakini kimsingi Mheshimiwa suala hili lazima tushirikiane baina ya serikali na wazazi. Masuala ya malezi ya watoto majumbani yatasaidia zaidi kuliko sheria au jambo jengine. Kwa hivyo, niwaombe sana wazazi wenzangu wa Zanzibar tujaribu kuwalea watoto wetu kwa silka na utamaduni wetu, hilo ndio jambo pekee litakalotusaidia.

Sasa kama ushauri wake wa kuliangalia kisheria tumeuchukua lakini kimsingi hili ambalo nimelizungumza la kwamba tujitahidi kuwalea watoto wetu vizuri, mtu ana mtoto wake ndani anamuacha anasuka nywele mwanamme mzima anamtizama anasubiri Waziri wa Habari lugha hiyo itakuwa ngumu sana, yaani anamuacha mtoto wake mwanamke anavaa vitopu anamuacha anasubiri Waziri wa Habari. Nadhani kwamba suala la malezi ndani ya jamii na ndani ya wazazi tushirikiane ili kuona kwamba tunawalea watoto wetu katika maadili mema, lakini ushauri wake wa kisheria nitauchukua Mheshimiwa.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na nimshukuru Mhe. Waziri kwa kuona hilo. Lakini mimi bado nataka niseme serikali ina mkono wake, sisi wazazi tutajitahidi kwa upande wetu lakini na serikali ina mkono wake. Tuchukue mfano wa uhai wa Marehemu Abeid Amani Karume, hii ilikuwa vijana wakifuga nywele kubwa, wakivaa vishati vya kubana na masuruali yale yaliyokuwa yakiitwa buga au chupa. Lakini serikali ilipoamua kwamba sasa vazi hili hatulitaki ilichukua hatua na tukaweza kuona kweli vazi lile liliondoka wanawake waliokuwa wakivaa *tight* ikawa tunashona meksi tumevaa.

Sasa hili pamoja na wazazi kweli serikali tushirikiane lakini na watoto wetu wa miaka hii wamekuwa watoto wa kisayansi, inawezakana kavaa kisuruali chake lakini akajitia buibui wewe mzazi pale pengine hukumuona mpaka akifika huko mbele. Lakini sasa akifika huko mbele yuko mlezi mwengine anamsubiri.

Kwa hivyo, mimi Mheshimiwa naomba na serikali iliangalie, kwa sababu wewe mzazi pengine ushajitahidi kumwambia nyumbani lakini kaondoka pale

kajigubika wewe hukumuona, lakini akifika mbele huko anakwenda kujizongoa anabaki na kisuruali chake. Sasa hili wewe mzazi utapomwambia na kule akifika kuna mtu wa kumwambia nadhani tutaweza kufanikiwa. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Kifungu 1207 Kamisheni ya Utamaduni na Michezo Pemba	50,000,000/-
Jumla ya Fungu	**8,357,000,000/-**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 31 – KAMISHENI YA UTALII

Kifungu 0201 Utawala Unguja	100,000,000/-
Jumla ya Fungu	**100,000,000/-**

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)

FUNGU 42 – WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, UTALII NA MICHEZO

Kifungu 0301 Afisi Kuu Pemba	100,000,000/-
Kifungu 1101 Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale Unguja	230,000,000/-
Kifungu 1201 Kamisheni ya Utamaduni na Michezo	80,000,000/-
Jumla ya Fungu	**410,000,000/-**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha Makadirio ya Fedha ya Wizara yangu bila ya mabadiliko, sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza liyakubali makadirio hayo.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Sasa niwahoji Waheshimiwa Wajumbe wanaokubaliana na Makadirio hayo wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2013/214 – Wizara ya Mifugo na Uvuvi

Mhe. Spika. Waheshimiwa kikao kinaendelea maana naona kama mtaniacha peke yangu. Mhe. Waziri sasa endelea.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu, likae kupokea, kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2013/2014.

Mhe. Spika**,** kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kutujaalia afya njema na kutuwezesha kukutana tukiwa katika hali ya amani na utulivu katika nchi yetu. Kwa niaba ya wafanyakazi wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dk. Ali Mohamed Shein kwa kuendelea kuiongoza nchi yetu kwa hekima na busara kubwa.

Pia napenda kuwapongeza Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais, Maalim Seif Sharif Hamad na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, Balozi Seif Ali Iddi kwa busara na hekima zao katika kumsaidia na kumshauri Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika kazi zake za kila siku.

Kwa hakika kitendo cha viongozi wetu cha ufuatiliaji wao wa karibu wa kazi tunazozifanya na ushauri wao kwetu, umetuwezesha kupata mafanikio makubwa katika utendaji wa majukumu yetu ya kila siku ya kuwahudumia wadau wote wa sekta za mifugo na uvuvi hususan wafugaji na wavuvi wadogo wadogo ambao kila uchao wanazidi kujiajiri katika sekta hizi. Hali hii sio tu inawapatia kipato bali pia inaongeza changamoto kwetu za kuwawezesha walengwa hawa kupata taaluma na nyenzo muhimu za kuzalisha kwa tija.

Mhe. Spika, napenda kuchukua fursa hii kukupongeza wewe binafsi kwa kuendelea kuliongoza Baraza letu la Wawakilishi kwa hekima, busara na

juhudi za hali ya juu, hali inayopelekea Baraza letu kufanya kazi zake kwa ufanisi mkubwa. Pia napenda kuwapongeza wasaidizi wako, wakiwemo Mhe. Naibu Spika, Waheshimiwa Wenyeviti wa Baraza hili, Katibu wa Baraza na Maafisa wa Baraza wanaokusaidia katika kutekeleza majukumu yako.

Mhe. Spika**,** napenda kunatoa shukrani zangu za dhati na kuipongeza Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari ya Baraza la Wawakilishi iliyomaliza muda wake hivi karibuni, kwa kutushauri kwa busara na hekima kubwa katika kufuatilia utekelezaji wa kazi za Wizara yetu ili kuweza kufikia kiwango cha juu cha maendeleo. Napenda kutoa shukrani za pekee kwa Mwenyekiti wa kamati hiyo, Mheshimiwa Bi. Asha Bakari Makame kwa umahiri na uzoefu wa kiutendaji alio nao, pamoja na wajumbe wa Kamati yake ambao umeisaidia sana Wizara yetu katika kufanikisha kwa kiwango kikubwa utekelezaji wa malengo yake.

Mhe. Spika**,** utayarishaji wa mpangokazi na bajeti ya Wizara yetu umepitia ngazi mbali mbali kwa kupata ridhaa, ikiwemo Kamati ya Uongozi ya Wizara na Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari. Naomba kuishukuru sana Kamati hii mpya chini ya Mwenyekiti wake, Mhe. Mlinde Mabrouk Juma, Mwakilishi wa Jimbo la Bumbwini, kwa kuichambua bajeti yetu kwa makini, kuihoji na hatimae kuiridhia iwasilishwe mbele ya Baraza lako tukufu. Tuna uhakika kuwa Kamati hii itaongoza vizuri utekelezaji wa mpango kazi tunaouombea bajeti hii kwa manufaa ya nchi yetu.

Mhe. Spika, naomba kuchukua fursa hii tena kuwashukuru wananchi wa jimbo langu la Magogoni kwa kuendelea kunipa mashirikiano yao makubwa katika kuleta maendeleo ya jimbo letu katika kipindi cha miaka miwili kilichopita. Ni imani yangu kwamba wananchi hao wa jimbo la Magogoni wataendelea kunipa ushirikiano wao katika kuyatafutia ufumbuzi matatizo yanayolikabili jimbo letu sambamba na kutekeleza majukumu yangu ya kitaifa.

Mhe. Spika**,** Mapinduzi katika sekta za mifugo na uvuvi, kama ilivyoelekezwa katika hotuba mbali mbali za Mheshimiwa Rais, ni suala la lazima katika kuongeza uzalishaji na tija kwa wafugaji na wavuvi na hatimae kupunguza umasikini. Matayarisho ya Mpangokazi na bajeti hii ni mwendelezo wa utekelezaji wa Dira 2020, Mpango wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini *MKUZA* II, Ilani ya Uchaguzi na Sera mbali mbali zinazoongoza sekta zetu pamoja na Malengo ya Maendeleo ya Milenia na Mpangokazi wa Wizara yetu katika kuleta mapinduzi ya mifugo na uvuvi.

HALI YA SEKTA ZA MIFUGO NA UVUVI NCHINI

SEKTA YA MIFUGO

Mafanikio katika sekta ya mifugo

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2012/2013 sekta ya mifugo imeweza kupata mafanikio kadhaa. Miongoni mwa mafanikio hayo ni kama yafuatayo:

- Kuimarika kwa utoaji wa huduma za uzalishaji na utabibu wa mifugo;

- Mitambo mipya 11 ya *biogas* imejengwa (Unguja 8 na Pemba 3) kwa njia ya kuchangia gharama. Kujengwa kwa mitambo hiyo kunafanya jumla ya mitambo iliyokwishajengwa Unguja na Pemba kuwa 24;

- Kuongezeka kwa wajasiriamali wa mazao ya mifugo wanaozalisha samli, siagi, jibini, mtindi na maziwa ya kunywa;

- Wizara inaendeleza siku ya unywaji wa maziwa nchini, ambayo huadhimishwa kila ifikapo tarehe 27 Aprili. Madhumuni makubwa ya kuanzishwa kwa siku hiyo ni kuwafanya wananchi kupenda kunywa maziwa na hivyo kuinua soko la ndani, kujenga afya zao pamoja na kunyanyua kiwango cha unywaji maziwa nchini ambacho kwa sasa kiko chini kulinganisha na nchi jirani; na

- Kwa kushirikiana na Tume ya Marekebisho ya Sheria, Wizara imeweza kufanya mapitio ya Sheria ya Rasilimali ya Mifugo (1999).

Mhe. Spika, sekta ya mifugo hivi sasa imeweza kutoa ajira kwa kaya 34,000 na kukua kwa asilimia 3.1 na kuchangia asilimia 3.8 ya pato la Taifa mwaka 2012.

Changamoto katika sekta ya mifugo

Mhe. Spika, licha ya hatua zilizofikiwa katika sekta ya mifugo, sekta hii bado inakabiliwa na changamoto mbali mbali zikiwemo:-

- Upungufu wa wataalamu mbali mbali wa sekta ya mifugo;

- Upungufu wa nyenzo za kufanyia kazi kama vile vyombo vya usafiri kwa watoa huduma za ugani;

- Ukosefu wa mitaji kwa wajasiriamali wa mazao ya mifugo;

- Maradhi ya mifugo na upungufu wa vifaa vya kudhibiti maradhi hayo;

- Uchakavu wa miundombinu ya kuendeleza uzalishaji wa mifugo ikiwemo vituo vya uzalishaji na utabibu wa mifugo (*Animal Health and Production Centres*) na majosho;

- Uhaba wa malisho hasa wakati wa kiangazi na uchache wa maeneo ya malisho; na

- Bajeti ndogo ya sekta ya mifugo.

Mtazamo wa baadae katika sekta ya mifugo

Mhe. Spika, katika jitihada za kuimarisha sekta ya mifugo nchini, mtazamo wa Wizara ni kama ufuatao: -

- Kuimarisha huduma za ugani ili ziwafikie walengwa wengi zaidi katika sekta ya mifugo;

- Kuongeza uwezo wa kitaaluma kwa wafanyakazi na kuajiri wataalamu zaidi ili kuongeza ufanisi wa utoaji huduma;

- Kuongeza ajira kwa vijana kupitia shughuli za uzalishaji mifugo;

- Kuendelea kuhamasisha na kupandisha ng'ombe kwa njia ya sindano ili kuongeza ubora wa ngombe wa maziwa na nyama;

- Kuimarisha utafiti katika sekta ya mifugo;

- Kukuza huduma za utabibu na uzalishaji wa mifugo;

- Kufanya mapitio ya sheria, kanuni, na mipango ya uzalishaji wa mifugo kwa ajili ya manufaa ya wananchi bila ya kuathiri mazingira;

- Kuimarisha miundombinu ya kuendeleza uzalishaji wa mifugo ikiwemo vituo vya uzalishaji na utabibu wa mifugo, majosho na maeneo mapya ya karantini;

- Kuimarisha ushirikiano kitaifa, kikanda na kimataifa katika nyanja mbali mbali za kuendeleza sekta za mifugo; na

- Kuwaunganisha vijana wajasiriamali na taasisi mbali mbali ikiwemo Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika ili kuweza kupata mtaji na kujiajiri wenyewe.

SEKTA YA UVUVI

Mafanikio katika sekta ya uvuvi

Mhe. Spika, sekta ya uvuvi imezidi kuimarika kutokana na kuongezeka kwa uvuvi wa baharini na pia wananchi wengi wameanza kufuga samaki na mazao mengine ya baharini. Hivi sasa wananchi wengi wameshajiika na wameanza kufuga mazao ya baharini kwenye maeneo yao. Mafanikio makubwa yameweza kupatikana hasa katika kisiwa cha Pemba.

Mhe. Spika, Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2012/2013, sekta ya uvuvi imepata mafanikio yafuatayo:

- Kuongezeka kwa idadi ya samaki wanaovuliwa kutoka kilogramu 28,758,997 zenye thamani ya Tshs 85,667,819,035 mwaka 2011 mpaka kilogramu 29,410,554 zenye thamani ya Tshs 103,180,991,590 mwaka 2012 ikiwa ni ongezeko la tani 651 sawa na asilimia 2.3;

- Kuongezeka kwa wingi wa samaki wanaofugwa, ambapo jumla ya tani 9.788 za samaki zimevunwa Unguja na

Pemba (Pemba tani 7.733 na Unguja tani 2.055) kwa mwaka 2012 kutoka kwenye mabwawa ya wananchi. Hali hiyo imeongeza kipato chao na kuchangia kupunguza umaskini;

- Kuongezeka kwa uzalishaji wa mwani kutoka tani 13,040 mwaka 2011 mpaka tani 15,088 mwaka 2012 ikiwa ni ongezeko la asilimia 16;

- Kuwekwa kwa matumbawe ya kienyeji 400 katika baharí ya Marumbi na Chwaka kwa lengo la kuiwezesha baharí kurejesha hali nzuri ya mazingira yake na kuongeza upatikanaji wa samaki;

- Kuongezeka kwa shughuli za ufugaji wa samaki na viumbe vyengine vya baharini kama vile kaa, chaza, majongoo na uhifadhi wa kasa. Hivi sasa kuna vikundi 146 vinavyofuga samaki wa mabwawa na mazao mengine ya baharí nchini (Unguja 61 na Pemba 85) ;

- Kupatikana kwa fursa nyengine kwa kundi la pili la watu 29 wakiwemo wajasiriamali 23 na wafanyakazi 6 kushiriki mafunzo ya muda wa mwezi mmoja ya ufugaji wa mazao ya baharini nchini China;

- Kukamilika kwa ujenzi wa bwawa moja la mfano kama bwawa darasa "*demonstration pond*" katika eneo la Jozani, mkoa wa Kusini Unguja na kukabidhiwa wajasiriamali wa ufugaji wa samaki;

- Kupatikana na kupimwa kwa eneo la ukubwa wa ekari 5 na kuwekewa alama *beacons* huko Mkokotoni, Mkoa wa Kaskazini Unguja kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Mazao ya Baharini. Ujenzi wa kituo hiki unategemewa kufadhiliwa na Serikali ya Jamhuri ya Korea;

- Eneo la ukubwa wa ekari 5 limepatikana, kupimwa na kuwekewa alama *beacons* huko Tumbe Mkoa wa Kaskazini Pemba kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Kusarifu Mwani. Ujenzi wa kituo hiki unaombewa fedha kupitia Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China;

- Kutiwa saini makubakiano ya ushirikiano wa kuendeleza shughuli za utafiti wa uvuvi na ufugaji wa mazao ya baharini baina ya Wizara na Mamlaka ya Utafiti wa Bahari ya China; na

- Majaribio ya upandaji mwani kwa kutumia mawe na mipira *stone and rubber band* yamefanyika katika vijiji vya Kidoti, Fukuchani, Bwejuu na Mtende ambapo jumla ya mbegu 669 za mwani zimepandwa. Majaribio haya yana lengo la kuangalia uwezekano wa kuwapunguzia gharama za vifaa kwa wakulima wa mwani pamoja na kupunguza ukataji wa miti.

Mhe. Spika, shughuli za uvuvi zimekuwa kwa asilimia 2.3 na mchango wa sekta ya uvuvi katika pato la taifa umeongezeka kutoka asilimia 6.7 mwaka 2011 hadi asilimia 7.1 mwaka 2012.

Changamoto za sekta ya uvuvi

Mhe. Spika, pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika kuendeleza sekta ya uvuvi katika mwaka wa fedha 2012/2013, sekta hii imekabiliwa na changamoto mbali mbali zikiwemo: -

- Kuongezeka kwa shindikizo la uvuvi *fishing pressure* katika maeneo ya hifadhi kutokana na kuongezeka kwa idadi ya wavuvi;

- Ukiukwaji mkubwa wa sharia ya uvuvi unaofanywa na baadhi ya wavuvi;

- Uhaba wa wafanyakazi na nyenzo za kufanyia kazi za doria;

- Uwezo mdogo wa jamii wa kuekeza katika ufugaji wa mazao ya baharini kutokana na gharama kubwa za uwekezaji;

- Uhaba wa taaluma na uelewa wa fani ya ufugaji wa mazao ya baharini kwa jamii;

- Migogoro baina ya wawekezaji wa sekta ya utalii *hotelier* na wavuvi, na kati ya wakulima wa mwani na wawekezaji, kati ya wakulima wa mwani na wavuvi na kati ya jamii za wavuvi; na

- Bei ndogo ya mwani inawarudisha nyuma wakulima wa mwani.

Mtazamo wa baadae katika sekta ya uvuvi

Mhe. Spika**,** mtazamo wa baadae katika sekta ya uvuvi ni kama ufuatavyo:-

- Kuelimisha wavuvi na wadau wengine juu ya uvuvi endelevu;

- Kushirikisha jamii katika kupanga, kutekeleza, kufuatilia na kufanya tathimini ya shughuli za uvuvi;

- Kushirikiana na Washirika wa Maendeleo na sekta binafsi katika kukuza sekta ya uvuvi ikiwemo kuwekeza katika ufugaji wa mazao ya baharini, uvuvi wa maji ya kina kirefu na viwanda vya usarifu wa samaki;

- Kushirikiana na wanajamii na vyombo vya sheria kuendeleza doria katika maeneo ya hifadhi na shughuli nyengine za baharini;

- Kuishirikisha jamii katika uhifadhi wa rasilimali za baharini na mazingira yake na kutoa ushauri wa kitaalamu katika harakati za ufugaji wa viumbe wa baharini;

- Kuendeleza mazungumzo na taasisi za fedha kuhusu uwezekano wa kutoa mikopo kwa wakulima wa mwani, wafugaji wa mazao mengine ya baharini pamoja na kujiunga na vikundi vya kuweka na kukopa; na

- Kuendeleza miundombinu ya ufugaji wa samaki na taaluma ya ufugaji kwa lengo la kuongeza tija kwa wafugaji wa mazao ya baharini.

TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MALENGO KWA MWAKA 2012/2013 NA MALENGO YA MWAKA 2013/2014

Mhe. Spika, malengo ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka 2012/2013 yametekelezwa na Idara sita ambazo ni Idara ya Mipango, Sera na Utafiti; Idara ya Uendeshaji na Utumishi; Idara ya Uzalishaji wa Mifugo; Idara ya Huduma za Utabibu wa Mifugo; Idara ya Maendeleo ya Uvuvi; Idara ya Mazao ya Baharini na Ofisi Kuu Pemba kama ifuatavyo:-

IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI

Mhe. Spika**,** Idara hii ina majukumu ya kuandaa, kutekeleza na kutathmini mipango, programu, sera na miradi ya maendeleo katika sekta za mifugo na uvuvi na kuendeleza mashirikiano na taasisi za kiserikali na zisizo za kiserikali.

Malengo ya Mwaka 2012/2013

Mhe. Spika**,** kwa mwaka wa fedha wa 2012/2013 Idara ya Mipango, Sera na Utafiti, ilijipangia kutekeleza malengo yafuatayo:-

- Kuendelea kutayarisha mipango kazi, mipango ya utekelezaji na miradi ya maendeleo kwa sekta za mifugo na uvuvi;
- Kuimarisha ukusanyaji wa takwimu za mifugo na uvuvi;
- Kuratibu kazi za utafiti wa mifugo na uvuvi;
- Kuzifanyia mapitio Sheria ya Mifugo na Sera ya Uvuvi na Mazao ya Baharini; na
- Kuendeleza mashirikiano na taasisi za kiserikali na zisizo za kiserikali za ndani, kikanda na kimataifa.

Utekelezaji wa Malengo ya Mwaka 2012/2013

Mhe. Spika, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti iliweza kuandaa Mpango Kazi wa Wizara wa mwaka 2012/2013 na kutayarisha Ripoti za Utekelezaji wa Mpango huo kwa kila robo mwaka na mwaka nzima kwa jumla. Kwa upande wa mipango na miradi ya maendeleo, Mpango wa Kuimarisha Kuku wa

Kienyeji umeandaliwa ili kuwawezesha wafugaji wetu kufuga kibiashara na kupata tija.

Vile vile, kufuatia kusainiwa kwa mkataba wa maeneo ya mashirikiano baina ya Tanzania na Oman, mapendekezo mawili ya miradi yameandaliwa katika hatua ya awali na kutumwa kwa Balozi ya Oman. Miradi hiyo ni ule wa kuwaendeleza wavuvi kuvua katika maji ya kina kirefu na mradi wa kuunganisha uzalishaji na masoko ya mazao ya mifugo ikiwemo ujenzi wa chinjio la kisasa ili kukuza soko la ndani hasa lile la utalii.

Mhe. Spika, wizara yangu imelenga kuimarisha ukusanyaji wa takwimu za mifugo na uvuvi. Idara pamoja na shughuli za kila siku za ufuatiliaji wa ukusanyaji wa takwimu za mifugo na uvuvi katika vyanzo vyake ikiwemo madikoni, machinjioni na vituo vya uzalishaji na karantini, imeweza kuwapatia mafunzo ya ukusanyaji wa takwimu za mifugo na uvuvi wafanyakazi 100 Unguja na Pemba.

Aidha, wizara yangu inashiriki kikamilifu katika utekelezaji wa Programu ya Kuimarisha Takwimu za Kilimo Tanzania. Programu hii ina lengo la kuimarisha upatikanaji wa takwimu za kisekta pamoja na kuelimisha wafanyakazi. Progaramu hii inafadhiliwa kwa pamoja na shirika la msaada wa maendeleo la Marekani "*USAID*", Benki ya Dunia na Shirika la Kilimo na Chakula la Umoja wa Mataifa "*FAO*".

Mhe. Spika, katika kuimarisha utafiti, Wizara yangu ilikuwa na azma ya kuanzisha Baraza la Utafiti wa Mifugo na Uvuvi, kazi iliyofanyika kwa kiwango kikubwa katika mwaka wa fedha 2012/2013. Hata hivyo, azma hiyo haipo tena hivi sasa kwa vile Wizara ya Kilimo na Maliasili imeunda Baraza la Utafiti wa Kilimo, baraza ambalo linajumuisha utafiti wa mifugo na uvuvi. Kwa mantiki hiyo, hivi sasa tumelenga kuanzisha vituo vya utafiti vya mifugo na uvuvi. Wizara yangu sasa inashirikiana na taasisi ya utafiti kutoka Korea kuanzisha kituo cha majaribio ya utafiti wa mazao ya baharini huko Mkokotoni Unguja. Aidha, kwa kushirikiana na Taasisi ya Utafiti wa Baharini kutoka China *"State Oceanic Administration*", wizara yangu imefikia makubaliano ya kuendeleza shughuli za utafiti wa ufugaji wa mazao ya baharini.

Mhe. Spika, katika kuzifanyia mapitio Sheria ya Rasilimali ya Mifugo, idara kwa kushirikiana na Tume ya Marekebisho ya Sheria, imeweza kuifanyia mapitio Sheria ya Rasilimali ya Mifugo kwa kuweza kukusanya maoni kutoka kwa wadau wa mifugo kutoka wilaya zote za Zanzibar ikiwemo watendaji wa

wizara yetu. Wizara imeweza kuelimisha jamii kutoa maoni kupitia vipindi vya redio na televisheni kwa ajili ya kuifanyia mapitio Sheria no.11 ya Rasilimali za Mifugo ya mwaka 1999. Aidha, Kanuni za Maeneo ya Hifadhi za Baharini imepitiwa. Kwa upande wa Sera ya Uvuvi na Mazao ya Baharini, kazi hii haikufanyika kutokana na uhaba wa nyenzo. Hata hivyo, kazi hiyo inatarajiwa kufanyika katika mwaka wa fedha wa 2013/2014.

Mhe. Spika, kazi ya kuendeleza mashirikiano na taasisi za kiserikali na zisizo za kiserikali za ndani, kikanda na kimataifa imefanyika kwa kushiriki vikao tofauti vya ndani na nje ya nchi. Baadhi ya vikao hivyo ni pamoja na vile vya Tanzania na Oman huko Dar es Salam kilichopelekea kusainiwa kwa maeneo ya mashirikiano, vikao na Ofisi ya Taifa ya Takwimu *"National Bureau of Statistics*" katika kuandaa Mpango wa Kuimarisha Takwimu za Kilimo ikiwemo mifugo na uvuvi. Aidha, Idara imeshiriki katika mkutano wa kimataifa wa mashirikiano na Shirika la Kimataifa la Nishati ya Atomiki na Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa.

Vile vile, wizara inashirikiana na Taasisi za Utafiti ya Korea ya Kusini kupitia *KOICA* na *State Oceanic Administration* (*SOA*) ya Jamhuri ya Watu wa China na kukubaliana kushirikiana katika kufanya utafiti katika uzalishaji wa mazao ya baharini. Ushiriki wetu katika vikao vyote hivi tumeweza kubadilisha uzoefu wa kiutendaji, kutoa mapendekezo yetu ya kisera na kimkakati katika kuendeleza sekta zetu za mifugo na uvuvi sambamba na kutafuta uwezekano wa kupata misaada ya kusaidia utekelezaji wa malengo yetu.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti iliidhinishiwa jumla ya shilingi 239,001,000 kutekeleza kazi za kawaida. Kati ya hizo, shilingi 73,327,000 ni kwa mishahara na shilingi 165,674,000 ni kwa matumizi mengineyo. Hadi kufikia mwezi Aprili 2013, jumla ya shilingi 55,003,650 sawa na asilimia 75 zimepatikana kwa kulipia mishahara na shilingi 77,000,000, sawa na asilimia 55.2 kwa matumizi mengineyo. Kwa upande wa miradi ya maendeleo, Idara ilipangiwa kupata shilingi 200,000,000 kutekeleza Programu ya Kuimarisha Miundombinu ya Mifugo na hadi kufikia Aprili 2013 programu hiyo ilishapatiwa shilingi 32,000,000 tu ambazo ni sawa na asilimia 16.

Malengo ya Mwaka 2013/2014

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2013/2014, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti inakusudia kutekeleza malengo yafuatayo:-

- Kuimarisha mipango ya utekelezaji wa malengo ya sekta ya mifugo na uvuvi;

- Kuendelea na mapitio ya Sera ya Uvuvi na Mazao ya Baharini

- Kuimarisha upatikanaji wa takwimu sahihi za mifugo na uvuvi;

- Kuratibu kazi za utafiti; na

- Kuimarisha mashirikiano na taasisi za ndani na nje ya nchi.

Mhe. Spika, Kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti inaombewa jumla ya shilingi 206,026,000. Kati ya fedha hizo, shilingi 73,328,000 ni mishahara na shilingi 132,698,000 ni kwa matumizi mengineyo.

Mhe. Spika, Katika mwaka wa fedha wa 2013/2014 Idara pia itatekeleza Programu moja ya Kuendeleza Miundombinu ya Ufugaji, ambayo inaombewa jumla ya shilingi 200,000,000 (Kiambatanisho nam. 1).

IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI

Mhe. Spika, Idara ya Uendeshaji na Utumishi inasimamia na kuratibu uendeshaji wa kazi za kila siku za Wizara, kuweka kumbukumbu za wafanyakazi, kutunza mali za Serikali zilizo chini ya Wizara, kusimamia haki na wajibu wa wafanyakazi na kuhakikisha ya kwamba sheria, kanuni na taratibu zote zinazohusu matumizi ya mali za Serikali ndani ya Wizara zinafuatwa pamoja na kuandaa na kutekeleza mpango wa mafunzo kwa wafanyakazi, kuratibu kazi za uhasibu, manunuzi, ukaguzi wa ndani wa hesabu za Wizara na mambo mtambuka.

Mhe. Spika**,** hadi kufikia mwezi wa Juni 2013, Wizara yangu ilikuwa na wafanyakazi 764 ambapo 575 wapo Unguja na 189 wapo Pemba. Kati ya wafanyakazi hawa, 232 ni wanawake na 532 ni wanaume (Kiambatanisho nam. 2). Idadi hiyo ni pamoja na wafanyakazi wapya 40 walioajiriwa na Wizara katika mwaka wa fedha 2012/2013 kati ya 159 wanaohitajika. Wafanyakazi 17 wamestaafu na 5 walifariki wakiwa wamo ndani ya utumishi wa umma. Mwenyezi Mungu awalaze Peponi, Amin.

Mhe. Spika, Hata hivyo, wizara yangu bado inakabiliwa na upungufu wa wafanyakazi wataalamu hasa katika nyanja za utafiti, takwimu, uvuvi na madaktari wa mifugo. Hivi sasa wapo wataalamu 193 ambapo mmoja (1) tu ana kiwango cha Shahada ya tatu *Ph D*, 19 shahada ya pili *MSc*, 26 Shahada ya kwanza *BSc*, 4 Stashahada ya uzamili *PGD*, 5 Stashahada ya juu *Advance Diploma*, 138 Stashahada ya kawaida *Ordinary Diploma*. (Kimbatanisho nam. 3).

Malengo ya Mwaka 2012/2013

Mhe. Spika**,** katika mwaka wa fedha 2012/2013, Idara ya Uendeshaji na Utumishi ilijipangia kutekeleza malengo yafuatayo:-

- Kuwaongezea uwezo wa kitaaluma wafanyakazi kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na mrefu;
- Kutoa mafunzo ya sheria mpya ya kazi (Utumishi wa Umma) ya mwaka 2011 kwa wafanyakazi;
- Kuimarisha mazingira ya utendaji kazi;
- Kushajiisha uzalishaji katika vikundi vya jamii;
- Kuongeza taaluma juu ya mambo mtambuka ikiwemo elimu ya Ukimwi, jinsia, ulemavu, utawala bora, mazingira na matumizi ya madawa ya kulevya; na
- Kuimarisha ushikiriano na taasisi nyengine za kitaifa, kikanda na kimataifa.

Utekelezaji wa Malengo ya Mwaka 2012/2013

Mhe. Spika, Idara hii imefanikiwa kutekeleza malengo iliyojipangia kwa mwaka wa fedha 2012/ 2013 kama ifuatavyo:-

- Jumla ya wafanyakazi 32 waliendelezwa kitaaluma katika ngazi tofauti ikiwemo mmoja katika ngazi ya Shahada ya tatu *PhD*, wanne ngazi ya shahada ya pili *MSc*, 15 ngazi ya Shahada ya kwanza *BSc*, nane ngazi ya stashahada na wanne ngazi ya astashahada. Aidha wafanyakazi wengine

12 walipatiwa fursa ya kuendelezwa kwa masomo ya muda mfupi ndani na nje ya nchi;

- Wafanyakazi 100 walipatiwa mafunzo juu ya sheria mpya ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2011;

- Mazingira ya utendaji kazi yameimarika kwa Wizara kuhamia katika majengo yake mapya Unguja *Nyangumi House* hapo Maruhubi na Pemba *Jodari House* huko Weni. Hali hii imeongeza nafasi ya kufanyakazi kwa ufanisi na kupunguza msongamano;

- Wizara iliweza kushajiisha vikundi vya uzalishaji Unguja na Pemba kuongeza uzalishaji wa bidhaa zao kwa kuwatembelea na kuwapatia ushauri na nyenzo kwa lengo la kuwaongezea ufanisi. Vikundi 13 vimepatiwa msaada wa nyenzo na fedha;

- Kamati ya mambo mtambuka ya wizara imeendelea kufanyakazi zake za kushajiisha uingizaji wa mambo mtambuka katika masuala ya kazi; na kuwapatia taaluma wafanyakazi 50 wa Wizara pamoja na wadau wa mifugo na uvuvi 50 juu ya masuala ya UKIMWI na jinsi ya kuepukana na maambukizo mapya; na

- Wizara imeendeleza ushirikiano na taasisi tofauti za nchini pamoja na Wizara nyengine za Serikali katika kutekeleza majukumu ya kuwaendeleza wananchi kiuchumi. Taasisi hizo ni Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo ambayo tunashirikiana nayo kwa masuala ya takwimu, miradi na mipango ya maendeleo. Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika, tunashirikiana nayo katika kuwawezesha vijana kujiajiri katika masuala ya mifugo na uvuvi kwa kuwapatia mitaji.

Mhe. Spika**,** kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Idara ya Uendeshaji na Utumishi iliombewa jumla ya shilingi 585,412,000 kwa kutekeleza shughuli za kawaida. Kati ya hizo shilingi 340,612,000 ni kwa mishahara na shilingi 244,800,000 kwa matumizi mengineyo. Hadi kufikia mwezi wa Aprili, 2013, shilingi 303,933,084 sawa na asilimia 89 zimepatikana kwa kulipia mishahara

na jumla ya shilingi 138,235,088 sawa na asilimia 56.4 zimepatikana kwa matumizi mengineyo

Malengo ya Mwaka 2013/2014

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Idara inakusudia kutekeleza yafuatayo:-

- Kuimarisha mazingira ya utendaji kazi; kwa kuwapatia wafanyakazi nyenzo zitakazo wezesha kufanyika kazi kwa ufanisi;

- Kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa kazi za Idara na Wizara kwa ujumla; kwa viongozi wa Wizara kutembelea na kukagua utendaji kazi katika vituo mbali mbali;

- Kuendelea kusimamia udhibiti wa mali za Serikali na kuyapatia hati miliki maeneo ya Wizara;

- Kuendelea kusimamia haki na wajibu wa wafanyakazi; na

- Kuwaendeleza wafanyakazi kitaaluma katika nyanja mbalimbali za uzalishaji na utabibu wa mifugo, uzalishaji wa mazao ya baharini, uvuvi wa bahari kuu, utawala, uchumi na mambo mtambuka.

Mhe. Spika, Kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Idara ya Uendeshaji na Utumishi inaombewa jumla ya shilingi 701,768,000 kutoka Serikalini kwa kutekeleza kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo, shilingi 352,723,000 ni kwa mishahara na shilingi 349,045,000 kwa matumizi mengineyo.

IDARA YA UZALISHAJI MIFUGO

Mhe. Spika**,** kazi za Idara hii ni kupanga, kuratibu na kusimamia utekelezaji wa mikakati na programu za maendeleo ya mifugo kwa lengo la kuongeza uzalishaji wa mifugo. Idara hii hutoa taaluma ya ufugaji bora wa mifugo na mazao yake, ili kuleta tija kwa wafugaji na wananchi kwa ujumla. Pia Idara hii ina jukumu la kuimarisha uzalishaji wa mifugo ya asili kwa kuboresha koosaafu za mifugo yetu ya asili.

Malengo ya Mwaka 2012/2013

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2012/2013 Idara ililenga kutekeleza yafuatayo:-

- Kuimarisha huduma za elimu kwa wafugaji kwa kuzingatia mahitaji ya jamii ya wafugaji;
- Kuongeza uzalishaji wa mifugo na mazao yake kwa kushirikiana na wafugaji na kufanya utafiti wa mifugo;
- Kuimarisha utoaji wa huduma za kupandisha ng'ombe kwa sindano;
- Kutoa nafasi za ajira kwa vijana kupitia shughuli za ufugaji,
- Kuimarisha mazingira ya utendaji wa kazi;
- Kuimarisha mashamba na vituo vya mifugo; na

Kushajiisha utumiaji wa nishati mbadala (*biogas*) ili kutunza mazingira.

Utekelezaji wa Malengo ya Mwaka 2012/2013

Mhe. Spika, utekelezaji wa malengo haya ulikuwa kama ifuatavyo:-

- Idara imetoa elimu kwa wafugaji kwa kuwatembelea wafugaji mmoja mmoja na vikundi vya ufugaji katika mashamba yao, kwa kutumia radio na *TV*, kufanya ziara za wafugaji kwa wafugaji miongoni mwao na kufanya mashamba darasa. Jumla ya wafugaji 18,001 wametembelewa na kupatiwa ushauri wa ufugaji kitaalamu ikiwa ni pamoja na ufugaji bora wa ng'ombe, mbuzi, kuku na bata. Vipindi 7 vya redio na 4 vya *TV* vimetayarishwa na kurushwa. Aidha, wafugaji 10 wamepata mafunzo juu ya uhifadhi malisho ya mifugo, ziara 2 za wafugaji 15 wa kuku na 20 za wafugaji mbuzi zimefanywa na wafugaji 20 wameshiriki mafunzo juu ya kuongeza thamani mazao ya mifugo;

- Utafiti mdogo wa kuku umeendelezwa kwa kushirikiana na wafugaji kwa kutumia aina 3 za kuku wa kigeni na kuku wa kinyeji. Mambo yanayoangaliwa katika utafiti huo ni pamoja na uzalishaji, ukuaji, ustahamilivu wa maradhi na ulezi. Katika matokeo ya mwanzo kuku chotara waliotokana na utafiti huu wameonyesha uwezo wa kutaga wastani wa mayai 180 kwa mwaka kutoka wastani wa mayai 65 yanayotagwa na kuku wetu wa asili. Jumla ya majogoo bora 180 yamesambazwa kwa wafugaji Unguja na Pemba;

- Katika kuimarisha utoaji wa huduma za kupandisha ng'ombe kwa sindano, Idara imekamilisha ujenzi wa uzio wa kituo cha kupandishia ng'ombe kwa sindano kilichopo Maruhubi. Ekari mbili za shamba la kituo zimeoteshwa malisho. Hadi kufika Aprili 2013, ng'ombe 2,540 wamepandishwa kwa sindano Unguja na Pemba (Kiambatanisho nam. 4);

- Kwa kushirikiana na Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika, vijana 40 (wanawake 20 na wanaume 20) wamepatiwa mafunzo ya ufugaji wa kuku na kupatiwa kuku 400 katika shehia za Kikobeni na Kibeni wilaya ya Kaskazini A, Unguja. Kila kijana amepatiwa kuku majike tisa wa kinyeji au chotara na jogoo bora 1. Kwa upande wa Pemba, vijana 40 (wanawake 21 na wanaume 19) wamepatiwa mafunzo ya ufugaji wa kuku na hivi sasa wanaendelea na kazi ya ujenzi wa mabanda ya kuku na baada ya kukamilisha vijana hao watapatiwa kuku ili waweze kujiendeleza katika ufugaji. Aidha, wafugaji 40 katika wilaya ya Kusini Unguja na vijana 40 kutoka wilaya ya Micheweni Pemba wamo katika matayarisho ya kupatiwa mafunzo na kuwezeshwa kufuga kuku na mbuzi;

- Idara imeendelea kuimarisha mazingira ya kazi kwa kununua vifaa vya ofisi na kuwapatia wafanyakazi 5 pikipiki, kuwaendeleza wafanyakazi 6 katika mafunzo ya muda mrefu na wafanyakazi 2 kwa mafunzo ya muda mfupi;

- Idara imeendelea kutoa huduma za kinga na tiba kwa mifugo yake iliyoko kwenye mashamba na vituo vya utafiti huko Kitumba, Chamanagwe na Pangeni. Aidha, ujenzi wa uzio wa waya wa mita 350 katika shamba la malisho la Kizimbani umekamilika na jumla ya ekari 13 zimepandwa majani ya aina mbali mbali ya malisho kwa ajili ya kuwapatia wafugaji mbegu bora za malisho, na ukarabati wa afisi katika kituo cha utafiti Chamanangwe umefanyika; na

- Vipindi 2 vya redio na TV vimetayarishwa na kurushwa hewani ili kushajiisha jamii juu ya matumizi ya samadi kwa uzalishaji wa nishati mbadala pamoja na kutunza mazingira na kupunguza matumizi ya kuni na makaa kwa kupikia. Jumla ya mitambo 11 ya *biogas* ya aina ya mahandaki imejengwa kwa wafugaji waliohitajia huduma hiyo; Unguja mitambo minane na Pemba mitambo mitatu.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013 Idara hii ilikadiriwa kukusanya mapato ya shilingi 9,000,000 yatokanayo na huduma ya kupandisha ng'ombe kwa sindano. Hadi kufikia mwezi wa Aprili 2013 jumla ya shilingi 2,245,000 zimekusanywa ambazo ni sawa na asilimia 25 ya lengo lililowekwa.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Idara ya Uzalishaji Mifugo iliombewa jumla ya shilingi 571,500,000 kutoka serikalini kwa kazi za kawaida. Kati ya hizo shilingi 452,500,000 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi 119,000,000 kwa matumizi mengineyo. Hadi kufikia mwezi Aprili 2013 jumla ya shilingi 70,500,000 sawa na asilimia 59 zimepatikana kwa matumizi mengineyo.

Mhe. Spika, Katika mwaka wa fedha 2012/2013, Idara ilitekeleza mradi mmoja wa Upandishaji Ng'ombe kwa Sindano ambao uliombewa shilingi 122,000,000 (Kiambatisho nam. 5) na hadi kufikia mwezi wa Aprili 2013, ulishapata shilingi 116,000,000 sawa na asilimia 95.

Malengo ya Mwaka 2013/2014

Mhe. Spika, kwa mwaka 2013/2014, Idara ya Uzalishaji Mifugo inalenga kutekeleza malengo yafuatayo:-

a) Kuongeza uzalishaji mifugo na mazao yake kwa kutumia mikakati ifuatayo:-

i. Kuimarisha huduma za ugani (elimu kwa wafugaji),

ii. Kuvijengea uwezo vituo vya utafiti wa mifugo,

a. Kuongeza thamani na ubora wa mazao na bidhaa za mifugo.

b) Kuongeza mwamko wa matumizi ya samadi kama nishati mbadala kwa kutumia mikakati ifuatayo:-

i. Kuchangia ujenzi wa mitambo 14 ya *biogas*,

a. Kuitangaza teknolojia ya biogesi kwa jamii kupitia kipindi kimoja cha redio na kimoja cha TV,

ii. Kutathmini ubora wa mitambo ya *biogas* iliyokwisha fungwa.

c) Kuimarisha utoaji huduma za mifugo kwa jamii kwa kutumia mikakati ifuatayo:-

i. Kuimarisha mazingira ya utendaji kazi,

ii. Kufanikisha haki na fursa kwa wafanyakazi,

iii. Kuimarisha ufuatiliaji wa kazi za Idara.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Idara ya Uzalishaji Mifugo inategemea kukusanya mapato ya jumla ya shilingi 9,000,000 yatokanayo na huduma za uzalishaji wa mifugo.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Idara inaombewa jumla ya shilingi 565,637,000 kutoka serikalini kwa kazi za kawaida. Kati ya hizo shilingi 112,948,000 zinaombwa kwa matumizi mengineyo na shilingi 452,689,000 kwa ajili ya mishahara. Aidha, Idara itatekeleza Mradi mmoja wa Upandishaji Ng'ombe kwa Sindano ambao unaombewa shilingi 100,000,000 (Kiambatanisho nam. 13).

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Idara hii itatekeleza Mradi wa Kuendeleza Wafugaji Wadogo Wadogo katika programu ya pamoja ya Ajira kwa Vijana (*Youth Employment Programme*) kwa kushirikiana na Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika. Mradi huu unatarajiwa kutoa nafasi 120 za ajira kwa vijana. Ajira 80 zitatokana na ufugaji wa kuku na ajira 40 ni kupitia ufugaji wa mbuzi wa maziwa. Mradi huu umetengewa shilingi 108,660,000 kutoka Programu ya Ajira kwa Vijana inayosimamiwa na Wizara ya Kazi Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika.

IDARA YA HUDUMA ZA UTABIBU WA MIFUGO

Mhe. Spika, maendeleo ya sekta ya mifugo yanategemea sana afya za mifugo yetu. Aidha, mifugo ndio chanzo kikubwa cha maambukizo ya maradhi kwa binaadamu. Idara ya Huduma za Utabibu wa Mifugo ina jukumu la kudhibiti maradhi kwa mifugo yetu kwa kutoa huduma za kinga na tiba za maradhi ya mifugo. Idara pia ina jukumu la kuhakikisha mifugo yetu haisambazi maradhi kwa binadamu na kuilinda nchi yetu isipate maambukizi ya maradhi ya mifugo kutoka nje ya nchi kwa kufanya ukaguzi wa wanyama wanaoingizwa nchini. Vilevile, Idara hii inasaidia kushajihisha jamii ili iondokane na vitendo vya ukatili wa wanyama na kufanya uchunguzi wa mwenendo wa maradhi ya kuambukiza na yenye kuathiri mifugo yetu, kubuni mbinu za kukabiliana na maradhi hayo na kufanya utafiti wa maradhi ya mifugo.

Malengo ya Mwaka 2012/2013

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2012/2013, Idara ililenga kutekeleza yafuatayo: -

a) Kuendeleza udhibiti wa maradhi ya mifugo kwa kuimarisha vituo vya karantini, maabara na vituo vya mifugo;

b) Kutoa taaluma kwa wafugaji juu ya kuwakinga wanyama na maradhi ya kuambukiza na kuzuia ukatili wa wanyama;

c) Kuongeza uwezo wa kitaaluma kwa wafanyakazi kwa mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu ndani na nje ya nchi;

d) Kuimarisha mazingira ya kazi; na

e) Kuendeleza utaratibu wa ufuatiliaji, takwimu na tathmini ya maradhi ya mifugo.

Utekelezaji wa Malengo ya Mwaka 2012/2013

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013, Idara ilitekeleza yafuatayo:-

a) Wanyama 372,953 walikaguliwa na kuruhusiwa kuingia nchini kupitia vituo vya karantini. Kati ya wanyama hao, ng'ombe ni 5,124, mbuzi ni 118, kuku (vifaranga vya mayai na vya nyama) 367,925 na wanyama wengine 70. Aidha, mayai ya mbegu 294,800 yaliingizwa nchini. Wanyama 125,639 (Unguja 53,554 na Pemba 72,085) walichanjwa na wanyama 44,999 (Unguja 21,117 na Pemba 23,882) walikogeshwa kwa lengo la kuwakinga na maradhi mbali mbali ya kuambukiza na maradhi yanayosambazwa na kupe na

wadudu wengine wanaoathiri mifugo. Vile vile wanyama 131,031 wametibiwa kutokana na maradhi mbalimbali ya mifugo; kati yao, ng'ombe ni 14,151, mbuzi 8,880, kuku na jamii ya ndege 90,896, punda 4,302, mbwa 9,080 na paka 3,722. Mbwa 445 na paka 680 walifungwa uzazi kwa lengo la kupunguza wanyama wazururaji. Aidha, jumla ya vituo 5 vya kutoa huduma za mifugo vimekarabatiwa. Vituo hivyo ni Potoa, Dunga, Kisakasaka, Wete na Chake Chake. Aidha majosho 2 ya Binguni na Makangale yamekarabatiwa;

b) Jumla ya vijana 43 (*Community Animal Health Workers – CAHWs*) kutoka wialya zote za Unguja na Pemba, walipatiwa taaluma ya kinga na tiba, aidha wafugaji 70 walipatiwa taaluma juu ya haki za wanyama na utunzaji bora wa mifugo sambamba na kutoa elimu kupitia redio na vipeperushi;

c) Wafanyakazi 12 wameendelezwa kitaaluma kwa kuwalipia gharama za masomo katika vyuo vya ndani na nje ya nchi katika viwango vya shahada ya tatu (PhD) mmoja, shahada ya kwanza (BSc) nane, Diploma wawili na Cheti mmoja;

d) Wafanyakazi 40 walipatiwa stahiki zao za likizo na 21 walilipwa posho za saa za ziada. Aidha, vifaa na madawa ya mifugo yamenunuliwa na kusambazwa vituoni; na

e) Ufuatiliaji na uwekaji wa takwimu za mwenendo wa maradhi mbali mbali ya mifugo umefanyika yakiwemo maradhi ya kupe, kutupa mimba, minyoo, maradhi ya kiwele, kichaa cha mbwa, maradhi ya kuku na maradhi ya mifugo yasiyokuwa na mipaka.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2012/2013 Idara ya Utabibu wa Mifugo ilikadiriwa kukusanya mapato ya shilingi 59,000,000 kutokana na huduma za utabibu wa mifugo. Hadi kufikia mwezi wa Aprili, 2013 jumla ya shilingi 37,009,100 zimekusanywa ambazo ni sawa na asilimia 63 ya lengo lililowekwa.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2012/2013, Idara ilipangiwa kutumia shilingi 628,630,000. Kati ya hizo shilingi 508,630,000 ni mishahara na shilingi 120,000,000 kwa matumizi mengineyo. Hadi kufikia mwezi wa Aprili, 2013 shilingi 64,000,000 sawa na asilimia 53 zimepatikana kwa matumizi mengineo.

Mhe. Spika, Katika mwaka wa fedha 2012/2013, Idara ilitekeleza miradi miwili ya maendeleo. Mradi wa Kudhibiti Mafua ya Ndege ambao uliombewa shilingi 80,000,000 na hadi kufikia mwezi wa Aprili 2013, ulishapata shilingi 10,725,000 sawa na asilimia 13. Mradi mwengine ni wa Mradi wa Kudhibiti Kichaa cha Mbwa ambao uliombewa shilingi 80,000,000 na hadi kufikia mwezi wa Aprili 2013 uliingiziwa shilingi 13,000,000 sawa na asilimia 16.25.

Malengo ya Mwaka 2013/2014

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2013/2014, Idara ya Huduma za Utabibu wa Mifugo inalenga kutekeleza yafuatayo: -

a) Kuendeleza udhibiti wa maradhi ya mifugo kwa kuimarisha vituo vya karantini, maabara na vituo vya huduma ya mifugo;

b) Kuendeleza huduma za ugani kwa wafugaji juu ya kuwakinga wanyama na maradhi ya kuambukiza, kupe na kuhamasisha wananchi juu ya kuzuia ukatili kwa wanyama;

c) Kuongeza uwezo wa kitaaluma kwa wafanyakazi kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu ndani na nje ya nchi;

d) Kuimarisha mazingira ya kazi kwa kuwapatia wafanyakazi stahiki zao na vitendea kazi na kufuatilia utekelezaji wa wajibu wao; na

e) Kuendeleza utaratibu wa ufuatiliaji wa kazi vijijini na kuweka takwimu na tathmini ya maradhi mbali mbali ya mifugo.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2013/2014 Idara hii inakadiriwa kukusanya mapato ya jumla ya shilingi 59,000,000 yatakayotokana na ushuru wa huduma za utabibu wa mifugo.

Mhe. Spika, katika kutekeleza malengo ya mwaka 2013/2014 Idara ya Utabibu wa Mifugo inaombewa jumla ya shilingi 605,598,000. Kati ya fedha hizo, shilingi 510,829,000 ni mishahara na 94,769,000 ni kwa matumizi mengineyo.

Mhe. Spika, Kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Idara itaendelea kutekeleza miradi miwili. Mradi wa Kudhibiti Mafua ya Ndege na Maradhi mengineyo yasiokuwa na mipaka (*Trans-boundary Animal Diseases*) ambao unaombewa shilingi 70,000,000 (Kiambatanisho nam. 6) na Mradi wa Kudhibiti Kichaa cha Mbwa ambao unaombewa jumla ya shilingi 160,000,000. Kati ya hizo

shilingi 60,000,000 ni fedha za Serikali na shilingi 100,000,000 zitatolewa na washirika wa maendeleo (*World Society for Protection of Animals*) (Kiambatanisho nam. 7).

IDARA YA MAENDELEO YA UVUVI

Mhe. Spika, Idara ya Maendeleo ya Uvuvi ina majukumu ya kuendeleza uvuvi wenye tija na endelevu kwa kuhifadhi mazingira ya bahari pamoja na rasilimali zake. Aidha, Idara hii ina jukumu la kusimamia matumizi bora na yalio endelevu ya rasilimali hizo, kwa kusimamia utekelezaji wa sheria na kanuni zilizowekwa kwa nia ya kuinua uchumi wa jamii na taifa kwa jumla.

Malengo ya mwaka 2012/2013

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2012/2013 Idara ya Maendeleo ya Uvuuvi ilipanga kutekeleza yafuatayo:-

a) Kuimarisha usimamizi wa rasilimali za bahari;
b) Kuimarisha shughuli za uvuvi wa kienyeji na bahari kuu;
c) Kuimarisha shughuli za utafiti na uwekaji wa matumbawe ya kienyeji;
d) Kuimarisha mazingira ya utendaji kazi;
e) Kuongeza uwezo wa kitaaluma kwa wafanyakazi kwa mafunzo ya muda mfupi na mrefu ndani na nje ya nchi; na
f) Kuendeleza utaratibu wa ufuatiliaji, takwimu na tathmini ya samaki na wanyama wanaohofiwa kutoweka.

Utekelezaji wa Malengo ya Mwaka 2012/2013

Mhe. Spika, katika utekelezaji wa malengo ya mwaka 2012/2013, kazi zifuatazo zilifanyika:-

a) Jumla ya doria 250 zimefanywa ikiwa ni pamoja na doria kwenye maji ya kina kirefu. Katika doria hizo hakuna mvuvi aliyekamatwa;
b) Mafunzo ya utunzaji mazingira ya baharini yametolewa kwa wavuvi 3,000 wa maeneo yote ya hifadhi;
c) Utafiti wa maeneo yaliyoharibika kimazingira umefanywa na kuonekana ipo haja kwa maeneo hayo kuwekwa matumbawe ya kienyeji kwa lengo la kujirudi kirasilimali na hivyo kuongezeka kwa

samaki. Kati ya maeneo hayo ni pamoja na eneo la Ghuba ya Chwaka ambapo kwa kuanzia matumbawe 400 yameshawekwa. Maeneo mengine yatayofuata ni Jambiani na Mtende;

d) Vifaa kwa matumizi ya ofisi vimenunuliwa. Aidha gharama za matumizi ya ofisi kama mawasiliano, posta n.k. zimelipwa;

e) Jumla ya wafanyakazi 13 wakiwemo 7 wanaoendelea na masomo Tanzania Bara na wengine 6 ambao wapo nje ya Tanzania walilipiwa ada za masomo yao; na

f) Kwa kushirikiana na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Idara iliandaa semina ya mafunzo kwa wakusanyaji wa takwimu pamoja na kutembelea maeneo yote yanayochukuliwa takwimu. Hatua hii imekwenda sambammba na taaluma ya kudhibiti kuvuliwa wanyama wanaohofiwa kutoweka kama kasa, pomboo n.k.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013 Idara ilikadiriwa kukusanya mapato ya jumla shilingi 30,000,000 yanayotokana na leseni za uvuvi wa kienyeji. Mpaka kufikia mwezi Aprili 2013, shilingi 14,085,800 zimekusanywa ambazo ni sawa na asilimia 46.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013 jumla ya shilingi 387,498,000 zilipangwa kwa ajili ya kutekeleza kazi za kawaida. Kati ya hizo shilingi 297,026,000 ni kwa mishahara na shilingi 90,472,000 kwa matumizi mengineyo. Hadi kufikia mwezi Aprili 2013 shilingi 49,500,000 zimepatikana kwa matumizi mengineyo ambazo ni sawa na asilimia 55.

Mhe. Spika, kwa upande wa kazi za maendeleo, jumla ya shilingi 400,000,000 ziliombwa kutekeleza miradi miwili ya maendeleo. Kati ya fedha hizo shilingi 100,000,000 ni kwa Mradi wa *MACEMP* na shilingi 300,000,000 ni kwa ajili ya Mradi wa Kuimarisha Uvuvi wa Bahari Kuu. Hadi kufikia mwezi Aprili 2013 Mradi wa *MACEMP* umepata shilingi 30,000,000 sawa na asilimia 30 ya makadirio. (Kiambatanisho nam. 8) na Mradi wa Kuimarisha Uvuvi wa Bahari Kuu umepatiwa shilingi 9,000,000 ambazo ni sawa na asilimia 3 ya makadirio (Kiambatanisho nam. 9).

Malengo ya Mwaka 2013/2014

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Idara ya Maendeleo ya Uvuvi imepanga kutekeleza yafuatayo:-

a. Kuimarisha uvuvi wa kienyeji kwa kuongeza uelewa wa jamii juu ya uvuvi endelevu;

b. Kufanya doria 310 kutoka maeneo ya hifadhi na maeneo ya maji ya kina kirefu;

c. Kuimarisha shughuli za utafiti na uwekaji wa matumbawe ya kienyeji; na

d. Kuimarisha mazingira ya utendaji kazi;

Mhe. Spika, Katika mwaka wa fedha 2013/2014 Idara ya Maendeleo ya Uvuvi inakadiria kukusanya mapato ya shilingi 30,000,000 yanayotokana na mauzo ya leseni za uvuvi wa kienyeji.

Mhe. Spika, Kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Idara hii inaombewa kutumia jumla ya shilingi 379,526,000 kwa kazi za kawaida. Kati ya hizo, shilingi 297,026,000 ni kwa mishahara na shilingi 82,500,000 kwa matumizi mengineyo. Kwa kazi za maendeleo, Idara imepangiwa kutekeleza Mradi wa Kuendeleza Uvuvi wa Kina Kirefu cha Maji ambao umetengewa shilingi 100,000,000 (Kiambatanisho nam. 9).

Mhe. Spika, Vile vile, Idara hii itatekeleza Mradi wa Kuendeleza Uvuvi wa Bahari Kuu (kina kirefu cha maji) katika programu ya pamoja ya Ajira kwa Vijana (*Youth Employment Programme*) ambayo itatoa nafasi ya kuanzisha ajira kwa vijana 30 kwa kuwapatia mafunzo ya uvuvi wa maji ya kina kirefu. Mradi uko katika Programu ya Ajira kwa Vijana inayosimamiwa na Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika.

IDARA YA MAZAO YA BAHARINI

Mhe. Spika, Idara ya Mazao ya Baharini ina majukumu ya kuwaendeleza wafugaji wa samaki na mazao ya baharini, wakulima wa mwani pamoja na wadau wengine wanaojishughulisha na mazao ya baharini kwa ajili ya kuinua hali zao kiuchumi na kuinua pato la taifa.

Malengo ya mwaka 2012/2013

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Idara ya Mazao ya Baharini ilikusudia kutekeleza yafuatayo:-

a) Kuimarisha ukulima bora wa mwani na ufugaji wa mazao ya baharini;
b) Kuongeza uzalishaji wa mazao ya baharini;
c) Kuhamasisha usarifu na matumizi ya mazao ya baharini na ukuzaji wa soko la ndani na nje;
d) Kuimarisha mazingira ya utendaji kazi;
e) Kuongeza uwezo wa kitaaluma kwa wafanyakazi kwa mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu ndani na nje ya nchi; na
f) Kuendeleza utaratibu wa ufuatiliaji takwimu na tathmini ya uzalishaji wa mazao ya baharini.

Utekelezaji wa Malengo ya mwaka 2012/2013.

Mhe. Spika, utekelezaji wa malengo ya mwaka 2012/2013 ulikuwa kama ifuatavyo:

a. Jumla ya watu 29 wakiwemo wajasiriamali 23 na wafanyakazi 6 walihudhuria mafunzo juu ya njia bora za ufugaji wa mazao ya baharini na kilimo cha mwani nchini China. Aidha, mafunzo ya uimarishaji wa ukulima bora wa zao la mwani na ufugaji wa mazao ya baharini yamefanyika kwa wajasiriamali 154 wa mazao ya baharini ikiwemo wakulima wa mwani, wafugaji wa samaki, kaa, chaza na majongoo;

b. Katika kuongeza uzalishaji wa mazao ya baharini, Idara imekamilisha ujenzi wa bwawa moja la mfano au bwawa darasa "*Demonstration pond*" katika eneo la Jozani mkoa wa Kusini Unguja na kukabidhiwa wajasiriamali wa ufugaji wa samaki. Pia, jumla ya vifaranga vya samaki 10,995 vimesambazwa kwa wafugaji wa samaki Unguja na Pemba. Vile vile, Idara imesaidia vifaa vya ufugaji wa samaki, majongoo na kilimo cha mwani kwa vikundi 18 vya mazao ya baharini Unguja na Pemba;

c. Mafunzo ya usarifu na matumizi ya mazao ya baharini yametolewa kwa wajasiriamali 100 kutoka katika wilaya zote za Unguja. Aidha, Wakulima wa mwani kutoka vijiji 47 Unguja na Pemba wamenufaika na taaluma ya uimarishaji na uhifadhi wa ubora wa mwani "*Quality maintaining*" kwa ajili ya ukuzaji wa soko la nje na uhamasishaji wa matumizi ya mwani kwa ajili ya soko la ndani kama vile utengenezaji wa sabuni, vyakula (keki, vileja n.k.) na juisi ya matunda;

d. Mazingira ya utendaji kazi yameimarishwa kwa kuwapatia wataalamu 4 pikipiki kwa ajili ya kuwawezesha kufanya ufuatiliaji wa maendeleo ya shughuli za ufugaji wa mazao ya baharini vijijini Unguja na Pemba;

e. Mfanyakazi mmoja anaendelea na masomo ya muda mrefu ya stashahada ya rasilimali watu "*Diploma in Human Resources*" katika chuo cha Utumishi wa Umma (*Institute of Public Administration – Zanzibar*). Aidha, wafanyakazi 14 walihudhuria mafunzo ya muda mfupi ya ufugaji wa mazao ya baharini nchini China na Korea; na

f. Takwimu zimeendelea kukusanywa na kufanyiwa tathmini, ikiwemo samaki waliovunwa na kuuzwa, mwani uliozalishwa na kuuzwa, mazao ya baharini yaliyosafirishwa nje ya nchi pamoja na wageni wa kitalii waliotembelea maeneo yanayohifadhiwa kasa. Jumla ya wageni wa kitalii 4,179 wametembelea maeneo yanayohifadhiwa kasa huko Nungwi katika Mkoa wa Kaskazini Unguja na Jozani katika Mkoa wa Kusini Unguja ambapo wanavikundi walijipatia kiasi cha shilingi 17,537,000-.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2012/2013, mapato yatokanayo na ushuru wa usafirishaji wa mazao ya baharini nje ya Zanzibar yalikadiriwa kuwa shilingi 70,000,000 na hadi kufikia mwezi Aprili, 2013, shilingi 65,219,050 zimekusanywa ambazo ni sawa na asilimia 93 ya lengo.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2012/2013, Idara ya Mazao ya Baharini Unguja iliombewa jumla ya shilingi 206,653,000 kwa kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo shilingi 94,248,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi 112,405,000 ni kwa ajili ya mishahara. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2013 jumla ya shilingi 48,000,000 zimepatikana kwa ajili ya matumizi mengineyo ambazo ni sawa na asilimia 51 ya lengo.

Malengo ya Mwaka 2013/2014

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2013/2014, Idara ya Mazao ya Baharini imepanga kutekeleza yafuatayo:-

a) Kuimarisha ufugaji wa samaki, kaa, chaza, majongoo na mazao mengine ya baharini;

b) Kuendelea utoaji wa elimu kwa wakulima wa mwani juu ya ukulima bora wa mwani, uhifadhi na kuhamasisha matumizi ya mwani

na bidhaa zitokanazo na zao la mwani kwa maslahi ya akina mama na vikundi vinavyozalisha mwani; na

c) Kuwahamasisha wakulima wa mwani na wafugaji wa mazao ya baharini kujiunga na vikundi vya ushirika vya kuweka na kukopa ili kujipatia mitaji ambayo itawawezesha kuanzisha vyanzo vya ziada vya kujiongezea kipato.

Mhe. Spika, Katika kutekeleza malengo ya mwaka wa fedha wa 2013/2014, Idara inaombewa jumla ya shilingi 198,745,000. Kati ya fedha hizi, shilingi 112,405,000 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi 86,340,000 ni kwa matumizi mengineyo. Kwa upande wa kazi za maendeleo, Idara hii itatekeleza Mradi mmoja wa Kuimarisha Ufugaji wa Mazao ya Baharini ambao unaombewa shilingi 100,000,000 (Kiambatanisho nam. 10).

Mhe. Spika, Katika mwaka wa fedha 2013/2014, Idara inakadiria kukusanya mapato ya jumla ya shilingi 70,000,000 kutokana na ada za uzafirishaji wa mazao ya baharini.

OFISI KUU PEMBA

Mhe. Spika, Ofisi Kuu ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi Pemba, ina jukumu la kuratibu na kusimamia utekelezaji wa kazi zote za Wizara kwa Pemba. Kwa mwaka wa fedha 2012/2013, kazi zilizotekelezwa na ofisi hii ni miongoni mwa kazi zilizokwishaelezwa chini ya Idara zote zilizomo katika Wizara.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Ofisi Kuu Pemba ilitarajia kukusanya mapato ya jumla ya shilingi 45,000,000 lakini hadi kufikia mwezi Aprili 2013, jumla ya shilingi 17,154,300 zimekusanywa ambazo ni sawa na asilimia 38 ya lengo.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Ofisi Kuu Pemba inalenga kukusanya jumla ya mapato ya shilingi 45,000,000. Mapato haya yatatokana na huduma za utabibu wa mifugo shilingi 12,000,000, huduma za uzalishaji mifugo shilingi 6,000,000, leseni za uvuvi shilingi 6,000,000 na ushuru wa usafirishaji wa mazao ya baharini shilingi 21,000,000.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013, Ofisi Kuu Pemba iliombewa jumla ya shilingi 910,306,000 kwa ajili ya kazi za kawaida. Kati ya fedha hizi,

shilingi 520,500,000 ni mishahara na shilingi 389,806,000 ni kwa matumizi mengineyo. Hadi kufikia mwezi Aprili 2013 shilingi 580,132,513 zimepatikana ambazo ni sawa na asilimia 64.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Ofisi Kuu Pemba, imekadiria kutumia jumla ya shilingi 953,700,000 kutekeleza malengo yaliyoelezwa katika Idara mbali mbali. Kati ya fedha hizi, shilingi 527,000,000 ni kwa mishahara na shilingi 426,700,000 ni kwa matumizi mengineyo. Kwa upande wa matumizi mengineyo, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti imekadiriwa kutumia shilingi 51,200,000, Idara ya Uendeshaji na Utumishi shilingi 73,500,000, Idara ya Mazao ya Baharini shilingi 76,500,000, Idara ya Maendeleo ya Uvuvi shilingi 82,500,000, Idara ya Uzalishaji wa Mifugo shilingi 73,000,000 na Idara ya Utabibu wa Mifugo shilingi 70,000,000.

MUHTASARI WA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA 2012/2013

Ukusanyaji wa Mapato 2012/2013

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2012/2013 Wizara ilipangiwa kukusanya mapato ya shilingi 2,290,000,000. Kati ya mapato hayo, shilingi 2,077,000,000 zitatokana na leseni za uvuvi wa bahari kuu na shilingi 213,000,000 zitatokana na mapato ya ndani ya Wizara (ikiwemo ada za leseni za uvuvi wa ndani, utibabu wa wanyama na ada ya mazao ya baharini). Hadi kufikia mwezi wa Aprili 2013, Wizara ilikusanya mapato ya shilingi 146,560,000, sawa na asilimia 7 kutokana na leseni za uvuvi wa bahari kuu na shilingi 135,713,250 sawa na asilimia 64 kutokana na makusanyo ya ndani (Kiambatanisho nam. 11).

Matumizi ya Fedha 2012/2013

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013 Wizara yangu iliidhinishiwa jumla ya shilingi 5,292,160,000 ambapo shilingi 3,529,000,000 zilikuwa ni kwa kazi za kawaida na shilingi 1,763,160,000 ni kwa kazi za maendeleo. Kati ya fedha za kawaida shilingi 2,305,000,000 zilitengwa kwa mishahara na shilingi 1,224,000,000 ni kwa matumizi mengineyo. Hadi kufikia mwezi wa Aprili 2013, fedha zilizopatikana kwa kazi za kawaida ni shilingi 2,490,032,435 sawa na asilimia 71. Kwa upande wa matumizi mengineyo fedha zilizopatikana ni shilingi 601,485,751 sawa na asilimia 49 ya makadirio (Kiambatanisho nam. 14). Kwa kazi za maendeleo, jumla ya shilingi

960,000,000 ziliombwa serikalini na hadi kufikia mwezi Aprili 2013 shilingi 224,565,000 zilipatikana sawa na asilimia 23.4. Aidha, jumla ya shilingi 803,160,000 ziliombwa kutoka kwa washirika wa maendeleo kutekeleza miradi miwili ya maendeleo (*MACEMP* na Mradi wa Kudhibiti Kichaa cha Mbwa) ambapo jumla ya shilingi 891,360,000 zilipatikana sawa na asilimia 110 (Kiambatanisho nam. 12).

MAKADIRIO YA MAKUSANYO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA 2013/14

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Wizara inakadiria kukusanya jumla ya shilingi 613,000,000 kutoka katika vyanzo vyake mbali mbali vya mapato (Kiambatanisho nam. 11). Vile vile Wizara yangu inatarajia kutumia jumla ya shilingi 3,611,000,000 kwa kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo jumla ya shilingi 2,326,000,000 ni kwa mishahara na shilingi 1,285,000,000 ni kwa matumizi mengineyo (Kiambatanisho nam. 15). Kwa upande wa kazi za maendeleo jumla ya shilingi 1,294,000,000 zimetengwa ambapo shilingi 664,000,000 ni fedha kutoka kwa washirika wa maendeleo kwa kutekeleza miradi miwili (Mradi wa Kichaa cha Mbwa, na Mradi wa Kushajiisha Ufugaji wa Mazao ya Baharini) na shilingi 630,000,000 ni kutoka Serikalini kutekeleza miradi sita ya maendeleo (Kuimarisha Miundombinu ya Mifugo, Kudhibiti Maradhi ya mafua ya ndege na maradhi yasiyokuwa na mipaka, Kudhibiti Kichaa cha Mbwa, Kupandisha Ng'ombe kwa Sindano, Kuimarisha Ufugaji wa Samaki na Kuimarisha Uvuvi wa Bahari Kuu).

HITIMISHO

Mhe. Spika, sasa nachukua nafasi hii kwa niaba ya Wizara yangu kuzishukuru taasisi za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Jamhuri ya Watu wa China, Jamhuri ya Watu wa Korea, Serikali ya India, Serikali ya Israel, Serikali ya Norway, Serikali ya Japan, Serikali ya Misri, Serikali ya Uholanzi, Serikali ya Marekani, Serikali ya Uingereza na Ufalme wa Oman kwa kushirikiana nasi katika kuendeleza sekta ya mifugo na uvuvi. Vile vile napenda kuyashukuru mashirika ya maendeleo yakiwemo "GEF", "KOICA", "SADC", "UNICEF", "WSPA", Benki ya Dunia, Jumuiya ya Maendeleo ya Afrika "AU", Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa "FAO", Shirika la Afya Duniani "WHO", Shirika la Maendeleo la Japan "JICA", Mfuko wa Kimataifa wa Kuendeleza Kilimo "IFAD", Jumuiya ya Afrika Mashariki, "EAC", na Umoja wa nchi za Ulaya "EU" kwa kusaidia maendeleo ya sekta za uvuvi na mifugo. Vile vile napenda kuzishukuru taasisi binafsi hapa nchini, Wizara za SMZ, taasisi za Serikali na zisizo za kiserikali

kama Taasisi ya Sayansi za Baharini *''Indian Ocean Marine Affairs Society*", "ZAASO", "ZALWEDA" na "ZSPA" ambazo pia zimesaidia Wizara yangu kuleta maendeleo katika sekta za Mifugo na Uvuvi.

Mhe. Spika, naomba kuwashukuru na kuwapongeza kwa dhati viongozi wa Wizara yangu wakiwemo Naibu Waziri Mhe. Mohammed Said Mohammed, Katibu Mkuu Dk. Kassim Gharib Juma, Naibu Katibu Mkuu Dk. Omar Ali Amir, Afisa Mdhamini Pemba Nd. Mayasa Ali Hamad, Wakurugenzi wote, wataalamu na wafanyakazi wote wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi walioko Unguja na Pemba kwa utendaji wao mzuri na kufanyakazi kwa bidii na ustahamilivu mkubwa. Aidha, nawapongeza, wafugaji, wavuvi, wakulima na wafanyabiashara wa mwani, na wadau wengine wa sekta za mifugo na uvuvi kwa mashirikiano yao na jitihada wanazochukua kuendeleza sekta hizi japokuwa wanakabiliwa na changamoto mbali mbali. Napenda kuwahakikishia kwamba changamoto zilizopo tutazifanyia kazi kulingana na nyenzo zilizopo.

Mhe. Spika, napenda kuchukua fursa hii adhimu kuwashukuru viongozi na taasisi nyengine za Serikali wakiwemo Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Madiwani, Masheha, Kamati za Maendeleo za Shehia, Kamati za Wavuvi, Vikosi vya SMZ na vyombo vya habari kwa mashirikiano yao mazuri waliotupa ili kusaidia utekelezaji wa kazi zetu. Kwa niaba ya Wizara yangu napenda kuchukua fursa hii kuwaomba na kuwashauri wananchi wote waendelee kutumia bidhaa za ndani za mazao ya mifugo na uvuvi ili kuimarisha afya zao, kukuza soko la ndani na kuongeza kipato cha wafugaji na wavuvi wetu.

Mhe. Spika, naomba kukushukuru wewe binafsi na waheshimiwa wajumbe wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Habari na Uwezeshaji kwa miongozo yao wanayotupa katika kuendeleza sekta za mifugo na uvuvi kwa manufaa ya nchi yetu. Miongozo tuliyoipata katika Kamati hiyo imeweza kutusaidia kutatua baadhi ya changamoto zinazokabili maendeleo ya sekta hizi.

Mhe. Spika, mwisho nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu waipokee, waijadili na kuikubali bajeti ya Wizara yangu. Aidha, nawaomba waheshimiwa wajumbe watupe maoni, ushauri na mapendekezo yao katika kuendeleza sekta za mifugo na uvuvi kwa manufaa ya wafugaji, wavuvi, wakulima wa mwani na wananchi kwa jumla.

Mhe. Spika, kwa heshima kubwa naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 4,905,000,000 kwa ajili ya matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha wa 2013/2014. Kati ya fedha hizo shilingi 3,611,000,000 ni kwa ajili ya kazi za kawaida na shilingi 1,294,000,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kazi za maendeleo.

Mhe. Spika, na Waheshimiwa Wajumbe nakushukuruni kwa kunisikiliza na naomba kutoa hoja.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

KIAMBATANISHO NAM. 1: MRADI WA KUIMARISHA MIUNDOMBINU YA MIFUGO

JINA LA MRADI	**MRADI WA KUIMARISHA MIUNDOMBINU YA MIFUGO**
MUDA WA MRADI	Umeanza 2011/12 unamaliza 2014/15
JUMLA YA GHARAMA	Shilingi 7,200,000,000
Lengo kuu	Kuimarisha miundombinu ya mifugo ya uzalishaji na masoko ili kuongeza uza mazao yatokana ya mifugo na bidha za mifugo.
Fedha zilizotengwa 2012/2013	200,000,000

Malengo ya mwaka 2012/2013

a. Kuendeleza shughuli ya ujenzi wa chinjio la kisasa Kisakasaka;
b. Kuandaa michoro ya ujenzi wa kituo cha utafiti wa mifugo Chamanangwe;
c. Kuandaa michoro ya ujenzi wa maabara ya mifugo Kizimbani; na
d. Ujenzi wa kituo cha Unguja Ukuu na kuendeleza ukarabati wa vituo vya Mahonda na D

Utekelezaji halisi 2012/2013

- Kazi za kuandaa michoro kwa ajili ya chinjio la kisasa huko Kisakasaka imekamilika, ambapo m na 'Tender Document' tayari zimeshawasilishwa kwa hatua nyengine za utekelezaji;
- Mchakato wa kumpata mchoraji wa Kituo cha Utafiti Chamanangwe umekamilika. Hata hivyo mzabuni kuwa kubwa sana kulingana na makadirio, uchoraji hautoweza kufanyika; na
- Mchakato wa kumpata mchoraji wa ujenzi wa Maabara ya mifugo umekamilika. Hata hivyo mzabuni kuwa kubwa sana kulingana na makadirio, uchoraji hautoweza kufanyika.

Fedha zilizotengwa mwaka 2013/2014	TZs 100,000,000

Malengo ya mwaka 2013/2014

- Kujenga ofisi ndogo za karantini Donge na Nziwengi;
- Kujenga kituo cha kutolea huduma za utabibu na uzalishaji (AHPCs) Makangale;
- na Unguja Ukuu,
- Kujenga josho kwenye kijiji cha Mjimbini - Mkoani Pemba;
- Kukiimarisha kituo cha Konde kwa kukarabati josho na kukipatia umeme;
- Kufanya vikao 6 vya zabuni ya michoro ya maabara ya mifugo na Kituo cha
- Utafiti Chamanangwe;
- Kujenga kituo cha utafiti wa kuku 'poultry Unit' Chamanangwe;
- Kuandaa uchambuzi yakinifu (feasibility study) mradi wa miundo mbinu ya mifugo; na
- Kufuatilia utekelezaji wa kazi za mradi na kununua vitendea kazi na mawasiliano.

KIAMBATANISHO NAM.2: ORODHA YA WAFANYAKAZI KIIDARA NA KWA JINSIA ZAO UNGUJA NA PEMBA

Na:	IDARA	UNGUJA			PEMBA		
		W'UME	W'WAKE	JUMLA	W'UME	W'WAKE	JUMLA
1	Mipango, Sera na Utaafiti	7	4	11	3	1	4
2	Uendeshaji na Utumishi	46	28	74	14	9	23
3	Huduma za Utabibu wa Mifugo	112	76	188	38	8	46
4	Uzalishaji wa Mifugo	115	48	163	50	11	61
5	Maendeleo ya Uvuvi	85	26	111	34	5	39
6	Mazao ya Baharini	16	12	28	12	4	16
	JUMLA	**381**	**194**	**575**	**151**	**38**	**189**

KIAMBATANISHO NAM. 3: IDADI NA VIWANGO VYA ELIMU VYA WAFANYAKAZI WA WIZARA UNGUJA NA PEMBA

Na	NGAZI ZA UTAALAMU	IDADI UNGUJA	IDADI PEMBA	JUM
1	Shahada ya tatu (PhD)	1	-	
2	Shahada ya pili (MSc/MA)	18	1	
3	Shahada ya juu (PGD)	6	1	
4	Shahada ya Kwanza (BSc/BA)	19	8	
5	Diploma ya Juu (Advance Diploma)	4	1	
6	Diploma (Ordinary Diploma)	116	28	
7	FORM VI	4	1	
8	Cheti	106	41	
9	FORM IV	71	17	
10	O – FORM III	228	91	
	JUMLA	**573**	**189**	

KIAMBATANISHO NAM. 4: IDADI YA NGO'MBE WALIOPANDISHWA (A.I.) KIWILAYA KWA MWAKA 2012/2013

NA.	WILAYA	LENGO	WALIOPANDISHWA
UNGUJA			
1.	Magharibi	657	
2.	Kaskazini A	245	
3.	Kaskazini B	364	
4.	Kati	508	
5.	Kusini	226	
Jumla ndogo		**2,000**	**1**
PEMBA			
6.	Wete	689	
7.	Micheweni	232	
8.	Chake Chake	765	
9.	Mkoani	314	
Jumla ndogo		**2,000**	**1,**
JUMLA UNGUJA & PEMBA		**4,000**	**2**

KIAMBATANISHO NAM. 5: MRADI WA KUPANDISHA NG'OMBE KWA SINDANO

JINA LA MRADI	MRADI WA KUPANDISHA NG'OMBE KWA SINDANO
MUDA WA MRADI	Umeanza 2010/11 unamaliza 2017/18
JUMLA YA GHARAMA	TZs 122,000,000
Lengo kuu	Kupunguza umasikini kwa kungeza kipato cha wafugaji wadogo wadogo kwa kuongeza uzalishaji wa ng'ombe wa kienyeji kwa kupandishia madume borayenye sifa za uzalishaji wa maziwana kuzalisha ng'ombe chotara.
Fedha zilzotengwa 2012/2013	**TZs 122,000,000**

Malengo ya mwaka 2012/2013

- Kukamilisha ujenzi wa uzio kituoni;
- Kuimarisha huduma za upandishaji kwa kuzalisha lita 3,000 za liquid nitrogen na kupandisha ng'ombe 4000 kwa njia ya sindano;
- Kuimarisha huduma za afya kwa vidume vya mbegu (ununuzi wa madawa ya kinga na tiba)
- Kuimarisha lishe ya vidume vya mbegu (ununuzi wa chakula cha ziada); na
- Kuanzisha shamba la malisho kwa vidume vya mbegu.

Utekelezaji halisi 2012/2013

- Ujenzi wa uzio wa kituo cha kupandisha ng'ombe kwa sindano Maruhubi umemalizika;
- Huduma za upandishaji zimeimarishwa kwa kuzalisha lita 1,972 za "liquid nitrogen" na kupandisha ng'ombe 2,407 kwa njia ya sindano hadi kufikia mwezi wa Machi 2013;
- Huduma za afya za vidume vya mbegu zimeimarishwa kwa kukingwa maradhi kwa kukogeshwa na kuchajwa chanjo za FMD, LSD na ECF. Aidha, dawa (antibiotics) zimetumika kwa matibabu mbalimbali;
- Huduma za lishe kwa madume zimeimarishwa kwa kuwapatia chakula cha ziada; na
- Ekari mbili zimetayarishwa (zimelimwa) kwa ajili ya kupanda malisho ya ng'ombe katika eneo la kituo na ekari

moja tayari imeshapandwa majani.	
Fedha zilizotengwa mwaka 2013/2014	TZs 100,000,000
Malengo ya mwaka 2013/2014 • Kuimarisha kituo cha AI Maruhubi na huduma za Upandishaji; • Kupandisha ng'ombe 3,000 chotara na 1,000 wa asili; • Kukipatia kituo usafiri wa kuaminika (ununuzi wa gari); • Kuufanyia "service" mtambo wa "Liquid Nitrogen"; • Kununua reagents kwa ajili ya usarifu wa mbegu maabara; • Kutoa huduma kwa madume ya mbegu yaliyopo Kituoni; • Kununua madawa kwa ajili ya madume; • Kununua chakula kilo 3,000 cha madume; • Kukarabati mazizi mawili ya madume; • Uwekaji kumbukumbu kwa ajili ya tathmini; na • Ufatiliaji na usajili wa ng'ombe 2,500 waliopandishwa na ndama 1,500 waliozaliwa.	

KIAMBATANISHO NAM. 6: MRADI WA KUDHIBITI MAFUA YA NDEGE

Jina la mradi	**MRADI WA KUDHIBITI MAFUA YA NDEGE**
Muda wa mradi	2006/2007 – 2014/2015
Jumla ya gharama	TZS 1,200,0000
Lengo Kuu	Kudhibiti mafua ya ndege na magonjwa yasiyo na mipaka kuingia Zanzibar
Fedha zilizotengwa 2012/2013	TZS 80,000,000 kutoka SMZ
Malengo ya Mwaka 2012/2013: • Kufuatilia mwenendo wa mafua makali ya ndege pamoja na maradhi ya mifugo yasiyokuwa na mipaka; • Kutoa mafunzo kwa madaktari wasaidizi wa mifugo Wilayani juu ya upashanaji habari za magonjwa ya mifugo; • Ununuzi wa vifaa na madawa ya maabara za mifugo; • Kufuatilia mienendo ya maradhi mbali mbali yanayosambazwa na kupe; • Kutoa chanjo ya maradhi ya mahepe kwa kuku na vibuma kwa n'gombe; na • Uchunguzi wa maradhi ya kiwele na usafi wa maziwa.	
Utekelezaji Halisi 2012/2013: Hadi kufikia mwezi wa Aprili, 2013 kazi zifuatazo zilikuwa zimekamilika:- • Taarifa juu ya ufuatiliaji wa magonjwa yasio na mipaka zilikusanywa; • Madaktari wasaidizi 18 na CAHWs 36 walipaitiwa mafunzo juu ya tahadhari tya mripuko wa magonjwa ya mifugo pamoja na mbinu bora za kutambua ugonjwa na kuutibu; • Lita 11 za dawa ya kuulia kupe na mabomba 11 ya kupulizia dawa yamenunuliwa na kusambazwa katika vituo vya mifugo; • Uchunguzi wa maradhi yanayosambazwa na kupe umefanyika na ngombe 3,504 wamegunduliwa na maradhi (East coast Fever 2,504, Anaplasmosis 567, heart water 211, na babesiosis 177);	

- Jumla ya kuku 38,925 kati ya 200,000 walichanjwa chanjo ya mahepe sawa na asilimia 19 ya lengo. Kwa upande wa chanjo ya Vibuma ndama 33 walichanjwa kati ya ndama1499 waliopangwa sawa na asilimia 2; na
- Uchunguzi wa maradhi ya kiwele kwa ngombe umefanyika na n'gombe 307 wamegunduliwa kuwa na maradhi ya mastitis na walitibiwa

Fedha zilizotengwa 2013/2014	TZS 70,000,000

Malengo ya Mwaka 2012/2013:

- Kuendeleza Kazi za ufuatiliaji na tathmini ya shughuli za mradi na kufuatilia mwenendo wa maradhi;
- Kuendesha Mafunzo juu ya Mikakati ya kudhibiti magonjwa yasiyo na Mipaka kama vile mahepe chambavu, miguu na midomo n.k.;
- Ununuzi wa vifaa na madawa ya maabara kwa uchunguzi wa magonjwa;
- Kufanya ufuatiliaji wa magonjwa yanayosambazwa na kupe (TBD surveillance); na
- Kuendesha kampeni ya uchanjaji wa ugonjwa wa mahepe.

KIAMBATANISHO NAM. 7: MRADI WA KUDHIBITI KICHAA CHA MBWA

JINA LA MRADI	**MRADI WA KUDHIBITI KICHAA CHA MBWA**
MUDA WA MRADI	2005/2006 – 2014/2015
JUMLA YA GHARAMA	Gharama za mradi huu hupangwa kila mwaka na kuidhinishwa na mfadhili (WSPA) na Serikali.
Lengo Kuu	i. Kudhibiti na hatimae kutokomeza kichaa cha mbwa ili kutokomeza maambukizi ya kichaa kwa binaadamu. ii. Kuongeza muamko kwa wafugaji na raia juu ya haki za wanyama na kudhibiti ukatili dhidi yao
Fedha zilizotengwa 2012/2013	Jumla ya shilingi 80,000,000 kutoka SMZ na dola za kimarekani 44,000 (TZS 69,960,000) kutoka kwa washirika wa maendeleo zimetengwa kutekeleza kazi za Mradi

Malengo ya Mwaka 2012/2013 ya mradi ni kama yafuatayo:

- Kuendeleza kampeni ya uchanjaji mbwa 14,000 na paka 1,500;
- Kufunga uzazi mbwa 300 na paka 500 kwa lengo la kupunguza kuenea kwa mbwa na paka wazuzuraji;
- Kufanya matibabu ya maradhi mbali mbali ya mbwa na paka;
- Kutoa taaluma kwa jamii juu ya utunzaji bora wa mbwa na paka;
- Kuiboresha maabara ya uchunguzi wa maradhi ya mifugo ya Maruhubi – Unguja na Wete – Pemba;
- Kuelimisha jamii juu ya maradhi ya kichaa cha mbwa kupitia vyombo vya habari; na
- Kusaidia maendeleo ya uchunguzi kuhusu maradhi ya kichaa cha mbwa.

Utekelezaji Halisi 2012/2013:

Mradi wa Kudhibiti Kichaa cha Mbwa ulifanikiwa kutekeleza mambo yafuatayo:-

- Jumla ya mbwa 11,138 na paka 3,458 walipata chanjo dhidi ya ugonjwa wa kichaa cha mbwa;
- Jumla ya mbwa 445 na paka 680 wamefungwa uzazi;

• Jumla ya paka na mbwa 2,749 walipatiwa matibabu ya maradhi mbali mbali. Vile vile mbwa na paka 7,195 walipatiwa dawa za minyoo, pia jumla ya 1,832 paka na mbwa waliogeshwa na mbwa 467 walipatiwa chanjo ya distemper. • Jumla ya wafugaji 70 wamepatiwa taaluma juu ya utunzaji bora wa mbwa na paka ili kuepukana na maradhi ya kichaa; • Maabara zimeboreshwa kwa kupatiwa madawa ya tiba na vifaa mbali mbali vya upasuaji (kufunga uzazi) pamoja na kufanya matengenezo ya mafriji 4; na • Kampeni ya mbwa na paka dhidi ya kichaa cha mbwa vijijini imefanyika kwa kurusha vipindi vya radio (Zenj FM na HIT FM) na TV.	
Fedha zilizotengwa 2013/2014	Jumla ya shilingi 60,000,000 kutoka SMZ za TZS 100,000,000 kutoka kwa Mshirika wa maendeleo zimetengwa kutekeleza malengo ya Mradi
Malengo ya Mwaka 2013/2014 ya mradi ni kama yafuatayo: • Kutoa taaluma mashuleni, viongozi wa jamii, kutayarisha vipeperushi na kutoa vipindi (radio, tv na magazeti) juu ya athari ya ugonjwa wa kichaa cha mbwa. • Kukusanya takwimu (demography) za idadi ya mbwa na paka waliopo Unguja. • Kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa watendaji wa mifugo/maabara kukabiliana na kichaa cha mbwa; • Kutekeleza kampeni ya chanjo dhidi ya kichaa cha mbwa katika Wilaya zote za Unguja; • Kukarabati maabara ya Maruhubi, kuiwekea vifaa na madawa ya kufanyia uchunguzi wa maradhi ya kichaa cha mbwa/paka waliopo ndani na kutoka nje ya nchi; na • Kutekeleza kampeni ya tiba na kuwafunga uzazi mbwa na paka katika Wilaya zote za Unguja.	

KIAMBATANISHO NAM. 8: MRADI WA USIMAMIZI WA MAZINGIRA YA BAHARI NA UKANDA WA PWANI (MACEMP)

JINA LA MRADI	**MRADI WA USIMAMIZI WA MAZINGIRA YA BAHARI NA UKANDA WA PWANI (MACEMP)**
MUDA WA MRADI	Umeanza: Februari 2006 Hatua za ukamilishaji wa Mradi zilianza 31 Agosti 2012 hadi Februari 2013.
JUMLA YA GHARAMA: US DOLA MILLION 61, **ZANZIBAR (40%): 25,906,737.31** **BARA (60%):**	
Lengo Kuu la Mradi wa MACEMP	Kuimairisha matumizi endelevu ya bahari kuu na bahari ya maji madogo, kuimarisha ukusanyaji mapato yatokanayo na uvuvi, kupuguza hatari za uharibifu wa mazingira, kuinua hali ya maisha ya wanajamii wanaoishi katika wilaya zilizo katika ukanda wa pwani. Pia mradi umelenga kuimarisha miundo mbinu na utendaji wa taasisi zinazotekeleza maradi
Gharama kwa mwaka 2012/2013	Jumla ya shilingi 100,000,000 kutoka SMZ zilitengwa kutekeleza Kazi za Mradi.

Malengo ya Mwaka 2012/2013 ya mradi ni kama yafuatayo:

- Kuendelea kutangaza mafanikio ya mradi ndani na nje ya nchi;
- Kuandaa ripoti ya ukamilishaji wa mradi (Implementation completion report);
- Kukamilisha malipo ya mafunzo kwa wanafunzi wa mwaka wa mwisho waliopo ndani na nje ya nchi;
- Kuratibu na kufuatilia miradi midogo midogo iliyobuniwa na wananchi wenyewe pamoja na kuweka matumbawe ya kienyeji;
- Kufanya malipo ya mwisho ya washauri elekezi pamoja na zabuni zilizokuwa hazijalipwa;
- Kuendelea na kuimarisha maeneo mapya ya hifadhi;

- Kuendelea kusafisha matumbawe ya baharini;
- Kuendelea na vikao mbalimbali vya wadau wa mradi;
- Kuendeleza mchakato wa kuanzishwa mfuko wa bahari (MLF); na
- Kuendelea na mazungumzo na wadau mbalimbali kuhusiana na upatikanaji wa miradi mbadala.

Utekelezaji Halisi 2012/2013:

- Mafanikio ya Mradi yametangazwa kwa njia mbali mbali zikiwemo magazeti ya ndani na ya nje ya nchi. Pia njia za mitandao zimetumika (mcu.go.tz/World_Bank_MCU.php na mcu.go.tz/MACEMP/). Jarida la biashara gazeti la Zanzibar Chamber of Commerce, Tanzania Review 2012/13, commercial directory 2012/13, vipindi vya TVZ na redio, Mikutano ya Kimataifa, Ziara za Kimasomo nje China, Sri lanka Mauritius, maldives, Kenya, n.k.;
- Ripoti ya ukamilishaji wa Mradi imekamilika na Kazi hii ilifanywa na mradi mshauri muelekezi Dr. Kofi Amponsah. Taarifa muhimu zikiwemo vigezo vya mradi (indicators) zimeshafanyiwa kazi;
- Jumla ya wanafunzi 18 wa mafunzo mafupi na ya muda mrefu kutoka ndani na nje ya nchi wamelipiwa gharama za masomo yao;
- Miradi midogo midogo iliyobuniwa na wananchi wenyewe imefuatiliwa pamoja na kuendelea na utayarishaji wa matumbawe ya kienyeji na kufanya ufuatiliaji ‘ patrols’ katika sehemu za hifadhi;
- Kazi za washauri welekezi ambazo ni pamoja na ICR, legal Institutional frame work, coastal marine development plan na M&E zote zimekamilika na malipo yao yamefanyika;
- Maeneo ya hifadhi ya CHABAMCA, TUMCA, na KIMCA yameekewa ‘coordinates’ na hivi sasa yanasubiri kanuni zikamilike ili yawe maeneo rasmi ya hifadhi. Vile vile taaluma za uhifadhi endelevu zinatolewa kwa wavuvi pamoja na kuimarisha kamati za wavuvi ili waweze kujua majukumu yaona wawee kusimamia wenyewe;
- Zoezi la kusafisha matumbawe limefanywa kwa kushirikiana na kampuni ya Scuba-Do na Wavuvi ili kuondoa vipande vya nyavu na matukambe;

• Katika hatua ya ukamilishaji wa mradi Vikao mbali mbali vikiwemo vya Benki ya dunia Wizara ya Fedha URT na Zanzibar vimefanyika wakati wa ufuatiliaji wa kazi za ukamilishaji wa mradi ICR amabpo taasisi zote muhimu zimejumuishwa katika mikutano; • Kazi ya awali ya utafiti kuhusu kuanzishwa kwa Mfuko wa Bahari (MLF) yameshawasilishwa serikalini kwa mazingatio. Utafiti ulifanywa na mtaalam David Meyers; na • Wizara ya Mifugo Zanzibar kwa kushirikiana na Wizara ya mifugo Tanzania bara imewasilisha Benki ya Dunia azma ya kuanzishwa kwa Mradi wa Uvuvi wa Ukanda wa magharibi mwa Bahari ya Hindi (South West Indian Ocean Fisheries Program – SWIOFish) Vikao mbali mbali vya kujadili muelekeo wa Mradi , Kazi zake na mipango ya utekelezaji vimeshafanyika.	
Gharama kwa mwaka 2013/14	MRADI HUU UMEKAMILIKA FEBRUARY 2013

KIAMBATANISHO NAM. 9: MRADI WA KUIMARISHA UVUVI WA KINA KIREFU CHA MAJI.

JINA LA MRADI	Mradi wa Uvuvi wa Bahari Kuu
MUDA WA MRADI	Miaka minne
JUML A YA GHARAMA	USD 22,323,529
LENGO KUU LA MRADI	Kuwawezesha vijana kuvua katika maji ya kina kirefu
FEDHA ILIYOTENGWA 2012/2013	Tshs 300,000,000
MALENGO YA MWAKA 2012/2013: • Kuendesha mafunzo kwa vijana 60 kuvua katika bahari kuu; • Kufanya doria ndani na nje ya maeneo ya hifadhi; • Kutoa taaluma juu ya uvuvi haramu; na • Kuvunja jengo la ZAFICO Malindi.	
UTEKELEZAJI HALISI 2012/2013 • Doria ilifanyika ndani na nje ya maeneo ya hifadhi ili kuyalinda na uharibu dhidi ya uvuvi haramu na uharibu mwengine wa kimazingira.	
FEDHA ILIYOTENGWA 2013/2014	Tshs 100,000,000
MALENGO YA MWAKA 2013/2014: • Kubomoa jengo kongwe la ZAFICO Malindi; • Kuendesha mafunzo ya uvuvi wa kina kirefu cha maji kwa vijana 30; na • Kukimu mahitaji ya vyombo vitavyonunuliwa kupitia Mradi wa Ajira kwa Vijana ili kuvua maji ya kina kirefu.	

KIAMBATANISHO NAM.10: MRADI WA KUIMARISHA UFUGAJI WA MAZAO YA BAHARINI

JINA LA MRADI	**MRADI WA KUIMARISHA UFUGAJI WA MAZAO YA BAHARINI**
MUDA WA MRADI	2012/2013 – 2014/2015
JUMLA YA GHARAMA	Gharama za mradi huu hupangwa kila mwaka na kuidhinishwa na mfadhili na Serikali
LENGO KUU	Kuimarisha ufugaji wa samaki na mazao mengine ya baharini
Fedha zilizotengwa 2012/2013	Jumla ya shilingi 78,000,000 kutoka Serikalini (SMZ) na dola za kimarekani 470,000 kutoka kwa washirika wa maendeleo zilitengwa kutekeleza Mradi huu kwa mwaka wa fedha 2012/2013.
Malengo ya Mwaka wa fedha 2012/2013: Mradi huu ulikuwa na malengo yafuatayo: • Kuainisha maeneo ya baharini yanayofaa kwa ufugaji wa samaki kwa kutumia vizimba; • Kukusanya taarifa za kimazingira za maeneo husika na aina za samaki wanaofaa kufugwa katika maeneo hayo; na • Kujenga uwezo wa wafanyakazi katika kuendeleza ufugaji wa mazao ya baharini.	
Utekelezaji halisi wa mradi katika mwaka 2012/2013 ulikuwa kama ifuatavyo: • Uchambuzi ya kinifu wa kuyatambua maeneo ya baharini yanayofaa kwa ufugaji wa samaki na mazao mengine ya baharini kwa kutumia vizimba umekamilika na maeneo hayo yameweza kuainishwa. Maeneo hayo ni Tumbatu (baina ya Kisiwa cha Tumbatu na kisiwa cha Unguja); Menai Bay (baina ya Bweleo na Kikungwi), Tumbe; baina ya kisiwa cha Fundo na kisiwa cha Pemba (Wete); Eneo la kaskazini mwa Ras Mkumbuu; Eneo la kusini mwa Ras Mkumbuu (Wesha); Wambaa; baina ya kisiwa Panza na kisiwa cha Pemba; • Kazi ya Ukusanyaji wa taarifa za kimazingira za maeneo husika na aina za samaki wanaofaa kufugwa katika maeneo hayo imefanyika, pamoja na kulipima na kuwekewa alama (beacons) 6 eneo la ukubwa wa	

ekari 5 linalotarajiwa kujengwa kituo cha kutotolea vifaranga huko Mkokotoni Mkoa wa Kaskazini Unguja na Tumbe Kisiwani Pemba; na • Katika kujenga uwezo wa wafanyakazi katika kuendeleza ufugaji wa mazao ya baharini, jumla ya wataalamu 6 wa mazao ya baharini walihudhuria mafunzo ya wiki mbili juu ya mbinu bora za ufugaji wa samaki na mazao mengine ya baharini huko nchini Korea. Aidha, vifaa kama vile (Current profiler 1, Do, salinity, Temperature, PH meter 1 na Handheld GPS 1) vimenunuliwa. Pia jumla ya pikipiki 4 kwa ajili ya ufuatiliaji wa kazi za ufugaji wa mazao ya baharini vijijini zimenunuliwa.	
Fedha zilizotengwa 2013/2014	Jumla ya shilingi 100,000,000 kutoka SMZ na dola za kimarekani 353,000 kutoka kwa washirika wa maendeleo zimetengwa kutekeleza mradi kwa mwaka wa fedha 2013/2014.
Malengo ya mwaka wa fedha 2013/2014: • Kuimarisha mazingira ya utendaji kazi; • Kuongeza uzalishaji wa samaki, mwani na mazao mengine ya baharini; na • Kujenga uwezo wa wafanyakazi katika kuendeleza ufugaji wa mazao ya baharini.	

Kiambatanisho nam 11 : MAPATO YALIYOKUSANYWA KWA KIPINDI CHA JULAI 2012 HADI APRILI 2013 NA MAPATO YANAYOTARAJIWA KUKUSANYWA KWA MWAKA 2013/2014

KASMA	MAELEZO	MAKADIRIO 2012/2013	MAPATO HALISI JULAI 2012 HADI APRIL 2013	
	AFISI KUU PEMBA			
142259	ADA YA UTABIBU WA VINYAMA	12,000,000	6,266,300	
142228	LESENI ZA UVUVI	6,000,000	4,283,500	
142229	ADA ZA MAZAO YA BAHARINI	21,000,000	5,233,500	
142290	MAPATO YA MIFUGO	6,000,000	1,371,000	
	JUMLA NDOGO	**45,000,000**	**17,154,300**	
	IDARA YA UTABIBU WA MIFUGO			
142259	ADA YA UTABIBU WA VINYAMA	59,000,000	37,009,100	
	IDARA YA MAENDELEO YA UVUVI			
142228	LESENI ZA UVUVI	30,000,000	14,085,800	
	IDARA YA MAZAO YA BAHARINI			
142229	ADA ZA MAZAO YA BAHARINI	70,000,000	65,219,050	
	IDARA YA UZALISHAJI MIFUGO			
142290	MAPATO YA MIFUGO	9,000,000	2,245,000	
	JUMLA NDOGO	**168,000,000**	**118,558,950**	
	JUMLA WIZARA	**213,000,000**	**135,713,250**	
	LESENI ZA UVUVI WA BAHARI KUU	2,077,000,000	146,560,000	
	JUMLA KUU	**2,290,000,000**	**282,273,250**	

Kiambatanisho nam 12: MATUMIZI YA KAZI ZA MAENDELEO KUANZIA JULAI 2012 HADI APRILI 2013

IDARA / MRADI	SMZ		WASHIRIKA WA MAEN	
	MAKADIRIO 2012/2013 (A)	FEDHA ZILIZOPATIKANA July – April 2013 SMZ (B)	MAKADIRIO 2012/2013 (C)	FED ZILIZOP NA July 2013
HUDUMA ZA UTABIBU WA MIFUGO				
MRADI WA KUDHIBITI KUCHAA CHA MBWA	80,000,000	13,000,000	69,960,000	158
MRADI WA MAGONJWA YASIYO NA MIPAKA	80,000,000	10,310,000		
UZALISHAJI MIFUGO				
MRADI WA UPANDISHAJI NG'OMBE KWA SINDANO	122,000,000	116,065,000		
MIPANGO, SERA NA UTAFITI				
MRADI KUIMARISHA MIUNDOMBINU YA MIFUGO	200,000,000	32,000,000		
MAENDELEO YA UVUVI				
MRADI WA HIFADHI YA MAZINGIRA ZA BAHARI NA UKANDA WA PWANI (MACEMP)	100,000,000	30,000,000		
MAZAO YA BAHARINI				
MRADI WA KUIMARISHA	78,000,000	14,190,000	733,200,000	733

IDARA / MRADI	SMZ		WASHIRIKA WA MAE	
UFUGAJI WA MAZAO YA BAHARINI				
JUMLA KUU	**960,000,000**	**224,565,000**	**803,960,000**	**89**

Kiambatanisho nam 13: MUHTASARI WA MAKADIRIO YA BAJETI KWA KAZI ZA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA 2013/2014

IDARA	MRADI	
MIPANGO, SERA NA UTAFITI	Kuimarisha Miundombinu ya Mifugo	
HUDUMA ZA UTABIBU WA MIFUGO	Kudhibiti Mafua ya Ndege	
	Kudhibiti Kichaa cha Mbwa	
UZALISHAJI MIFUGO	Kupandisha Ng'ombe kwa Sindano	
MAZAO YA BAHARINI	Kuimarisha Ufugaji wa Samaki	
	Kuimarisha Uvuvi wa Bahari Kuu	
JUMLA		

Kiambatanisho nam 14: MAKADIRIO YA MATUMIZI KWA MWAKA 2012/2013, FEDHA ZA KAZI ZA KAWAIDA KUANZIA JULAI 2012 HADI APRILI 2013

KASMA	IDARA	MAKADIRIO 2012/2013			FEDHA ZILIZ AP	
		MISHAHARA	MATUMIZI MENGINEYO	JUMLA YA MAKADIRIO	MISHAHARA	MATUMIZI MENGINEYO
03	**AFISI KUU PEMBA**	**520,500,000**	**389,806,000**	**910,306,000**	**425,881,850**	**154,250,663**
02	MIPANGO, SERA NA UTAFITI	73,327,000	165,674,000	239,001,000	55,003,650	77,000,000
04	UENDESHAJI NA UTUMISHI	340,612,000	244,800,000	585,412,000	303,933,084	138,235,088
06	HUDUMA ZA UTABIBU WA WANYAMA	508,630,000	120,000,000	628,630,000	397,998,400	64,000,000
08	UZALISHAJI WA WANYAMA	452,500,000	119,000,000	571,500,000	361,163,450	70,500,000
07	MAZAO YA BAHARINI	112,405,000	94,248,000	206,653,000	94,927,000	48,000,000
016	MAENDELEO YA UVUVI	297,026,000	90,472,000	387,498,000	249,639,250	49,500,000
	JUMLA UNGUJA	**1,784,500,000**	**834,194,000**	**2,618,694,000**	**1,462,664,834**	**447,235,008**
	JUMLA KUU	**2,305,000,000**	**1,224,000,000**	**3,529,000,000**	**1,888,546,684**	**601,485,751**

Kiambatanisho nam 15: MAKADIRIO YA FEDHA ZA MATUMIZI YA KAWAIDA KWA MWAKA 2013/2014

IDARA	MAKADIRIO YA KAZI ZA KAWAIDA F 2014		
	MISHAHARA	**MATUMIZI MENGINEYO**	
UNGUJA:			
MIPANGO SERA NA UTAFITI	73,328,000	132,698,000	
UENDESHAJI NA UTUMISHI	352,723,000	349,045,000	
HUDUMA ZA UTABIBU WA MIFUGO	510,829,000	94,769,000	
UZALISHAJI MIFUGO	452,689,000	112,948,000	
MAZAO YA BAHARINI	112,405,000	86,340,000	
MAENDELEO YA UVUVI	297,026,000	82,500,000	
JUMLA UNGUJA	**1,799,000,000**	**858,300,000**	
AFISI KUU PEMBA:			
MIPANGO SERA NA UTAFITI	-	51,200,000	
UENDESHAJI NA UTUMISHI	527,000,000	73,500,000	
HUDUMA ZA UTABIBU WA MIFUGO	-	70,000,000	
UZALISHAJI MIFUGO	-	73,000,000	
MAZAO YA BAHARINI	-	76,500,000	
MAENDELEO YA UVUVI		82,500,000	
JUMLA PEMBA	**527,000,000**	**426,700,000**	
JUMLA KUU	**2,326,000,000**	**1,285,000,000**	

Mhe. Spika: Hizi *speed* naona zinatofautiana, hii ya leo. *(Vicheko).*

Mhe. Waziri tunakushukuru na hoja imeungwa mkono, mjadala utaanza kesho. Waheshimiwa Wajumbe, kuna matangazo mawili. Tangazo la kwanza Waheshimiwa Wajumbe wanawake wanaombwa na Mwenyekiti wao wabakie kidogo baada ya kuondoka humu ndani.

Tangazo la pili, nimeombwa niwatangazie Waheshimiwa Wajumbe wote kwamba yale mazoezi yetu ya kawaida na hasa maalum kwa ajili ya safari ya kimichezo Arusha yameanza. *(Makofi).*

Safari hiyo ya Arusha inategemewa kuwa baada ya kumalizika kwa mwezi mtukufu wa Ramadhani. Tunategemea kwenye majaaliwa itakuwa kwenye tarehe 22/08/2013. Hiyo ndio siku ya safari ya michezo kwenda mjini Arusha. Tangazo hili limeletwa na Meneja Msaidizi Mhe. Nassor Salim Ali. *(Makofi).*

Waheshimiwa Wajumbe baada ya hayo machache na kwa mashirikiano makubwa niwashukuruni. Sasa niakhirishe kikao hiki mpaka kesho tarehe 25/07/2013 saa 3:00 barabara za asubuhi.

(Saa 8:00 mchana Baraza liliakhirishwa mpaka
tarehe 25/07/2013 saa 3:00 za asubuhi)